Maswali Na Majibu Juu Ya Mihuri

[Ndugu mmoja ananena kwa lugha. Ndugu mwingine anafasiri. Kusanyiko linaomba kwa sauti kubwa.—Mh.]

Baba yetu wa Mbinguni, tunashukuru sana kwa ajili ya wakati huu ambapo twaweza kushiriki tena kwenye Neno la Mungu, Machoni pa Mungu. Tunashukuru sana ya kwamba Wewe u pamoja nasi, asubuhi hii, kutusaidia na kutubariki. Twaomba msamaha wa dhambi zetu, ili taa zetu zipate kujazwa na Mafuta, na kutengenezwa na ziwe zinawaka, ili Wewe upate kututumia sasa kulitukuza Jina Lako kuu. Kwa maana tunaomba hayo katika Jina la Mwana mpendwa wa Mungu, Yesu Kristo. Amina.

Mnaweza kuketi.

2 Nilikuwa ndio tu ninaingia wakati niliposikia ujumbe huo ukitolewa. Kwa hiyo mimi . . . Ni kweli kwamba inatubidi kujaza taa zetu wakati wote, kudumisha ninii zetu . . . Unajua, wakati ninii . . . Wakati mtu unawaka, huwezi kuendelea kutegemea kile ulichokwisha kutenda sasa. Unaona? Kwa sababu, moto, unaowaka kwa mafuta, hufanya kaboni. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu kule kutengenezwa kwa . . . zitengenezeni taa zenu, kwa sababu ya ile kaboni iliyoko juu kwenye ya—ya utambi. Wengi wenu ninyi watu wa rika langu, wakati tulipokuwa tukitumia taa—taa ya mafuta ya makaa ya mawe, unaona, zili- . . . Inge—inge—ingepata kaboni hapo juu, pale ambapo ingewaka, na kwa hiyo ingezuia mwanga. Kwa hiyo inakulazimu kukata kuondoa kaboni yote, na ili kwamba "tukaze mwendo, tuifikilie mede ya thawabu ya wito mkuu katika Kristo."

3 Sasa, ni—ni asubuhi nzuri sana ipendezayo, nje na ndani, kwa kuwa majira haya ya Pasaka yanakaribia sasa.

4 Na—na sasa tunakaribia ule Muhuri wa mwisho, usiku huu, Bwana akipenda. Na ni Muhuri wa kisiri sana, sana, sana, kwa sababu hata hauta- . . . Hata hautajiwi katika Maandiko mahali po pote, hakuna mifano, hauna cho chote cha kushikilia. Hauna budi kuja moja kwa moja kutoka Mbinguni.

5 Na kwa namna fulani ni—ni ninii—ni saa ya uchovu wa akili kwangu. Imekuwa hivyo, juma zima. Sasa hii ni ninii yangu—itakuwa ni siku yangu ya nane ndani ya chumba. Nami niliona katika haya, mengi, katika maombi haya, . . . ilinibidi kwa namna fulani kuyachagua. Kulikuwa na watu wengi waliokuwa wakitaka mazungumzo ya faragha. Nami na—napenda jambo hilo. Ningetaka ku—kutimiza hilo sasa, unaona,

lakini siwezi kwa sasa hivi. Kwa sababu, mwaelewa, ya kwamba yo—yote yale tunayojaribu kufanya sasa ni kupata ufunuo wa mapenzi ya Bwana, mnaona. Kisha tutakuwa na mazungumzo ya faragha, ndipo yanakuondoa, kukupeleka upande mwingine kwa jambo lingine, unaona.

6 Na, hivyo basi, na kama vile katika maombi ya kuombea wagonjwa, hilo ni jambo tofauti kabisa. Wewe. . .Ni maono na kadhalika; unasoma kwa ajili ya jambo la tofauti, na umeninii—umetiwa upako kwa ajili ya kitu cha tofauti. Ni kama tu vile Biblia ilivyosema pale, "M—mti uliopandwa kando kando ya vi—vijito vya maji." "Vijito vya maji," unaona, maji yale yale, lakini kuna mkondo unatokea upande *huu*, upande *huu*, na upande *huu*. Inategemea ni kwenye kijito kipi. Ni Roho yule yule.

7 Paulo, I Wakorintho 12, alisema jambo lile lile, alinena kuhusu, "Kuna karama nyingi, lakini ni Roho yule yule."

8 Kwa hiyo, unaona, kama unatenda kazi, tuseme, na kitu kimoja, halafu ugeuzwe kujia kitu hiki kingine *hapa*. Unajua ninalomaanisha. U—ukisoma katika mwelekeo huo, utawafanya watu. . .Na sasa mioyo yao imeelekezwa kabisa, iko tayari, "Mihuri hii ni nini?" Matazamio yao, "Ni nini?" Usiku baada ya usiku niingiapo humu ndani, kuna wasiwasi sana, mpaka ninalazimika kuongea juu ya jambo lingine; ili kwa namna fulani nipate—nipate kuutuliza, unaona, na, basi, mpaka Roho Mtakatifu atakapovunja huo Muhuri. Na ndipo—ndipo kufanya hivyo, yanibidi kila usiku namna hiyo. Basi tunapogeuza jambo hilo kwa uponyaji ama kitu fulani, unaona, wewe. . .Watu wameelekea kwenye jambo moja. Ni vigumu kubadilisha kurudi kwenye lile lingine, mara moja.

9 Na—na tena, pia, tukijua ya kwamba papo hapo kati yenu, mambo yanatendeka, unaona, ya kwamba mimi—mimi ninaninii tu. . .Na—najua. Najua ha—hamyaoni, unaona. Nina hakika hamyaoni, unaona. Nanyi mnasema, "Ndugu Branham, hilo ni jambo gumu kwako kusema jambo hilo." Najua ni gumu.

10 Lakini, tazama, hebu ngoja niseme tu jambo hili sasa. Nafikiri hizi ni kanda kwa ajili ya sisi wenyewe, na kadhalika. Lakini hebu niseme jambo hilo, mnaona. Ya kwamba, ham—hamninii. . .hamlipati, mnaona, na hampaswi kulipata. Kwa hiyo msijaribu kutafsiri cho chote, mnaona. Usijaribu kuweka tafsiri yako mwenyewe kwa hilo; unaninii tu—unaenda tu mbali zaidi. Chukueni tu ushauri wangu, iwapo mnaniamini sasa, iwapo Mungu ame—amenipa kibali machoni penu.

11 Nanyi mnajua, ya kwamba, hayo mafunuo na kadhalika. Ni—nimekuwapo hapa pamoja nanyi kwa muda mrefu, mnaona, na kila mara yamekuwa sahihi. Na sasa ili kuthibitisha hilo maradufu, moja kwa moja, yanaambatana moja kwa moja na Neno. Mnaona? Kwa hiyo, ninyi mnajua ni BWANA ASEMA HIVI. Hilo ni kweli kabisa. Mnaona, limethibitishwa kwenu.

12 Sasa shikeni shauri langu, kama ndugu yenu. Msiweke tafsiri yenu binafsi kwa cho chote. Endeleeni tu na mwishi maisha mema ya Kikristo. Kwa sababu, utajizongazonga na jambo lililo halisi ukifanya hivyo. Unaona? Utaninii, utaenda mbali tena tu na kitu chenyewe.

13 Na ninyi nyote mnafahamu na mnajua ya kwamba kuna kitu fulani cha siri kinachotendeka. Na kinatendeka. Nami najua hicho ni kitu gani. Sasa, sijisemi tu jambo hilo; ni neema ya Mungu inayonifanya nijue ni kitu gani. Ni kitu fulani kilicho cha ajabu sana. Na kimeondoka sasa hivi, wala hakuna njia kamwe kwenu kukiona. Na ni . . . Mimi . . . Lakini hivyo na anisaidie, nikiwa nimeshika Biblia hii mkononi mwangu, najua hicho ni nini. Mmeambiwa, habari Zake hapo nyuma. Kwa hiyo hebu tu—hebu tu msijaribu kuweka tafsiri yo yote, lakini niaminini tu, kama ndugu yenu. Mnaona? Tunaishi katika saa yenye mambo makubwa. Tunaishi katika wakati ambapo ile . . . Vema, tuna- . . .

14 Sasa, wewe uwe tu mnyenyekevu sana, uwe Mkristo, na ujaribu kumwishia Mungu. Na uishi mwaminifu kwa mwenzako, na uwapende wale wasiokupenda. Usijaribu kufanya kitu cho chote . . . Unaona, ukijaribu, unakifanya tu kuwa kitu fulani kisichoeleweka, na kuvuruga ule mpango halisi wa Mungu. Unaona?

15 Jana alasiri, jambo fulani lilitendeka chumbani mwangu, ambalo nita—sitaweza kamwe ku—kusahau, unaona. Na kwa hiyo ninyi . . . Na yapata majuma mawili yaliyopita, jambo fulani lilitendeka, halitaweza kamwe . . . Kadiri niishivyo humu duniani, si—sitaweza kuondokana nalo kamwe, unaona. Na, kwa hivyo, lakini . . .

16 Na ka—kanisa, hampaswi kuyajua mambo haya, kwa hivyo msiweke tafsiri yo yote kwa cho chote. Mnaona. Endeleeni tu na mkumbuke tu mnayoambiwa. Ishini maisha ya Kikristo. Hudhuria kanisa lako. Uwe mwanga halisi po pote ulipo, na uwakewake tu kwa ajili ya Kristo, na uwaambie watu jinsi unavyompenda Yeye. Na hebu tu ushuhuda wako ufanyike kwa upendo, wakati wote, kwa watu. Unaona? Kwa sababu, usipofanya hivyo, utapotoka uingie kwenye jambo fulani huko nje, na ndipo ume—umeondoka kwenye njia iliyo halisi. Unaona, kila wakati ulipojaribu kufanya jambo hilo, umefanya hivyo. Unaona? Kwa hiyo usininii tu, usininii, usijaribu kufanya tafsiri yo yote.

17 Na hasa, usiku wa leo, wakati huo Muhuri utakapokuja mbele yenu, unaona, usijaribu kabisa kuutafsiri. Wewe endelea tu na uwe mnyenyekevu tu, uendelee tu na Ujumbe ule ule ulio rahisi.

18 Sasa unasema, “Ndugu Branham, je, hiyo ni . . . Sisi, tukiwa ndio Kanisa la Mungu ailiye hai, je, tusininii . . . ?” Vema, kama

nilivyokuwa nikijaribu. . .Tazama hapa, nataka kusema. . . Kusema, "Vema, je! kwa nini nisifasiri? Yabidi nipate. . . " La. Sasa, usifasiri.

19 Kumbukeni, nasema hili kwa manufaa yenu. Mnaona, ninasema jambo hili kusudi mfahamu. Kama mnaniamini mimi, sasa, sikilizeni yale ninayowaambia. Unaona? Unaona?

20 Sasa, hapa, sasa hapa pana kituo, na, hicho ni, tutakiita hicho kwamba ni kituo cha kusikilizia, unaona. Na katika ninii yake, kina redio, unaona, na kuna maonyo na mambo mengi yanayoweza kutangazwa. Kama vile upanga mkononi mwako, unaona, kinaweza kunasa kutoka kwenye uovu au kunasa kutoka kwa jinsi vile tu. . . tu. . .kinavyopata ujumbe wake, unaona.

21 Sasa, lakini sasa, kwa mfano, kwa mtu wa kawaida, kumekuwa na madhehebu mengi sana na vikundi vya dini vilivyoinuka, kutokana na umwagika kudogo kwa Roho, mpaka watu wamechangamka sana katika lundo la upuuzi, wanaondoka wanaenda na kuanzisha kundi lingine dogo, na, mnajua, na kadhalika. Mnaona? Hamtaki kufanya jambo hilo sasa. Mnaona? Sasa, kumbukeni tu, dumuni tu jinsi vile mlivyo.

22 Nanyi mnasema, "Vema, Bwana alinionyesha. . . " La. Sasa iweni tu waangalifu.

23 Angalieni hapa. Hebu niwaonyesheni jambo fulani, mnaona. Je! mlijua kuwa kuna kumi elfu za sauti katika chumba hiki sasa hivi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Halisi, sauti za watu ambazo zinaingia kupitia kwenye mawimbi ya elektronia ya redio! Mbona hamzisikii? Ni sauti. Sivyo? ["Amina."] Zinapita mumu humu kwa mawimbi sasa. Kuna viwiliwili na miili ya watu inayopita humu chumbani sasa. Sivyo? ["Amina."] Vema, mbona hamuwaoni? Mnaona? Ziko hapa, sauti halisi kama sauti yangu. Vema, kwa nini hamwisikii? Mnaona? Haina budi kugusa kitu fulani kwanza, ipate kufunuliwa. Unaona? Sasa mnaelewa? ["Amina."]

24 Sasa usitafsiri tu cho chote. Mungu akitaka ujue cho chote, Yeye atakituma kwako. Unaona? Kwa hiyo uwe imara, imara sana sasa. Tulieni. Jambo fulani limetendeka. Na sasa iweni sana tu. . .Mnaelewa ninalomaanisha, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Na mwe tu. . .Usijaribu kujifanya mtu wa kipekee, ili uwe Mkristo, kwa sababu uta—utajiondoa mwenyewe kwa Mungu. Na wewe—wewe—wewe. . .

25 Kama mnaweza kufahamu jambo hilo, huu ndio ule Mvuto wa Tatu. Mnaona? Mlipaswa kuwa mmelipata jambo hilo, hivi majuzi. Mnaona? Kwa hivyo basi, kumbukeni tu, hakutakuwako na kuigiza kama ilivyokuwa katika ile mingine miwili. Unaona? Kwa hiyo, huo ndio umbali tu mnao—mnaopaswa kujua sasa. Kumbukeni tu—kumbukeni tu ya kwamba. . .

26 Mnaona, sasa, kuna jambo fulani linalotendeka humu chumbani, na kuna Jambo fulani hapa. Kuna—kuna, kwa kweli, katika chumba hiki, Malaika, Sauti ya Mungu. Unaona? Lakini unawezaje . . . Huwezi . . . Kama huwezi kusikia sauti ya kawaida, pasipo kitu fulani cha kuitoa, utawezaje kusikia Sauti ya kiroho?

27 Sasa waweza kujifanya uamini ya kwamba mtu fulani anaimba wimbo fulani *huu*. Huenda hata wasiwepo, unaona. Lakini igusapo ile fuwele ambayo inapaswa kugusa, basi inatoa tafsiri halisi, na kuonyesha, na kuthibitisha jambo hilo kwa kuonyesha hiyo picha. Mnaona ninachomaanisha? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.]

28 Sasa, Roho ya Mungu, inaponena kupitia katika lile Neno la kweli, inajithibitisha Yenyewe, kujionyesha Yenyewe, ya kwamba ni sahihi. Mnaelewa sasa? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Vema.

Sasa hebu na tuombe, tena tu.

29 Baba wa Mbinguni, tuko karibu ku- . . . -fungua vifuniko vya Kitabu hiki, na kama sehemu inayoonekana ya—ya kujaribu kurudisha kile ulichotufungulia katika mazingira ya kiroho. Na sasa naomba, Mungu, ya kwamba utanisaidia mimi kutoa tafsiri iliyo sahihi kwa maswali haya. Ili iweze kusemwa ya kwamba—ya kwamba ni ya . . . kwa ajili ya kuwasaidia watu. Ni kwa ajili ya kuwapa ufahamu. Nami naomba ya kwamba utanipa ufahamu, ili niweze kuutuma kwa watu Wako, ili waweze kupata ufahamu, ili kwa pamoja tuweze kuishi kwa utukufu na uchaji wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

30 Sasa, nilitaka tu kusema jambo hilo.

31 Nami nilidhani kidude hiki *hapa* kinasimamisha hizo kanda, lakini hapana, unaona. Na hiki ni—ni cha taa ya dawati. Nami nilidhani kidude kinachozima kanda kilikuwa hapa zamani. Lakini niliambiwa niwapungie tu mkono ndugu walio—walio mle ndani kwenye chumba, kile chumba cha kurekodia, nao wangejua ni wakati gani wa kusimamisha kanda, ama wakati gani wazifungulie.

32 Mnaona, kanda hizi zina huduma ulimwenguni kote kila mahali, unaona, kila mahali. Zinaenda katika kila aina ya lugha na kila kitu. Kwa hiyo kuna mambo ambayo tungesema papa hapa, ambayo hatungeyasema mahali pengine, mnaona, na hiyo ndiyo sababu tunaisimamisha.

33 Sasa, kujibu maswali ni jambo la kuangalia. Kwa hiyo, sasa ni-ni- . . . Katika—katika—katika kujibu hili, mengi ya hayo, mengi ya hayo maswali, nje ya . . . Sasa, kila moja . . . Baadhi ya hayo hata hayahusiki na Ujumbe, hata kidogo, lakini nita- . . . ama na Mihuri hata kidogo, lakini nitajaribu kuyajibu. Na walinipa hayo, na kama vile walivyoambiwa. Niliambiwa karibu yote. Ama, sehemu kubwa ya hayo yanahusu haja za maombi,

na wagonjwa na wanaoteseka. Na—na mambo mbalimbali kama hayo, yanaendelea, na kwa hiyo hayakuhusu cho chote kwa swali lo lote la kujibiwa. Na halafu wao. . .Nilipewa lundo ambalo lilikuwa—ambalo lilikuwa juu ya mambo mbalimbali, Maandiko na kadhalika; lakini labda, tukipata muda, tutajaribu kuyajibu vizuri tuwezavyo. Sasa, na kama nikifanya kosa, mbona, kumbukeni, sikusudii kufanya kosa.

34 Kwa hiyo kila mtu anajisikia vizuri? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Amina. Je! hi si ni ninii. . .Nena kuhusu ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu, ni mahali pazuri sana jinsi gani, ni wakati mzuri sana jinsi gani!

35 Katika nyakati zote ambapo nimepata kuwa mimbarani humu Maskanini, sijawahi kamwe, kamwe, katika wakati wo wote wa huduma yangu, kufanya kazi katika mazingira ya Mungu na mazingira ya kiroho kama vile ilivyokuwa wakati huu; zaidi ya jambo lo lote nililowahi kutenda katika wakati wo wote wa huduma yangu, katika mkutano wo wote mahali po pote pale, kama huu. Mara nyingi, huwa ni kuhusu uponyaji. Huku ni kufunuliwa kwa zile Kweli, kwa Roho yule yule, Roho yule yule.

36 Nami ni—nimekuwa peke yangu, kabisa, na nimekuwa nikilala mahali fulani, au kwenda kula mahali fulani. Na nimekuwa tu peke yangu; kwa hiyo umekuwa kweli ni wakati mzuri sana.

37 Na sasa, moja kwa moja, aidha asubuhi, ama asubuhi inayofuata, mimi. . .Labda, kama tunaweza kuwahi kumaliza, nitawaombea tu wagonjwa asubuhi ya leo, ikiwa maswali haya hayatachukua muda mrefu sana.

38 Kwa hiyo ya—yanipasa kukaa peke yangu kwa kitambo kidogo, unaona. Ubongo wa mwanadamu unaweza tu kustahimili kiasi fulani. Unaona? Na unapofikia mahali ambapo unaketi saa moja, umekufa ganzi kwa Uwepo wa Mungu, na ile Nguzo ya Nuru ikining'inia hapo mbele yako, hu—huwezi kuketi hapo kwa muda mrefu sana, unaona. Mwanadamu hawezi, hawezi kuustahimili.

39 Na kwa hiyo, sasa, maswali haya ni mazuri sana. Ninafurahia, na hekima na mambo ambayo watu wanatumia. Sasa, kwa la kwanza. Nami nitajaribu kuyajibu. Na halafu kama ni—nisipolijibu vizuri, vema, ni—nisameheni basi.

40 Na ikiwa una tafsiri ya tofauti, na unaamini ya kwamba wazo lako kuhusu hilo ni sahihi, vema, hebu endelea tu. Hilo halitadhuru, kwa sababu hayako isipokuwa karibu moja au mawili tu ya hayo yanayohusu wokovu. Ni kwamba tu. . .

41 Karibu maswali yote, yameulizwa, upande huu mwingine wa ile dhi-. . .ama juu ya kule Kunyakuliwa kwa Kanisa. Kwa hiyo, mnaona, ni maswali upande huu, ambayo yatatimia na hayana budi kutimia, upande ule mwingine. Sababu, sasa tuko ng'ambo ya ule wakati wa kanisa, katika mafundisho yetu kwenye—

humu kwenye Kitabu. Tumepita, tuko katika ule wakati wa kuitwa kwa wale mia moja na arobaini na nne elfu. Basi, la kwanza hapa:

173. Je! wale wanawali watano wenye busara, wa Mathayo 25, ni watumishi wa—wa Bibi-arusi, ama wao ndio Bibi-arusi? Unaona? Kama hawa wanawali wenye busara ni watumishi wa Bibi-arusi, Bibi-arusi yuko wapi?

42 Unaona, Sasa, nijuavyo mimi kabisa, hawa wanawali watano. . . Walikuwa kumi, mwajua, waliotoka kwenda, unaona. Na huu hapa ni mfano tu, au methali, unaona, ambayo—ambao nitawaeleza. Unaona, walikuwa kumi. Kwa kweli, walikuwa zaidi ya kumi. Hiyo ni hesabu tu iliyotajwa. Lakini, basi, wa—wale wanawali wenye busara walikuwa na Mafuta katika taa zao. Wale wajinga hawakuwa na Mafuta katika taa zao.

43 "Kwa hiyo ikiwa hao kumi hapo, wa Mathayo, kama. . ." Hili ndilo swa—swali la mtu huyo. "Kama hao kumi, hapo, je! hilo lilimaanisha ya kwamba hiyo ingekuwa. . . au hawa watano, hasa, hao wangekuwa watano tu, unaona, watu watano tu?" La, haimaanishi hivyo.

44 Ni mfano tu, wa wale wanawali, unaona, ya yule mwanamwali aliyekwenda akiwa na Mafuta katika taa zao. Wao ni sehemu ya huyo Bibi-arusi. Na nionavyo mimi. . .

45 Ndipo unaona, sasa, ya kwamba wao walikuwa wanawali wa ile zamu ya mwisho. Kupitia katika zile zamu, kulikuwa na zamu saba. Na katika zamu ya saba, usiku wa manane, kama tunavyoufikia sasa, unaona. Sasa katika zamu hii ya usiku wa manane, hawa wanawali waliamka na kutengeneza taa zao, kisha wakaingia; hali wale wanawali waliolala. . .

46 "Sasa sehemu hii hapa, hawa watano," kama hilo ndilo kusudi la swali hilo, ina maana gani, "je! kulikuwa na watano tu?" Na tuna maswali mengi ndani hapa, kuhusu wale—wale elfu saba, na mengineyo. Sasa, hiyo, huo ulikuwa ni mfano tu, sehemu yao. Na wote ambao waliamshwa katika huu wakati wa mwisho hapa, ile zamu ya saba, ambao. . . . "Kama hawakuwapo ila—ila watano walioamka wakati huo, waliohamishwa, wakaingia pamoja na yule Bibi-arusi, na kadhalika, yule Bwana-arusi? Sasa ikiwa wao wenyewe. . . "

47 Hilo halimaanishi watakuwako watano tu. Kwa sababu, wao wanalala, tokea zamani katika zile nyakati zote; kama vile tulivyopitia juma hili, mnaona.

48 Katika siku za—za Paulo, yule malaika wa kanisa lililoko Efeso; Paulo, akianzisha kanisa hili, akiwa mjumbe wake. Kumbuka, Paulo, akianzisha kanisa kule Efeso, akawa mjumbe wa kanisa hilo. Na Roho, aliyekuwa nchini wakati huo, alikuwa Roho wa simba. Na huyo simba ni yule Simba wa kabila la Yuda, ambaye ni Kristo, naye Kristo ni Neno. Paulo, akiwa na

Neno kwa wakati huo! Maelfu walilala katika wakati huo. Sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

49 Ndipo ukaja wakati uliofuata, na wakati kanisa lile lilipotulia katika—katika wakati wa giza, yule Roho wa ndama akatoka; kazi, na bidii, na kujitoa, na kutoa uhai wao. Maelfu mara elfu walilala, chini ya kufia imani na kadhalika. Wanangoja, mnaona.

50 Halafu, na wakati mwingine uliofuata, ule wa Waluteri, ule wakati wa matengenezo. Kuliondokea wenye busara sana, katika ujanja wa mwanadamu. Ukiangalia, mwanadamu alitoka kwenda na huo, na, alipoenda na huo, akaongezea werevu wake mwenyewe. Huo ndio uliomwoza upande ule mwingine, unaona. Unaona? Kama angekaa tu na hekima ya Mungu, kutengeneza tu na kutoka . . . Lakini yeye alifanya nini? Baada ya mtu yule aliyekuwa na ujumbe, Luther; baada ya kifo cha Luther, wakaunda madhehebu ya Kiluteri.

51 Baada ya kifo cha Wesley, wakaunda madhehebu ya Kimethodisti. Unaona? Hapo, unazidi kuendelea namna hiyo. Ina—inaninii tu . . . Inakuwa hivyo. Sasa nataka mwone—mwone—mwone jambo hili, unaona. Sasa mtu fulani angeweza kuuliza kuhusu Mpentekoste, ambaye alikuwa ni ule—ule wakati wa tatu.

52 Unaona, kila mmoja wa zile nyakati ulipata mchovyo tu katika Roho Mtakatifu. Kuhesabiwa haki ni kazi ya Roho Mtakatifu; kutakaswa ni kazi ya Roho Mtakatifu, lakini ubatizo *ni* Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo sababu ilibidi Nabii anayetabiri kushuka. Hakuna mjumbe kwa wakati huo, kwa sababu Roho Mtakatifu alikuja Mwenyewe, katika utimilifu Wake, wa ubatizo.

53 Lakini mwishoni mwa wakati huu, kama vile unavyoishia daima katika zile nyingine, tunaona hapo, basi, mjumbe alitumwa. Na mashaka hayo yote na kadhalika vitawekwa mahali pao namna hiyo, ndipo Unyakuo unakuja kwa Kanisa.

54 Lakini kama vile wengi wanavyopangia mambo yote haya mbalimbali, “Jua kugeuka kuwa giza, mwezi . . .” Wao wanayaweka hayo huku nyuma kabisa katika wakati wa Kikristo. Wanakosa tu kuyaona hayo maswali matatu aliyoulizwa Bwana wetu pale, unaona, hapo Yeye alipowajibu.

55 Sasa, jana usiku, nafikiri hakuna swali kabisa. Tulichukua kila moja ya hayo maswali na kuyaweka barabara kabisa chini ya ile Mihuri. Na Mihuri ni Kitabu kile chote kizima, Chenyewe.

Unaamini jambo hilo, daktari? [Ndugu fulani anasema, “Naam.”—Mh.]

56 Unaona, kitu chote kizima kimefungamanishwa pamoja. Nasi tulichukua yale Yesu aliyosema hapa. Wao waliuliza maswali matatu, unaona, “Mambo haya yatakuwa lini? Ni nini

dalili ya Kuja Kwako? Na nini nini mwisho wa dunia?" Naye akaja moja kwa moja . . . Nasi tuliyachukua, kila moja, chini ya huo, ila mmoja. Huo ulikuwa upi? Ule Muhuri wa Saba. Kwa nini? Mnaona, haujulikani. Hiyo ni sawa. Kila mmoja wa hiyo ulikuja dhahiri kabisa. Niliilinganisha, kikamilifu kabisa, kwenda mbele na kurudi nyuma.

57 Na, mimi, nilipoandika usiku uliopita, na nikaingia humo na kufikia . . . Nilirudi nikaenda kuiangalia mihitasari yangu ya zamani niliyotoa kutoka—kutoka kule nyuma. Vema, niliona ambapo niliweka mmoja katika mahali pa mwingine, namna hiyo. Niliichanganya, nyuma na mbele. Hivyo ndivyo nilivyofanya. Nadhani mlilipata. Ninyi je! mlilipata? Mnaona?

58 Nilikuwa nimeandika hapa yale niliyokuwa niandike upande *huu* mwingine, na nikayaandika *hapa*. Ni—nikaweka yote mawili, 9, 11, ama 9, 6, ama ninii . . . ama 6 na 11, na—na—na 9 na 11, wala sivyo ilivyokuwa. Ilikuwa ni vinginevyo, fungu lililofuata chini yake. Mnaona? Na hivyo ndivyo ilivyokuwa, lile—lile jibu, kati ya tauni na vita, mnaona? Hapo ndipo ilipokuwa.

59 Kwa hiyo nilikuwa na furaha sasa tu! Nilikuwa nikipiga makelele tu kama ni—ninii . . . Nilikuwa nikifurahia changamko kutokana na ufunuo. Kwa hiyo, ni—nililiweka, hili upande huu. Nikiketi pale na penseli, au kalamu ya wino, nami niliandika 11 mahali pote pawili, ambapo haikupaswa kuwa hivyo. Nadhari ilikuwa ni 9 badala ya 11 kwa upande huo mwingine.

60 Lakini sasa je! mliona jinsi ilivyoenda sawasawa kikamilifu? Sasa, msisahau jambo hilo. Ilienda sambamba hadi kwenye ule wa Sita, kisha ikakoma, mnaona. Basi angalia ninii—angalia kule kufunguliwa kwa zile Muhuri; inafikia ule wa Sita, na inakoma. Ni ninii tu, "Kimya Mbinguni," hivyo tu ndivyo ulivyosema, "kwa muda wa nusu saa."

61 Sasa—sasa, katika haya, unaona, mimi . . . Itanibidi kuharakisha na kujibu haya. Kwa sababu, unaona, kila moja la hayo ni mahubiri ya ibada moja, ya muda wa majuma manne unaona katika—katika kila moja, nawe unatoka tu na kuingilia tu jambo lingine. Lakini, si—sikusudii kufanya hivyo, kwa sababu nataka kufikia swali la kila mtu, kadiri niwezavyo.

62 Hawa wanawali, unaona, walikuwa wametokana na . . . hiyo ni sehemu tu ya wao, katika wakati huo, unaona. Kila wakati una wanawali. Unaona? Ule—ule Muhuri . . .

Malaika hulijia kanisa. "Kwa malaika wa kanisa lililoko Efeso, andika." Unaona?

63 Halafu njoo upande huu, basi baada ya kule kuandikia kanisa lile la Efeso, linganisha hilo huku nyuma, Muhuri unafunguliwa. Hivyo ndivyo tu tunavyouleta, kujaribu kuleta kitu chote kizima kwenu, (mnaona ninachomaanisha?), Bwana akipenda.

64 Hao wangepata nini kwanza? Nyakati za Kanisa. Sivyo? Jambo linalofuata—ule ujumbe kwa nyakati za kanisa. Kila mtu analipata hilo waziwazi sasa? Mnaona?

65 Kwanza, tulipata zile nyakati za kanisa, na tukachukua historia, tukaeleza yale mabaraza ya Nikea na mabaraza yaliyotangulia Nikea, na kila kitu ambacho tungeweza kukipata katika historia, na tukaona ya kwamba tafsiri sahihi ya Neno iliambatana kabisa na historia. Na kulileta hadi wakati huu, katika wakati huu wa Laodikia. Na ha—haikubidi kuwa na historia yake; huku ni kuandika historia hivi sasa, mnaona. Hiyo hapo. Na halafu, tukaonyesha yatakayotendeka katika wakati huu.

66 Sasa tunarudi na zile Muhuri, na kufungua huo Muhuri. Mungu anatufungulia huo Muhuri. Huo ni nini? Kwanza, kuna mjumbe, wakati wa kanisa; baadaye ni zile Muhuri Saba.

67 Sasa, tunaona uchafu ulioingia katika wakati wa saba wa kanisa. Lakini ule Muhuri wa Saba haufunui cho chote, kile kitakachotendeka kwake. Unaona? Kwa sababu, mwishoni mwa wakati huo wa kanisa kunapaswa kuje kipawa cha kiunabii kufunua mambo haya. Unaona? Mnaelewa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema. Sasa angalia jinsi kila moja ya Mihuri hiyo . . .

68 Hivyo nikaja hapa, na maswali hayo matatu aliyoulizwa Yesu Kristo, "Ni nini, mambo haya yatatokea lini, 'Halitasalia jiwe juu ya jiwe'? Hili litaangamizwa lini, makao haya makuu ya kidini ulimwenguni, na makao mengine kusimamishwa? Unaona, itakuwa ni lini?" Kupanda farasi kwa mpinga-Kristo! Mnaona? Na ni kitu gani kilichoenda kukabiliana naye? Neno, Neno dhidi ya neno.

69 Ndipo likaishia katika siasa na cho chote kile kinginecho, kisha pakaondokea ile juhudi ya ndama. Mnaona? Hiyo hasa ni ya pili hapa. Na Yesu alisema hivyo, katika Mathayo 24, unaona. Ndipo tukatoka katika hilo, tukaingia kwenye ujanja wa wale watengenezaji, yule Mwenye Uhai mwanadamu aliyetoka akaenda kukabiliana naye. Hayo ndiyo yaliyotendeka. Ndipo tukaja, baadaye, kwenye ule Muhuri wa Nne, wakati mpinga Kristo alipokuwa kusanyiko la vitu vingi, na akapata jina, "Mauti."

70 Sasa tazama aliyosema Yesu, "Naye angemtupa katika mioto, na hata awaue watoto wake." Huyo ni mauti, amepanda farasi. Hao ni Waprotestanti na Wakatoliki pia, chapa ya mauti juu ya kila mmoja wao. Mnaona, "Yeye ataangamizwa pamoja na watoto wake." Kwa hiyo kama unategemea madhehebu yako, heri uyaaache mara moja sasa hivi.

71 Na basi inapofikia kwenye Muhuri wa Saba, Yesu alisimama papo hapo. Akaufungua Muhuri wa Sita, kwa kusema, "Mwezi utageuzwa kuwa damu, na giza na kila kitu." Mambo haya

yatatendeka. Tulikuja papa hapa na kufungua Muhuri wa Sita. Baada ya Muhuri wa Sita kufunguliwa, ndipo anarudi nyuma moja kwa moja kuonyesha jambo lile lile.

72 Haya basi, kukiwako na mahali patatu mbalimbali katika Maandiko, akipaambatanisha na ufunuo. Unaona? Angalia. Mahali ambapo Yesu alisema hivyo; mahali ambapo wakati Yeye alipofungua kile Kitabu, palikuwa pamefichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu; na halafu ufunuo wa siku hii hapa, akipaweka moja kwa moja, akipafungamanisha mahali hapo patatu pamoja. Na tatu ni ushuhuda. Kwa hiyo ni kweli. Ni kweli kabisa.

73 Basi, hawa wanawali waliokuja hapa, hao ndio wale waliolala usingizi, na kwa hiyo mwili wote umefanywa kwa kundi hilo. Hilo linaenda kufanyiza. . . . unaona, linafanyiza wa—wananawali wenye busara. Na wale wanawali wapumbavu ndio walioanzia huko nyuma katika wakati ule ule ambao wanawali wenye busara walianza, mpinga-Kristo, nao ndio wanaojaribu kununua Mafuta.

74 Sasa hebu angalia tu hapa na uone jinsi lilivyo kamilifu, po pote uendapo. Kama ningeweza kusimama hapa na kuzungumza mambo yaliyofunuliwa katika chumba kile, nawaambieni, yangewafanya mpate kizunguzungu. Lakini utawezaje kufanya hivyo, wakati una mambo kemkem hapa.

75 Kisha wewe, sijui kwa nini, unapoondoka kwa watu, ndipo siri zinaanza kufunguka. Pia, ndipo unaona mambo ambayo huthubutu kuwaambia watu. Kwa sababu, mnaona, kama ukiwaambia, wangeanzisha itikadi ndogo-ndogo.

76 Halafu hebu tuone vile hiki kipawa kidogo cha uponyaji kimefanya, jinsi kilivyolitatanisha kanisa. Kila mtu alikuwa na kituko fulani, kila mtu alikuwa na *hiki*; na moja kwa moja ndani ya moyo wangu, (Mungu anajua ni kweli,) nilijua haikuwa sahihi, kwa sababu Yeye aliniambia hivyo. Unaona? Lakini ni uongo wa kuiga, wa kuwapoteza tu watu. Sasa, hiyo ni kweli. Sasa, lakini, mnaona, huwezi kusema mambo hayo. Ni heri kabisa tu kuyaacha yalivyo.

77 Nanyi mnakumbuka ule Mvuto wa Tatu? Yeye alisema, "Usimwambie mtu ye yote." Nilisema huo ulikuwa ni kitu gani? Wangapi wanakumbuka jambo hilo? Hakika. Mnakumbuka, niliposimama pale, nikijitahidi kuingiza ile kamba ya kiatu kwenye kijitundu cha kile kijiatu, katika lile ono? Yeye akasema, "Huwezi kuwafundisha watoto wachanga wa Kipentekoste mambo ya kimbinguni."

78 Nikasema, "Huu utakuwa ni ule Mvuto wa Tatu, nao hautajulikana, kwa hiyo na anisaidie, kwa neema ya Mungu."

Sasa—sasa, tuko—tuko moja kwa moja kwenye wakati wa mwisho sasa. Haitakuwa muda mrefu hata Kiti cha Neema kitakapokuwa ni Kiti cha Hukumu. Unapoona mambo haya

yakiingia, na watu hawa wakiingia, heri na wewe uingie, pia, ikiwa bado hujaingia. Unaona?

79 Sasa, "Kukusanyika katika ulimwengu wa Roho," mnaona, inamaanisha pia zaidi ya kushangilia tu. "Katika ulimwengu wa Roho, kama ninyi hakika mmekusanyika katika Kristo, ni jambo la kuogofya!

80 Ukisimama karibu na . . . yule Malaika wa Bwana, unafikiri ungekuwa tu ukipiga makelele na kufanya shangwe. Hivyo, si hivyo. Linakuogopesha nusura ya kufa, nusura ya kufa. Unaona? Kwa hiyo, unaona, kuna—kuna tofauti baina ya kushangilia tu na kujifurahisha, ambako ni sawa, na halafu kufikia kwenye jambo lenyewe halisi. Unaona? Unaona? Hapo ndipo penye hofu. Ni jambo la kuogofya. Si kwamba unahofu umepotea; lakini uko kabisa mbele ya Kiumbe cha mbinguni, na Roho Mtakatifu Mwenywe amesimama hapo.

81 Sasa, hao watakuwa ni sehemu ya yule Bibi-arusi. Hao ndio watakaomfanyiza, mnaona, hao wote waliolala. Na sisi je! hatuwezi kuona kabisa . . .

[Vyombo vya kunasia sauti vinaharibika. Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] . . . tunaomba sasa ya kwamba utawajalia watu kuponywa, kupitia vitambaa hivi, vikiwekwa juu yao. Katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa, ni sawa sasa? [Ndugu wanasema, "Amina."—Mh.] Asanteni. Mtu fulani amekanyaga kitu fulani? [Ndugu fulani anasema, "Wameweka vinasa sauti vingi kupita kiasi kwenye laini ile."] Vinasa sauti vingi kupita kiasi vimelemea laini kupita kiasi. Unaona? Vema, badilisheni tu. Chukueni tu kanda na mwibadilishe kanda hiyo, na kunakili nyingine kwake. Sasa, tazama sasa swali linalofuata.

174. Je! wainjilisti waendelee na kazi yao?

82 "Katika saa hii," bila shaka, vile wanavyomaanisha. Ndiyo, hakika. Msibadilishe kitu cho chote. Kama Yesu anakuja asubuhi, hubiri leo kama kwamba inaenda kuwa ni miaka kumi toka leo hii, lakini uishi kama kwamba itakuwa ni saa hii hii.

83 Usi—usihangaike sasa. Hivyo ndivyo ninavyojaribu kuwaonya, unaona. Usiwe tu wa ajabu, mtu asiye wa kawaida. Usibadilishe cho chote. Lakini kama unatenda jambo lo lote baya, au unatenda maovu, tubu, unaona, mrudie Mungu. Endelea tu na huduma yenu ya uinjilisiti kama tu vile mnavyofanya sikuzote.

84 Kama unajenga nyumba, ijenge. Yesu akija kesho, ukutwe mwaminifu kazini. Ikiwa mnajenga kanisa, endeleeni, lijengeni. Afadhali niwe niziingize fedha zangu katika kitu kama hicho, kuliko nikutwe nazo mfukoni mwangu. Unaona.

85 Kwa hiyo hebu—hebu endelea tu, endelea tu jinsi ulivyo. Kila mtu anaelewa sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Endelea moja kwa moja tu, na uendelee tu jinsi ulivyo. Sasa, kwa kweli—kwa kweli usiache. Usikae bure . . . Endelea tu moja kwa moja jinsi ulivyo. Endelea kumtumikia Bwana.

86 Sasa, kwa mfano, ikiwa ulikuwa—ikiwa ulikuwa ukimfanyia mtu kazi, na ulijua ilikuwa imebakia dakika kumi na tano kabla ya wakati wa kuondoka. "Vema," ungesema, "en-he, ni dakika kumi na tano tu zimebakia, kwa hiyo heri niende tu nikaketi chini." Utahukumiwa kwa ajili ya hizo dakika kumi na tano.

87 Ikiwa unapanda ngano; panda ngano yako. Ikiwa unavuna viazi; endelea, vivune. Useme, "Vema, hakuna mtu atakayevila"? Hiyo haijalishi. Vivune, haidhuru. Unaona? Naam. Endelea tu jinsi ulivyo.

88 Nilipata barua toka kwa mtu fulani hivi majuzi. Mtu fulani aliwaambia, akasema, "Vema, wakati u karibu. Uza shamba. Sasa, hutahitaji vyakula unavyotumia, kutoka shambani," kasema, "maana Utawala huu wa Miaka Elfu utaanza, nawe hutalihitaji. Kwa hiyo endelea tu . . . Na wakati ile dhiki inapoendelea, watoto wako hawajaokolewa, kwa hiyo waache tu . . . Acha—acha watoto hao wachukue hilo shamba, ambamo wataweza kujilisha, bali ninyi nyote muuze mashamba yenu," na—na, ama kitu kama hicho. Na, loo! wao walijuta . . .

89 Nikasema, "Loo! jamani!" Kama nilijua Yeye anakuja kesho, nami nilikuwa mkulima, ningepanda zao langu leo. Hakika. Kama Yeye alinifanya mimi kuwa mkulima, nitadumu papo hapo kwenye wajibu wangu. Hiyo ni kweli. Kama Yeye alinifanya makanika, kasema ni nani . . .

90 Mtu fulani alisema, hivi majuzi, alisema . . . "Jamaa fulani aliingia na kusema, 'Aisee, ndugu, je! wajua?' Akasema, "Nitakupa seti ya pili ya funguo. Nilinunua gari jipya.' Akasema, 'Nitakupa seti ya pili ya funguo hizo,' akamwambia mchungaji wake. Kasema, 'Nitakupa fungu la pili la funguo hizo, sababu huenda ule Unyakuo ukaja, unajua, na,' akasema, 'sitazihitaji hizo tena.'" Mchungaji wake angeukosa, unaona. Loo! Huko ni kujiweka tayari, sivyo? Vema. Lakini hivyo—hivyo ndivyo ilivyo, unaona, haitupasi kuwa hivyo.

91 Yatubidi tuwe Wakristo we—wenye akili timamu, imara, unaona, ambapo nimewekwa hapa kufanya kazi hadi dakika ya mwisho kabisa. Nina kazi ya kufanya, nami nitakuwa sawa nikikutwa kwenye wajibu wa kazi. Yeye akija asubuhi hii, nataka niwe nimesimama papa hapa mimbarani.

92 Unasema, "Ndugu Branham, kama Yeye angekuja asubuhi hii, je, haikupasi kuwa *huko* nje?" La, bwana!

93 Huu ndio wajibu wangu wa kazi. Nitakuwa nimesimama papa hapa, nikihubiri, Yeye ajapo, nikisema mambo yale yale ninayosema. Ndipo, Yeye ajapo, nitaondoka tu moja kwa moja niende pamoja Naye, unaona.

94 Kama ninapalilia viazi, nitakuwa nikipalilia tu, kwa bidii tu niwezavyo. Yeye ajapo, nitatupa tu jembe langu nipae juu.

Mnakumbuka katika mwaka wa yubile, kama walikuwa wakipalilia—wakipalilia kwa jembe, waliendelea tu kupalilia. Wao walijua kuwa mwaka wa yubile ulikuwa labda uko dakika kumi zaidi zijazo, na baragumu italia katika ule mwaka wa yubile. Wao waliendelea tu kufunga majani ya ng'ombe, cho chote walichokuwa wakifanya. Lakini baragumu ilipolia, ndipo walitupa fimbo zao panda za kukusanya majani, na wakaenda zao. Unaona, hivyo ndivyo ilivyo. Endelea tu kukusanya majani ya ng'ombe hadi baragumu itakapolia. Vema.

[Sauti inasikiwa kutoka kwenye kitu kilicho karibu—Mh.] Swali, "Kulingana na kule kufunguliwa . . . " Je! hilo . . . Jambo lo lote lilitukia? En-he? Ku—kulitokea sauti fulani hapa. Swali:

175. Kulingana na kule kufunguliwa kwa Muhuri wa Ta—Tano, Musa na Eliya hawana—hawana budi wafe. Vipi kuhusu Henoko?

95 Sijui. Unaona? Si—si- . . . Kama sijui, nitawaambia tu sijui. Mnaona? Mimi—si—sijui majibu yote, jamani. Si—sijui. Na kama sijui, nitawaambia sijui. Kama ninajua . . . Sitawaambia mpaka nitakapojua, mnaona. Lakini si—sijui.

96 Mara nyingi nimeshangaa juu ya jambo hilo mimi mwenyewe. Kulikuwako na Henoko . . . Ninamwona Musa akija, na Eliya akirudi, nao wanauawa, unaona, lakini sasa Henoko alihamishwa kabla ya wakati. Mara nyingi mimewazia, na kushangaa, mimi mwenyewe, "Vema, vipi, vipi kuhusu jambo hilo?"

97 Lakini, basi, hii hapa faraja pekee ninayoweza kusema, ni hii. Sasa angalia, Musa alimtumikia Mungu miaka arobaini tu. Unaona? Yeye alikuwa ninii—alikuwa na mia na ishirini. Lakini miaka ishirini . . . Miaka arobaini ya kwanza, ninamaanisha, alikuwa akipata elimu yake. Hiyo ni kweli? Miaka arobaini ya pili, Mungu alikuwa akiitoa ndani yake. Na miaka arobaini ya tatu, akamtumikia Mungu. Mnaona? Vema. Lakini Henoko alitembea miaka mia tano mbele za Mungu, na alikuwa hana hatia." Mnaona? Mnaona? Kwa hiyo, Musa yuaja tena kutumika kwa wakati zaidi; yeye pamoja na Eliya.

98 Sasa, hilo, sisemi kuwa hilo ni sahihi, mnaona. Nimewapa tu hilo kama wazo, mnaona. Lakini kusema tu ni sehemu ipi, sijui. Kweli siwezi kuwaambieni kile—kile kilichotendeka huko, au kile Mungu atakachotenda.

176. Ni ji—jina lipi la- . . . watakalopewa watu wa Ufunuo 3:12?

99 Si—sijui. Naam. Yeye alisema, "Tawapa jina jipya." Si—si—sijui hilo ni lipi, mnaona. Itakuwa labda litajulikana tutakapofika huko, lakini si—sijui ni lipi sasa, unaona. Unaona,

Yeye atafanya jambo hilo. Unaona? Yeye aliwapa jina jipya mbalo—ambalo walilijua tu, wao wenyewe. Mnaona?

177. Sasa, Ndugu Branham, je! kuna Andiko lo lote linaloruhusu ndoa baada ya talaka? Hili ni muhimu sana.

100 Linasema, "Muhimu." Vema, hiyo ndiyo sababu. . . Halikuhusiana na haya. Kadiri niwezabyo kuona, ndugu yangu, ama dada, ye yote yule, halipo, isipokuwa mwenzio amekufa. Kwa sababu, Biblia ilisema, "Tumefungamana nao mradi tu wao wakali hai." Unaona?

101 Kwa hiyo, ku—kuhusu kuwapo na "Andiko lo lote?" Hilo ndilo lililoulizwa hapa, "Je! kuna Andiko?" Unaona? "Je! kuna Andiko lo lote?" Siwezi kulipata, unaona, siwezi kulipata.

Kwa sababu, Paulo alisema ya kwamba mu—mume na mke waliofunga ndoa, "Kama mwenziwe amekufa, basi wao wako huru kufunga ndoa na ye yote wampendaye katika Bwana." Lakini mpaka wakati huo, lakini, angalia, unalichukua, "Hadi mauti itakapotutenganisha." Hivyo ndivyo ilivyo. Tayari mmefanya nadhiri juu ya jambo hilo, unaona.

102 Kwa hiyo, sidhani lipo. Sasa, kama kuna . . . kama umepata baadhi yake, na ni sahihi, mbona, ve—vema. Lakini, kwangu mimi mwenyewe, si—sioni lo lote.

178. Nini maana ya "angalia usiyadhuru mafuta wala divai" katika Ufunuo 6:6?

103 Ni Roho Mtakatifu. Unaona? Ndiyo kwanza tupitie hayo. Labda mtu fulani, unajua, aliingia amechelewa kidogo wakati wa huo Ujumbe, wao . . . vema, kwa ajili ya kanda zile nyingine, unaona.

"Wala usidhuru mafuta wala divai." Nini maana ya mafuta na divai?

104 Mafuta, kama tulivyoeleza jambo hilo katika mfano, maana yake ni Roho Mtakatifu. Unaona? Divai ni . . . na mafuta, vinahusishwa pamoja, katika Biblia, katika ibada. Unaona? Na divai, kama tulivyoeleza, hapo ndipo nilipopata wazo, "changamko." Divai huchangamsha. Na divai, katika ninii yake—asili ya mfano wake, kutoka kuchangamka, ni ufunuo.

105 Sasa hebu fikiria tu. Ni kitu gani kinacholichangamsha Kanisa? Ufunuo. Unaona? Kwa hiyo, divai, ile divai mpya, ingekuwa . . . Sasa tazama. Mafuta na divai viliambatana pamoja, katika dhabihu; viliambatana, katika—katika ibada ya kanisa. Sasa angalia, kukusanyika pamoja, vimeshikamanishwa pamoja.

106 Kama una itafaki, tazama uone mfululizo mzima ambapo divai na mafuta vinaambatanishwa katika ibada. Iwapo una ile ya—ya Cruden, mbona, inasema hayo hapo.

107 Sasa tazama katika jambo hili. Lakini sasa, unaona, mafuta kila mara ni Roho Mtakatifu. Tunaona hayo katika Ezekieli. Na tunalipata hilo katika Agano la Kale. Tunaona jambo hilo kote katika Agano Jipya.

108 Kwa sababu gani tunawapaka wagonjwa mafuta? Tunawapaka wagonjwa mafuta kwa sababu inaonyesha mfano wa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu juu yao. Unaona? Pia, wale wanawali wenye busara walikuwa na Mafuta; wale wapumbavu hawakuwa na Mafuta. Roho, unaona. Sasa, hayo ndiyo Mafuta. Na halafu divai, ni—ni . . . Kama mafuta yanamwakilisha, yanamwakilisha Mungu, Mungu ni Roho. Unaona?

109 Mungu ni Neno. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno; Neno alikuwako kwa Mungu. Neno alifanyika mwili, na huyo alikuwa ni Mungu." Sasa, basi, ikiwa Neno sasa katika . . . limeketi hapa katika hali ya kawaida sasa, divai ni kama maji, ambayo, ama ufunuo unaofunua hiyo tafsiri ya Neno, ambao humchangamsha mwamini, unaona. Jamani, wao wanasema tu, "Sijapata kuona jambo Hilo hapo kabla! Jamani! Utukufu!" Hiyo ni nini? Unaona, changamko, unaona, la ufunuo.

110 Wala sikujua jambo hilo mpaka hivi majuzi, nikiketi pale. Mnaona? Sasa, hiyo ni, "Maana ya mafuta na divai ni . . ." Hiyo ilikuwa, "Angalia kwamba usiyadhuru." Huyo alikuwa ni yule mpanda farasi mweusi. Na hiyo ilikuwa katika ule wakati wa giza, ule wakati wa tatu wa—wa kanisa. Tazama. Na, ndani humo, "Yako kidogo tu yaliyosalia, kidogo tu, lakini usiyadhuru Hayo."

111 Nami ninaamini kama ukiupata huo huo—huo Muhuri wa Tatu, kwenye kanda, utaninii . . . ungelipata humo, tulikolielezea kwa kirefu, au kwa urefu, hasa.

179. Je! Ndugu Branham, Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo na Kitabu cha Uzima, ni Kitabu kile kile?

112 Hakika, unaona, kwa sababu humo ndimo ambamo ukombozi wote umeandikwa, katika Kitabu hiki. Unaona? Majina yao yamo ndani Yake. Unasema, "Vema jina letu limeandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, Ndugu Branham. Ni—nilijiandikisha, juzi usiku." La, hukuliandikisha. La, hukuliandikisha. Uligundua tu lilikuwa Humo, juzi usiku, unaona, kwa sababu majina yao yaliandikwa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Unaona? Hicho, ni Kitabu kile kile, unaona.

180. Sasa, Ndugu Branham, je! ni kweli ya kwamba—ya kwamba kila Myahudi, aliyezaliwa tangu Kristo alipokuja, ataokolewa? Na wale mia na arobaini na nne elfu ni akina nani? Je! hao ni wale waliochaguliwa tangu zamani watakaotiwa muhuri na Roho Mtakatifu? Na kazi yao ni ipi?

113 Kuna karibu maswali matatu katika hilo moja, hapo. Lakini, hapa, la kwanza:

> **Je! ni kweli ya kwamba kila Myahudi aliyezaliwa tangu Kristo, alipokuja ulimwenguni, ataokolewa?**

114 La. Hakuna watakaookolewa, ila wale tu ambao majina yao yaliwekwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, Myahudi ama Mmataifa. Unaona? Hivyo tu. Kitabu hicho kinashikilia siri hiyo, na Kitabu hicho kinaifungua tu hivi sasa; si jina la kila mtu, lakini kwamba siri ya Kitabu hicho ni, wakati inapoyaita majina hayo. Hatimaye mnafahamu jambo hilo sasa? Mnaona?

115 Kitabu hicho hakisemi, "Sasa, Lee Vayle ataokolewa katika kipindi cha wakati huu wa kanisa, ama—ama Orman Neville," ama—ama ye yote yule. La, hakisemi hivyo. Kinaonyesha tu ile siri, kinafungua tu siri ya kwamba kitu hicho ni nini. Lakini sisi, wenyewe, kwa imani, tunaamini jambo Hilo. Hivyo ndivyo nilivyosema hivi majuzi.

116 Mtu fulani alisema, "Vema, hakuna haja ya mimi kujitahidi. Ndugu Branham alisema kutakuwa na mmoja tu atakayeokolewa kutoka Jeffersonville." Mnaona? Sasa, mnaona, ni kuonyesha mfano. Hivyo—hivyo—hivyo sivyo, hivyo—hivyo sivyo hivyo. Huenda maelfu wakaokolewa. Sijui. Natumaini kila mmoja wao ameokoka, unaona, lakini sijui.

Lakini nataka kuamini jambo hilo kwa namna hii hapa, "Huyo mmoja ni mimi." Wewe amini vivyo hivyo kwa ajili yako. Usipoamini hivyo, basi kuna kasoro katika imani yako; huna hakika ya kile unachofanya.

117 Wawezaje—wawezaje uende pale mbele ya mauti, wakati huna hakika mno kabisa kama umeokoka ama hujaokoka? Unaona? Wawezaje kwenda hapa na kumwambia huyu mwanamume kilema anayelala hapa, amepofuka na amelemaa, "BWANA ASEMA HIVI. Amka! Yesu Kristo anakuponya"?

118 Wawezaje kustahimili, maskini mwili huo baridi na mkavu uliolala pale, ambao umekufa, na umekufa kwa masaa kadha wa kadha, na umelala pale, na uko pale, wenye baridi na ni mkavu; na useme, "BWANA ASEMA HIVI, simama kwa miguu yako"? Heri, heri ujue unachoongea. Unaona?

119 Vema, wasema, "Mauti huchukua kila kitu. Yote yamekwisha." Naam, lakini Neno la Mungu linapofunuliwa, na unajua ni Mungu, hilo hubadilisha mambo. Hiyo ni kweli.

120 Sasa, naam, hawa Wayahudi si . . . Si Wayahudi wote watakaookolewa. La, bwana. Hawataokolewa; ila wale tu ambao . . . Yeye anaponena kuhusu M—Myahudi, "Mayahudi," ni jina tu walilopewa baada ya kuondoka . . . Naamini, Nebukadreza, kule, ndiye aliyeanza kuwaita ni "Wayahudi," kwanza, kwa sababu lile kabila la Yuda lilichukuliwa kule. Nao

wakapewa jina la "Myahudi," sasa, kwa sababu walitoka Yuda, nao wakapata jina la Myahudi.

121 Lakini sasa, Israeli ni kitu tofauti. Israeli, na Myahudi, ni vitu tofauti kabisa kabisa. Kila Myahudi—kila Myahudi si Mwisraeli, unaona. La, yeye ni Myahudi tu. Lakini, basi, Israeli . . . Paulo hakusema Wayahudi wote wataokolewa. Alisema, "Israeli wote wataokolewa." Kwa nini? Jina la Israeli, hilo—hilo ni jina la ukombozi, kutoka huko nyuma kote. Unaona? Na Israeli wote wataokolewa, lakini si Uyahudi yote—Kila aliye wa dini ya Kiyahudi atakayeokolewa. Mnaona?

122 Kama vile tu Mataifa, kutakuwa na . . . Kuna maelfu mara maelfu ya—ya watu, naam, mamilioni kabisa, katika madhehebu haya, na yanaitwa "ya Kikristo, kanisa la Kristo," na majina yote kama hayo. Hayo hayamaanishi cho chote. Si . . . Hiyo haimaanishi wataokolewa.

Watu husema, "Sasa, yabidi uwe katika *hili* ama *lile*, madhehebu, madhehebu fulani. Kama jina lako halimo katika kitabu chetu, umepotea." Sasa, hilo ni kundi lililojitenga. Unaona? Hilo ni kundi lililojitenga. Unaona?

123 Kuna njia moja pekee uwezayo kuokolewa, na, hiyo ni, "Si katika uwezo wa yeye atakaye, wala yule apigaye mbio, yeye ambaye . . . Basi, ni Mungu arehemuye." Naye Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, alichagua Kanisa kwa ajili ya Utukufu Wake, na hao ndio wanaokolewa. Kweli. Sasa, imani yako imetiwa nanga sana Hapo!

124 Unasema, "Vema, imani yangu imetiwa nanga Huko." Na basi angalia unaishi maisha ya namna gani. Unaona hata hustahili kuwa Huko. Nanga yako imetiwa mahali pabaya. Umeitia kwenye changarawe badala ya kuitia kwenye mwamba. Wimbi dogo la kwanza litaing'oa. A-ha.

125 Hebu Neno lifunuliwe katika kitu fulani. "Kanisa langu halifundishi jambo Hilo!" Hiyo inaonyesha papo hapo wewe hukuwa umetiwa nanga kwenye mwamba wo wote. Wewe ulikuwa kwenye mchanga. A-ha. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, sasa unaona, sasa.

Na wale mia na arobaini na nne elfu, je! hao ni wale waliochaguliwa tangu zamani?

126 Naam, bwana. Hao ni Israeli, Israeli wa kiroho.

127 Hebu fikiria tu, kutakuwako na mamilioni yao humo. Sijui ni wangapi walioko humo sasa; Nadhani ni kundi lote, lakini si wote watakaookolewa ati kwa sababu wako Uyahudi. Mnaona?

Mna habari ni wangapi walioko humo hivi sasa? Sijui. Lakini wao labda . . . Baada ya haya mateso yajayo kuanza kutokea . . . wanakusanyika kwa . . . Mwajua, nina kanda yao, ambayo ninaenda nayo huko magharibi sasa kwa—kwa moja la—la kanisa la Agano ambalo liko ninii . . .

128 Ni ninii tu la kale . . . Lo! nasahau sasa. Lilianza ninii . . . Wanayo huko Afrika. Dutch Reform. Hilo ni Kanisa la Dutch Reform, la Agano. Sasa, ikiwa kuna ye yote wenu anayeketi hapa, nitawaambia sababu yake. Mngali mnashikilia ile Katekisimo ya kale ya Heidelberg, na hiyo hasa ndiyo sababu mngali katika ninii . . . mngali Dutch Reform. Kwa hiyo, mwaweza kulipamba kwa jina la Kimarekani. Hicho—hicho ndicho kitu kilicho nyuma yake, sababu mngali mnafundishwa kutoka kwenye katekisimo iyo hiyo, ile ya kale ya Heidelberg. Mwulize mchungaji wako kama hilo si kweli. Unaona? Kwa hiyo, sasa, angalieni jambo hili.

Wale mia na arobaini na nne elfu, hao ndio waliochanguliwa tangu zamani watiwe muhuri na Roho Mtakatifu?

129 Ndiyo, bwana. Hiyo ni kweli kabisa. Vema. Sasa kama kuna ninii yo yote . . . Sasa kama mimi nina ninii . . .

Kama sikulijibu, kukuridhisha, mbona, labda mimi ni . . . Ningeweza kukosea, unaona. Lakini, haya, ndiyo yote kabisa nijuayo mimi, mnaona. Haya ni kadiri nijuavyo mimi kabisa.

181. Ndugu Branham, kwa kuwa umeutaabikia ama kutaa- . . . juu ya ule uzao wa nyoka . . . (En-hee, sikuona hili hata. Hili liliniponyoka) . . . **uzao wa nyoka juma hili, je! itakuwa vema kuuliza swali hili? Rafiki zangu wameniomba nieleze Mwanzo 4:1, nami siwezi. Je! waweza kunisaidia?**

130 Liko—liko nje ya somo. Lakini, hata hivyo, nita—nita—nitajaribu niwezavyo, kwa msaada wa Mungu. Hebu na tuone sasa. Hebu nilifafanue kidogo, kwa muda kidogo tu. Nadhani hapo ndipo ambapo alisema, "Nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana." Na—naamini ni hapo . . . Nafikiri Hawa alisema hivyo hapo. Nitachunguza, kusudi niwe na hakika.

131 Sababu, nilisema, usiku uliopita, saba . . . badala ya . . . mia saba badala ya elfu saba. Kwa hiyo inanifanya kuwa na wasiwasi sana, unaona, na yapasa tu mwe waangalifu. Na adui yuko kila upande, nawe una—unajua jambo hilo, unaona. Naam, ndivyo hivyo.

Adamu akamjua Hawa mkewe; naye akapata mimba, na akamzaa Kaini, na akasema, Nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana.

132 Sasa, nitajibu tu swali lako, ndugu yangu au dada. Na sasa, kuwashambulia, si kuwatupia, la. Ninajaribu kuwasaidia, unaona. Nawapenda, na ninampenda mtu ambaye huenda alikuwa mkinzani wa jambo hilo. Lakini sidhani mtu huyu anapinga. Wao walisema, "Nisaidie," unaona, kwa sababu watu wanaliamini, lakini hawakufundishwa vya kutosha, na Roho, wajue la kumwambia mtu aliyewauliza hilo.

133 Sasa, yeye anasema hapa ni swali gani, hakuna shaka, kwamba wanasema, "Hawa alisema alimpata mtu huyu kwa Bwana."

134 Wadhani uhai ungekujaje ikiwa haungekuja kutoka kwa Bwana, uwe wa halali ama wa haramu? Ni nani aliyemtuma—Ni nani aliyemtuma Yuda Iskariote duniani? Niambieni hilo. Biblia ilisema yeye alizaliwa "mwana wa upotevu." Hebu waulizeni tu hilo; itakuwa kama mnyoo ndani ya limau, unaona. Unaona? Sasa, unaona, hawawezi— hawawezi . . . Ndivyo ilivyo.

135 Tazama, basi kama ukitaka kuwachukua kwa ustadi kidogo zaidi. Tazama. Hawa alizungumza hapa, kama ukitaka kulichukua katika lugha iliyo hapa, iliyoandikwa kusudi ifichwe jichoni, mwa wenye hekima na akili. Hawa, hapa, jinsi inavyofundishwa, ya kwamba alimpata mtoto huyu mwanamume kwa uwezo wa Mungu. Naye ni Roho, na hawezi kufanya jambo hilo. Unaona? Sasa tazameni hapa, kama mnataka kuona jambo hilo. "Nimepata m—mtoto mwanamume kwa uwezo wa Bwana." Unaona, huwezi kulifanya liseme vyo- . . . Lakini halina budi kuwa na tafsiri yake ya kweli, unaona. Naam, bwana. La, bwana, kama jambo hilo, basi roho . . .

136 Nasi daima hurithi tabia ya mzazi wetu. Mnajua hilo. Mwangalie mtoto mchanga, tabia yake. Vema, basi, Adamu alikuwa mwana wa Mungu; Hawa alikuwa binti wa Mungu; vema, kitu cha kwanza cha viumbe vya Mungu, ambacho hakingeweza kuwa na hata chembe moja ya—ya uovu po pote karibu nacho. Uovu hata haukujulikana.

137 Basi mbona Kaini alikuwa ni mwongo, mwuaji, na kadhalika? Hayo yalitoka wapi? Hebu jiulize tu mwenyewe swali hilo. Huo ulikuwa ni uzao wa nyoka. Unaona? Je! Biblia haisemi hivyo? Uchunguze uzao wake wote. Kwa hiyo, yeye akawa . . .

138 Je! ulimwengu ni wa nani? Ibilisi. Ni nani anayeuongoza hivi sasa? Ibilisi. Sawa kabisa. Ibilisi anautawala ulimwengu. Yeye alimwambia Yesu, kasema, "Unaona jinsi huu ulivyo mzuri, utukufu wake wote? Nitakupa ukiniabudu." Unaona, Yeye ndiye anayeutawala. Sasa, yeye anaumiliki.

139 Sasa angalia, watoto wake wana maarifa; watoto wa Ibilisi. Ama, wachukue wana wa Kaini, ukitaka, na uwafuatilie kwenye vizazi vyote, nawe utaona ya kwamba walikuwa ni watu werevu, kila mmoja wao.

140 Lakini basi wakati alipomwua Habili; na Mungu akamrudishia Sethi, ilikuwa ni mfano wa wenye haki, kukomboa; wakiwa wafu na kufufuka tena. Na tangu wakati huo . . . Sasa angalia. Si kutoka katika uzao wa kwanza, wa maumbile ya kawaida; wao walikufa. Sasa akili zenu zimefunguka? Mnaona? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Ule uzao wa kwanza, wa uzao wa maumbile ya kawaida, ukiwa ni mzuri wa kawaida tu, ulionyesha mfano wa kanisa la kisasa, Habili. Ili kuhifadhi uzao huo upate kuendelea, huyo mmoja alikufa kusudi mwingine apate kutokea, unaona. Kwa hiyo, hapana budi iwe ni kuzaliwa upya, tena. Mnalipata? ["Amina."] Vema, ili kwamba tu mlipate, mnaona?

141 Ndio huo hapo, ule mfano ulio kamili. Kwa hiyo hata mtu wa kawaida, aliyezaliwa na—na Adamu, baba yake, anaonyesha huo mtindo asilia. Haiwezekani; mtu wa kawaida hayasikii mambo ya Mungu. Kwa hiyo Mtu mmoja alikuja kwa njia ya maumbile ya kawaida, na akafa, ili kurudisha jambo hilo tena; naye amewakilishwa katika mauti ya—ya—ya Habili, na mahali pake kuchukuliwa na—na Sethi.

142 Basi angalia hao walikuwa ni watu wa aina gani, sasa, roho hiyo ilicholeta toka kwake; wanyenyekevu, wakulima, wachungaji wa kondoo. Angalia kilichotoka kwenye hekima hii ya ulimwengu hapa; watu werevu, wajenzi, na—na kwa chuma, na kila namna ya werevu wa akili na mambo kadha wa kadha. Angalia mahali walikoishia. Walikuwa wako huko chini, na Mungu akaangamiza kila mmoja wao, kila mmoja wao, na kuwaokoa walio wenyenyekevu. Je! Yesu hakusema, katika Mathayo 5, "Wenye upole watairithi nchi"?

143 Kwa hiyo, naam, usione wasiwasi. Hawana hata pa kuweka mguu. Unaona? Wao hawaamini kwamba huyo ni mwana wa Kaini. Lakini tuna kanda kuhusu hayo, ukitaka kuyasikia yakielezewa kwa undani hasa. Mnaona? La, bwana.

144 Nami nimeona wameandika makala ndogo kwenye gazeti huko, ambapo sayansi sasa itathibitisha ya kwamba "Hawa hakula tofaa hata kidogo. Alikula aprikoti." Mnaona? Nina gazeti hilo huko nyumbani hivi sasa, mnaona. "Ilikuwa ni aprikoti." Ni umbali gani watu wawezao . . . hayo ni mawazo ya kimwili, mnaona.

"Halafu, kwa kweli, Musa hakuvuka yale maji hata siku moja. Alivuka bahari ya matete; akawavushia Israeli sehemu ya ncha ya juu ya mwisho wa Bahari ya Chumvi. Kulikuwa na chaka la matete mengi huko, bahari nzima ya matete, mahali ambapo palikuwa na maji wakati mmoja, yakapungua kidogo. Ndipo Musa akachukua njia ya mkato na akazunguka kwa njia ya huko." Nayo makanisa ya Kiorthodoksi yalilikubali hilo. Mliona jambo hilo. Makanisa ya Kiorthodoksi yalikubali jambo hilo, kwamba hivyo ndivyo ilivyokuwa.

145 Loo! jamani, hivi hamwezi kuuona huo uzao wa nyoka, huyo mpinga-Kristo, na jambo nzima likiwa liko hapo wazi? Kweli. Ndiyo, bwana.

Ndugu Branham, tafadhali mwombee nanii wangu mdogo . . . (Vema, hilo ni ombi la maombi; naona.) . . .

Mwombee mjukuu wangu mdogo wa kiume, yuko taabani ana mafua. Yeye yuko katika Hoteli ya Riverview.

146 Bwana Yesu, maskini mtu huyu hapa hakuandika hayo bure tu hata kidogo. Yeye aliishakuona Wewe hata ukimponya dhahiri mtoto mdogo mwanamume homa ya baridi yabisi hivi majuzi usiku. Anajua ya kwamba Wewe ndiye yule Mungu mkuu, nasi twatoa maombi yetu kwa ajili ya huyo mvulana mdogo. Katika Jina la Yesu Kristo, na aponywe. Amina.

147 Mtu anapoandika cho chote, si bure. Wa—wa—wa wana ninii. . .Haidhuru inaonekana ni jambo dogo vipi kwetu, na ni cha uzito wa kiasi gani, lakini—lakini kuna kitu fulani nyuma yake, unaona; huyo mama, huyo mvulana mdogo, kitu fulani.

182. Je! yule Eliya, anayekuja kuwahubiria Wayahudi, ni yule mtu mwenyewe hasa aliyeishi duniani, ama atakuwa ni Roho wa Eliya katika mtu mwingine?

Sasa, hilo ni, ni—ninaogopa kusema. Sijui. Unaona? Hebu nilisome hilo tena.

Je! yule Eliya, anayekuja kuwahubiria Wayahudi (loo! naam), **ni yule mtu mwenyewe hasa aliyeishi duniani, au atakuwa ni roho wa Eliya katika mtu mwingine?**

148 Sasa, kama ningeweza kujibu hilo vizuri, ningeweza kuwaambia kuhusu Henoko, mnaona. Lakini si—siwezi kuwaambia, mnaona. Jambo tu nijualo ni kwamba, ninii tu, Maandiko yanasema jinsi itakavyokuwa. Na sasa huenda ikawa ya kwamba ninii. . .Sasa, kwa namna fulani ni— ninafikiria. . . Sasa hebu niliseme jambo hilo hivi. Nami natumaini kanda, ndugu wanaosikiliza kanda, wataelewa na jambo hili. Naelekea kuamini ya kwamba itakuwa ni watu waliotiwa upako, na roho zao hao. Kwa sababu, mnaona, yeye anasema, "Je! si ninii. . .kuhusu Elisha? Je! roho ya Eliya si iko juu ya Elisha?" Unaona, "roho ya Eliya." Naye alitenda tu kama alivyotenda Eliya, mnaona. Kwa hiyo, mimi, kama mimi. . .Lakini siwezi kusema hilo ni kweli. Si—sijui, mnaona. Mimi ni mwaminifu kwenu; sijui.

183. Ndugu Branham, waweza tafadhali kunijibu hili, kuhusu ubatizo? Mathayo 28:19 inafundisha, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Naye Petro, katika Matendo 2:38, "katika Jina la Bwana Yesu." Badiliko hili lilitokea lini katika Matendo ya Mitume? Sasa, ninamwamini "Bwana Yesu."

149 Vema, ndugu au dada, ye yote aliyeandika haya, ha—hapakutokea badiliko, mnaona. Ni. . .Na Petro alitenda yale hasa Yesu aliyosema atende. Sasa, kama mtu fulani akija na kusema, "Tumia wadhifa wa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," walitenda yale Petro aliyosema yasitendwe, kupinga yale Mungu aliyosema yasitendwe. Mnaona? Sasa, Yesu alisema ya kwamba. . .

150 Tutachukua ninii tu—kidogo tu. Sisi ni-. . .Nataka tu kuwaonyesha jambo fulani hapa. Angalia. Sasa angalia, kama uko hapa, mtu huyo. Nitaweka vipande vitatu vya vitu hapa. Sasa angalia, [Ndugu Branham anaweka vitu vitatu kama vielelezo—Mh.] *Hiki* ni Baba, *hiki* ni Mwana, *hiki* ni Roho Mtakatifu; kama watu waaminio utatu wanavyowaamini, wanavyoamini kwamba ni nafsi tatu mbalimbali. Wao wanaamini hivyo. Unaona? Vema, basi, sasa hebu mimi . . .

151 Na halafu katika Mathayo 28:19, Yesu alisema, "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Yeye. . ." La, samahani. Ninanukuu Matendo sasa, ama katika Matendo 2, naamini. La, Luka 24:49, ninanukuu. Yeye alisema. . .Hebu niisome, ndipo nimeipata, mnaona, halafu basi. . .sababu juzi nilisema hivyo ambapo sikuninii. . . Ninataka kuwa na hakika ninapata jambo hili vizuri. Na—najua kichwa cha maneno yale unayosema pale, lakini nataka nipate tu hasa yale Yeye aliyosema. Hebu na tuanzie kifungu cha 16, cha 29 . . . "Ndipo wale kumi na mmoja walipoketi wapate kula, ninii . . .

> *Na wale . . .kumi na mmoja wakaenda Galilaya mpaka mlima ule aliowaagiza Yesu.*
>
> *Nao walipomwona, walimsujudia, lakini baadhi yao waliona shaka.*
>
> *Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia,* mamlaka yote mbinguni na katika nchi imepewa . . . *Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.*

152 Sasa iko wapi mamlaka ya Mungu? Mungu yuko wapi? Ikiwa mamlaka yote inayotoka Mbinguni, na mamlaka yote iliyoko duniani, imetolewa, sasa Mungu yuko wapi? Huyo hapo, unaona. Huyo ndiye anayekuzungumzia. Vyema.

> *Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;.*

153 Sasa mtindo wa wanaoamini utatu wa jambo hilo ni, "Nakubatiza katika jina la Baba, katika jina la Mwana, na katika jina la Roho Mtakatifu." Hilo hata halimo katika Maandiko Matakatifu. Unaona? Yeye alisema, "Wabatizeni katika Jina la Baba, na la Mwana, na la. . ." Si katika. . . na kuweka jina mbele kila kimoja. Jina moja! Angalia hapa. Haikusema, "Mkiwabatiza katika majina." J-i-n-a, Jina moja, "Katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Mnaona?

154 Sasa nataka kuwaulizeni. Je! Baba ni jina? [Kusanyiko, "La."] Je! "Mwana" ni jina? ["La."] Kuna mababa wangapi hapa? Ni nani wenu ambaye jina lake ni "Baba"? Kuna wana wangapi hapa? Kuna wanadamu wangapi hapa? Unaona? Vema, ni nani kati yenu anayeitwa kwa jina la "Baba," "Mwana," au "Mwanadamu,"? Unaona?

155 Kama vile mwanamke fulani alivyosema wakati mmoja, alisema, “Ndugu Branham, ‘Roho Mtakatifu’ ni jina. Ni Nafsi.”

156 Nikasema, “Naam, bwana. Mimi ni mtu, lakini jina langu si ‘Mtu.’ Mimi ni mtu, mnaona. Jina langu ni William Branham; lakini mimi ni mtu.”

Roho Mtakatifu ni Mtu, hivyo ndivyo alivyo Yeye. Si jina; ni cheo cha Utu wa Mungu. Unaona? Ni cheo cha utu wa Mungu, kile alicho Yeye. Sasa—sasa ikiwa . . .

157 Yeye alisema, “Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na la Mwana, Roho Mtakatifu.”Si “katika Jina la Baba, jina la Mwana, jina la Roho Mtakatifu.” Ama, si “katika *majina* ya Baba, na la Mwana, Roho Mtakatifu,” lakini, “Katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.” Na kama “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” si jina, ni vipi basi?

158 Ukisema kama ni “jina,” vema, ni lipi? Ukitaka kuita mojawapo la hayo, ni jina lipi? Kama ukitaka kuita cheo hicho ni jina, basi ni lipi, gani, ni cheo gani unachotaka kubatizia, cha “Baba” ama “Mwana”? Ni umoja, unaona.

Sasa, na tufungue hapa, na hicho ni kitabu cha mwisho cha Mathayo.

159 Kama vile nilivyolielezea sikuzote. Kama ukisoma hadithi ya mapenzi, na ilisema, “Yohana na Mariamu wakaishi raha mustarehe sikuzote.” Unaona, ni kwa sababu wewe hujaninii—hujui Yohana na Mariamu ni nani. Rudi mwanzoni mwa hadithi yako, chunguza Yohana na Mariamu ni akina nani. Unaona?

160 Sasa hicho ndicho unachofanya hapa katika Mathayo. Unasoma tu sehemu yake ya mwisho. Rudi mwanzoni mwa Mathayo na usome hiyo hadithi inasema nini. Hiyo ni sura ya mwisho ya Mathayo, na aya za mwisho.

161 Ni kama vile ungalichukua kitabu, na kusema, “Yohana na Mariamu wakaishi raha mustarehe sikuzote. Huyo alikuwa ni Yohana Jones na—na Mariamu *Fulani*. Huyo alikuwa . . .? La, huyo alikuwa ni Yohana . . .? Huyo alikuwa ni Yohana Henry na huyo alikuwa *Fulani*? Huyu ni Yohana *Fulani* na *Fulani?*” La, hujui bado, unaona. Jambo pekee la kufanya, ili uwe na hakika, ni kurudi kwenye kitabu hicho na kukisoma. Unaona, huwezi kuokota sehemu *hapa*. Unapaswa kuweka kitu hicho chote kizima pamoja, ili uitoe hiyo picha.

162 Sasa rudi katika Mathayo, sura ya 1. Nayo inaendelea na kuzionyesha hizo koo, tukiendelea kwenye sura ya 1. Halafu inafikia kwenye kifungu cha 18, na ikasema: “Basi kuzaliwa Kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi.” Sivyo? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.]

163 Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani. Sasa sikilizeni tena. Ninyi, ninyi mseme jina lake. [Ndugu Branham anaelekeza

kwenye kila kimoja cha vile vitu vitatu kama vielelezo—Mh.] *Huyu* ni Nani? Mungu Ba-. . . [Kusanyiko, "Baba."] Mungu Mwa-. . . ["Mwana."] Mungu Ro-. . . ["Roho Mtakatifu."] Sasa *huyu* ni nani? ["Baba."] *Huyu* ni nani? ["Roho Mtakatifu."] Nani *huyu*? ["Mwana."] Mwana. Vema. Sasa tumelipata sasa. Sasa mlisema *huyu* alikuwa ni nani; Mungu *nani*? ["Roho Mtakatifu."] Roho Mtakatifu. Vema. Sasa, vema.

> *Basi kuzaliwa Kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi. Mariamu mama Yake alipokuwa. . . ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa. . .*

164 [Kusanyiko linasema, "Roho Mtakatifu"—Mh.] Sasa, nilidhani mlisema Mungu alikuwa ndiye Baba Yake. Sasa kuna kasoro fulani hapa. Yeye hawezi kuwa na Baba wawili. Mnajua jambo hilo. Mnaona? Sasa kuna kitu kasoro. Sasa ni nani kati ya Watu hawa, iwapo wao ni Nafsi tatu, ni nani kati yao aliye Baba Yake? Biblia inasema hapa, dhahiri, "Alionekana ana mimba ya Roho Mtakatifu," Mungu Baba hakuhusika kwa vyo vyote na jambo hilo. Na Yesu alisema Mungu alikuwa ndiye Baba Yake, na sisi tunajua Mungu alikuwa ndiye Baba Yake. Ikiwa ndio hivyo, Yeye alikuwa na baba wawili; basi Yeye ni wa haramu, kweli kabisa. Sasa unaona mahali umejiingiza? Sasa:

> *Naye Yusufu, mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri.*
>
> *Basi alipokuwa akifikiri hayo. . .*

165 Kumbuka, yeye alikuwa ni mtu mzuri, sasa. Na mkono wa Bwana ni mkono kama sasa; wale waliochaguliwa tangu zamani wataelewa. Mnaona?

> *Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto,. . .*

Unafuatilia katika Biblia yako? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema.

> *. . . akisema, Yusufu, ewe mwana wa Daudi, usihofu. . . -mchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uwezo wa. . .*

166 "Mungu Baba"? Je, nilisoma hilo vibaya? [Kusanyiko linasema, "Ndio."—Mh.] Hakika nilisoma vibaya. "Mimba yake," haina uhusiano wo wote na Mungu Baba, ni "Roho Mtakatifu." Na sasa tunajua ya kwamba Mungu alikuwa ndiye Baba Yake. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Kwa hivyo ni nini? Roho Mtakatifu ni Roho wa Mungu, bila shaka. Sasa, mmelipata. Mnaona?

167 Mungu Baba na Roho Mtakatifu ni Mtu yule yule, la sivyo Yeye alikuwa na baba wawili. Na basi—basi ni mtu wa aina gani mnayemwabudu? Mna Mungu wa aina gani sasa? Mnaona?

Mnaona? Mungu Roho Mtakatifu, na Mungu Baba, ni Roho yule yule.

> *Naye atazaa mwana,*. . .(Mtu huyu hapa). . .*nawe utamwita jina lake* . . .

Ati nini? [Kusanyiko linasema, "YESU."—Mh.] "Jina Lake!" ["YESU."] Sasa kumbukeni.

> . . .*jina lake YESU, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu Wake* kwa. . .*na dhambi zao.*

> *Basi hayo yote* yamekuwa*, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii* ambaye hujiliwa na Neno, *akisema,*

> *Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana; nao watamwita jina lake Imanueli; yaani, Mungu pamoja nasi.*

168 Jina la Mungu ni lipi? Jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni lipi? [Kusanyiko linasema, "YESU."—Mh.] Biblia ilisema Jina Lake lilikuwa ni "YESU."

Harafu mtu huyu hapa akikazana kulibishania wakati mmoja, hapa maskanini, alisema, "Ndugu Branham amejitoa kwenye hayo yote, lakini hataweza hili." Kasema, "Hapa inaonyesha nafsi tatu mbalimbali, hasa, kabisa." Kasema, "Mathayo, sura ya 3! *Huyu* hapa Yohana amesimama akihubiri; *Huyu* hapa Mwana anakuja, akienda zake kubatizwa. Akaingia majini, akabatizwa na Yohana; akapanda kurudi kutoka majini. Na, 'Tazama,' kasema, 'mbingu zilifunguka mbele Zake.' Kisha akasema, 'Roho Mtakatifu akashuka toka Mbinguni, kama hua akishuka. Na Sauti kutoka Mbinguni, ikisema, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ambaye. . ."' Nafsi tatu mbalimbali, kwa wakati mmoja." Loo! Jamani!

169 Naam. Inaonyesha tu kwamba watu ambao hawajabatizwa bado, wala hawajaitwa kwenye kazi ya—ya mhudumu, hawana shughuli yo yote mimbarani. Hiyo ni kweli.

Ni—ni—ningeweza kumchukua mtu huyo, sasa, kwa msaada wa Mungu, na kuwafunga kifundo hivi kwamba ingefanya kichwa chao kione kizunguzungu. Angalia, sijali kile. . .

La, simaanishi "mimi." Hilo halisikiki kuwa jema. Nisamehe. Sikumaanisha hilo, Bwana. Sikumaanisha, sasa. Nilimsikia akinikemea kwa ajili ya hilo, unaona, kwa hiyo sikumaanisha kulisema namna hiyo. Nina—ninasikitika. Naamini kuwa Roho Mtakatifu angeweza kumfunulia mtu huyo siri fulani. Hilo linasikika afadhali.

170 Ni kama tu kutuni chombo cha muziki, ukikosea. Na waweza kutambua, kama Mkristo, ulisema kitu kibaya. Yeye hakufurahishwa na jambo hilo. Unaona, hiyo ilikuwa ni mimi nikijiweka hapo. Mnaona? Mimi simo kwenye picha, hata kidogo. Mimi ninaninii tu. . .sitaki hata iwe ni mimi mwenyewe

ama cho chote kile. Ni Yeye tu, nimwache Yeye atende kazi. Yeye ndiye anayepiga. Baragumu ni bubu; ile sauti iliyo nyuma yake, ndiyo itoayo mlio.

171 Sasa, angalia hapa. Mtu huyo alifasiri Neno vibaya. Unaona, Hilo ni . . . Kumbuka, "Limefichwa kwa macho ya wenye hekima na akili; likafunuliwa watoto wachanga."

Sasa, *huyu* hapa huyo Mtu mmoja, Yesu Kristo, amesimama duniani. Sasa, Mbingu; bila shaka, kuna anga la juu. Sasa angalia. "Na Yohana anashuhudia . . . "

172 Sasa mtu huyo hana budi kusema, "*Huyu* hapa Mungu Baba; na *huyu* hapa ni Mungu Roho Mtakatifu, kama hua; na huyu *hapa* Mungu Mwana; ikifanya watu watatu." Ni kosa.

173 Yohana, akisimama nyuma *hapa*, alijua *huyu* alikuwa ni Mwana-Kondoo. Yohana alisema, "Nashuhudia, nikimwona Roho wa Mungu kama Mwana-Kondoo . . . " *Huyo* hapo Mungu Roho, mfano wa hua, namaanisha. Sasa hilo hapo jambo lile lile nililosema usiku wa hivi majuzi, mnaona; badala ya mia saba, sa- . . . Mnaona? Roho wa Mungu! Huyu alikuwa ni Mwana-Kondoo *hapa*. Na Roho wa Mungu, yule Hua, alikuwa ni Mungu. "Roho wa Mungu akishuka kutoka Mbinguni. Na Sauti kutoka Mbinguni, ikisema, 'Huyu ni mwanangu mpendwa Wangu, ninayependezwa kukaa ndani Yake.'"

"Mamlaka yote ya Mbinguni na duniani yamewekwa mkononi Mwangu." Unaona? Unaona? Unaona? Huyo Ndiye. Sasa Jina Lake lilikuwa ni nani? [Kusanyiko linasema, "YESU"—Mh.] Ndiyo. Mnaona?

174 Kwa hiyo, kadiri nadharia ya watu wa utatu, ya kuwa Miungu watatu mbalimbali, huo ni ukafiri! Hilo halikufundishwa hata siku moja katika Biblia. Halikufundishwa kamwe katika ule Ujumbe wa simba, lakini liliingizwa katika huo uliofuata, ambao ulikuwa ni upinga-Kristo. Mwulize mtu ye yote unayetaka, mwanatheolojia ye yote. Hilo halikuwahi kuja, ila tu kupitia kwenye fundisho la Wanikolai. Hiyo ndiyo sababu lilitoka likaja na Martin Luther; hiyo ndiyo sababu liliendelezwa na John Wesley; na kutapakaa katika Wapentekoste.

175 Katika siku ambayo Wapentekoste walitoka, wao waliunda kundi la "Yesu Pekee." Sasa, hilo ni makosa, tena. Yesu anawezaje kuwa Baba wa Yeye Mwenyewe? Unaona? Kwa hiyo linatupilia hilo mbali.

176 Lakini, kunapaswa kuje wakati wa tai. Unaona? Huo ndio wakati wa kunyosha siri hizo zote. Mnaona?

177 "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu" ni vyeo vya Bwana Yesu Kristo. Tazama, hivyo vyote vitatu! Mathayo alisema, "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Petro akasema: "Bwana Yesu Kristo." Baba ni nani? "Bwana alimwambia Bwana wangu, 'Keti mkono Wangu wa kulia.'" Sivyo? Baba; Mwana, Yesu; Roho

Mtakatifu, yule Logos aliyetoka kwa Mungu. "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu" ni vyeo vitatu hasa vya Nafsi ya Mungu iliyodhihirishwa katika—katika—katika njia tatu mbalimbali, ama sifa tatu Zake Binafsi.

178 Na ili kulifanya dhahiri, kwa mtu ambaye hangeelewa, ni kama ofisi tatu za Mungu yule yule. Kwa kweli, ni sifa tatu za Mungu yule yule. Mungu akitenda kazi katika ninii tatu, mbalimbali; chini ya Ubaba, chini ya Uwana, chini ya kipindi cha wakati wa Roho Mtakatifu. Mungu hukamilishwa katika tatu. Mnakumbuka namba ya mpinga-Kristo, nne? Unaona? Mungu, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," ni "Bwana Yesu Kristo" kabisa.

179 Mnapobatiza, Jina la "Yesu" pekee, hilo ni kosa. Kuninii tu, "Nakubatiza katika Jina la Yesu," hilo ni kosa kabisa. Ninawajua Yesu wengi. Mbona, nchi za himaya ya Kirumi zimejaa hao, akina Yesu.

180 Lakini huyu ni "Bwana Yesu Kristo," linaonyesha Yeye ni nani hasa.

181 Kuna akina Branham wengi, kama ukitaka kunena habari zangu mimi binafsi, lakini mimi ni—mimi ni William Marrion Branham pekee. Huyo—huyo ni mimi. Lakini kuna William Branham wengine wengi, na kadhalika, kila mahali.

182 Lakini hili linataja Mtu mmoja waziwazi, Bwana Yesu Kristo, unaona, Yule Mtiwa mafuta. Kuna Mmoja wao tu. Sasa, hiyo ni Kweli.

Kwa hiyo kama kuna la zaidi juu ya jambo hilo, andika barua ama cho chote kile, ama—ama wakati mwingine nikiwa niko kwenye maswali mengine. Nataka kujaribu kupata hili, ili niweze kuona kama tunaweza kuwaombea baadhi ya hawa watu wagonjwa wanaoteseka.

184. Ndugu Branham, endapo swali hili hali—halifai, halifai kwenye ninii. . . usilijibu. (Hilo ni jambo zuri. Nafurahia hilo.) **Ni watoto gani—ni watoto gani watakaonyakuliwa, iwapo kuna wo wote wachanga? Asante.**

Hawakuandika jina lo lote. Sasa, usipoliandika, si lazima.

183 Lakini, angalia. Mungu anapoandika jina kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwan-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, hakuna kitu cho chote ulimwenguni kinachoweza kulifutilia mbali, kwa sababu limeandikwa na wino wa Damu ya Kristo. Liwe ni kubwa *hivi*, ni kubwa *hivyo*, au *ni kubwa hivyo*, ama vyo vyote inavyoweza kuwa, ni vile vile tu. Mnaona? Watoto wote, Kanisa lote, cho chote kilichoko, ni . . . Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani.

184 Sasa, hatujui. Unasema, "Ndugu Branham, waweza kuthibitisha kuwa wewe umo?" La, bwana. Siwezi kuthibitisha jambo hilo. Mungu angeweza kunitumia mimi kama chombo cha

kitu kingine, na akutumie wewe vivyo hivyo. Lakini naamini, na kwa imani, nimeokolewa. Sijaokolewa kwa maarifa; kwa imani! Hivyo ndivyo unvyookolewa. Hivyo ndivyo sisi sote tunavyookolewa.

185 Lakini, kumbuka, Mungu hana kikomo. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Hana kikomo! Vema, akiwa hana kikomo, hiyo inamfanya Yeye . . . Na, tena, Yeye anajua yote. Mnaamini jambo hilo? ["Amina."] *Kujua yote* linamaanisha "Yeye anajua mambo yote." Yeye hawezi kuwa—hawezi kuwa mjua yote pasipo kuwa asiye na kikomo. Mnaona, hapajawahi kuwapo na cho chote ila kile Yeye alichojua. Yeye alijua kila mbu mdogo atakayekuwako duniani na ni mara ngapi angepepesa na kufumbua macho yake, na angekuwa na shahamu kiasi gani, kiasi gani cha jumla yao ya pamoja. Alijua kila pumzi ambayo ungevuta, na kina gani kule kupumua kungeingia mapafuni mwako. Hiyo ni kutokuwa na mpaka.

186 Sasa, kama Yeye hana mpaka, hilo linamfanya ajue yote. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Na ikiwa Yeye anajua yote, hilo linamfanya awe mahali pote, kwa sababu Yeye anajua vizuri ile dakika hasa, saa, wakati, hadi kwa usahihi wa kiasi cha elfu hamsini na tano ya sekunde, kwamba litatukia lini. Unaona? Umepata wazo hilo sasa? ["Amina."] Basi, Yeye anajua mambo yote. Na hiyo ndiyo sababu Yeye ana mamlaka yote, anajua mambo yote, na aweza kufanya mambo yote.

187 Sasa, hebu tuone. Sasa, "Na watoto wote ambao Mungu . . . Kila mtu ambaye Mungu . . . Wakati wao . . . " Sasa, kumbukeni, ni wakati gani Yesu . . . Biblia ilisema . . .

188 Sasa tunajua ya kwamba Yesu aliuawa yapata 30 B.K. Sivyo? Yapata, ilikuwa kama katikati ya mwaka, nadhani, 30 B.K.

189 Sasa, lakini Biblia ilisema ya kwamba Yeye alichinjwa kabla ya kuumbwa kwa dunia. Na jina lako, wakati kile Kitabu cha Mwana-Kondoo . . . Mwana-Kondoo alipochinjwa, kukikomboa Kitabu hiki . . . Hapa kuna jambo kuu sasa. Huenda likasababisha changamko. Tazama. Wakati ninii— wakati ninii— wakati Mwana-Kondoo . . . Sasa kumbuka, Biblia ilisema kile kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kiliandikwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na jina lako liliandikwa humo, lilikuwa kwenye kile Kitabu wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, apate kukomboa kila jina lililoandikwa katika Kitabu hicho. Unaona? Mmelipata sasa?

190 Mnaona, hakuna kitu kisicho katika utaratibu. Inatendeka barabara kabisa kama tu saa kuu ya Mungu, unaona, kama saa kubwa inayozunguka moja kwa moja. Jina lako liliandikwa mle ndani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati yule Mwana-Kondoo alipochinjwa apate kukomboa kile kilichokuwa

katika Kitabu hicho. Na sasa Yeye anajitokeza na kukichukua Kitabu hicho, apate kudai alichokomboa.

Sitaki kuanza mambo hapo; hatungeweza kujibu swali lingine leo. Vema. Swali:

185. Je! kuzimu, na ziwa linalowaka moto na kiberiti, ni mahali pamoja?

191 La. Kuzimu, tafsiri katika Biblia, naamini . . . Sasa, kuna wanachuoni wanaoketi hapa, nami nataka kuheshimu jambo hilo. Ndugu yetu Iverson anayeketi hapa, na Ndugu Vayle, na wengi wa hawa ndugu ambao ni wanatheologia kweli. Neno hilo likitafsiriwa, *kuzimu* maana yake ni "kaburi." Sivyo? Neno la Kiyunani la kaburi. Lakini Ziwa la Moto ni kitu kingine. Kwa sababu, hapa katika Ufunuo, "Kuzimu na vyote pia, vilitupwa katika Ziwa la Moto." Unaona? Vema. Sasa hebu tuone.

186. Ikiwa sivyo, je! Ziwa la Moto, na kuzimu, ni vya Milele?

192 La, bwana. La, bwana. Cho chote kilichoumbwa si cha Milele. La. Kila kitu kilichoumbwa . . . Hiyo ndiyo sababu hakuwezi kuwa na kuzimu ya Milele. Mtu ye yote akikwambia utachomwa moto kuzimu milele nataka Andiko kwa jambo hilo. Unaona? Hakuna kitu kama hicho.

193 Kuzimu iliumbiwa Ibilisi na malaika zake, kwa ajili ya mpinga-Kristo na watu wake; huyo alikuwa ni Ibilisi, Ibilisi aliyefanyika mwili. Kuliumbiwa hao, kusudi wakaangamizwe. Na cho chote ambacho kilikuwa na ninii . . . Cho chote . . .

194 Kuna jambo moja tu, kabisa, kutoka katika kila kitu kilichopo, ulimwengu wote na cho chote kile, kuna kitu kimoja tu kilicho cha Milele, nacho ni Mungu. Kabla hapajakuwapo na atomi, ama elektroni, ama kabla hakujakuwapo na hata mialimwengu, elektroni ama cho chote kile, Yeye alikuwa ni Mungu. Yeye ni Muumba.

195 Na hiyo ndiyo njia ya pekee unayoweza wewe kuwa wa Milele, ni kuupokea Uzima wa Milele. Neno hilo la Kiyunani hapo, nafikiri, ni *Zoe*. Sivyo? Zoe. Zoe. Na ndipo, Uzima hu—huo, Mungu anakupa. Kama vile baba, baba yako, anavyokupa uhai wake, kwa kupitia na—nadhiri ya ndoa kwa Mama yako; naye, kwa kufanya hivyo, anakupa fu—furaha ya kukupa, (nieleweni) ya kutoa uhai kwa mwana. Na hivyo ndivyo Mungu afanyavyo, furaha ya kutoa Uzima Wake kwa mwana. Unaona? Na ndipo unakuwa sehemu Yake, ambayo ni Zoe, Uzima wa Mungu Mwenyewe. "Nawapa Uzima wa Milele."

196 "Kuwafufua, katika siku ya mwisho." Hicho ndicho kitu pekee ambacho—ambacho . . . Mna Uzima wa Milele. Na huo Uzima wa Milele unajua mwili wake, nao hapana budi ujitokeze. Kwamba unaweza . . . Haiwezekani kwa huo kukaa hapo. Kama vile Roho wa Kristo alivyozunguka-zunguka juu ya ule mwili,

Roho wa Mungu juu ya Kristo, katika siku ile kuu, ulijua ungefufuka tena; vivyo hivyo na watakatifu katika miili yao.

197 Sasa kumbuka. Yesu, alipokufa, alienda kuzimu. Maana, ilimbidi kwenda huko; Yeye alikuwa kizuizi cha dhambi. "Naye alizihubiria zile roho zilizokuwa kuzimu, ambazo hazikutubu katika ule uvumilifu, siku za Nuhu." Sivyo? Yeye alienda kuzimu na akazihubiria zile nafsi, nafsi zilizotengwa na Mungu. *Mauti* maana yake ni "utengano." Na wao walikuwa wametengwa na Mungu, hawangeweza kurudi tena. Na Yesu alikwenda kuwashuhudia ya kwamba Yeye ndiye aliyenenwa habari Zake—yule Mzao wa mwanamke.

198 Ule uzao wa nyoka, mnaona kile uzao wa nyoka ulichotenda? Mpinga-Kristo; anaishia mautini, utengano, yule farasi mwekundu. Mzao wa mwanamke, Uzima, unaishia kwa yule farasi mweupe, Yesu Kristo. Mnaona? Ni nini? Mmoja akipingana na mwingine, uzao wa nyoka ukipingana na Mzao wa mwanamke. Mnalipata sasa? Loo! tungeweza kudumu muda mfupi juu ya jambo hilo! Je, jambo hilo lisingekuwa zuri? Lakini hebu na tuendelee na hili.

187. Ndugu Branham, je! yule mpanda farasi wa kwanza, Muhuri wa Kwanza, anatimiza Wathesalonike wa Pili, "kule kufunuliwa kwa yule asi"?

199 Ndiyo. Hiyo ni kweli. Huyo anaitimiza. Hilo ni rahisi. Huyo anaitimiza. Huyo ndiye yule asi. Mtu huyo huyo anaendelea tu, katika hatua, akipanda farasi mpaka atakapompanda yule farasi wa kijivujivu anayeitwa "Mauti." Kristo anashuka moja kwa moja, kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa, ahadi kwa farasi mweupe, na huyo ndiye ule Uzima, mnaona.

188. Ilikuwaje kwa wale waamini waliozaliwa mara ya pili walio katika madhehebu mbalimbali ila hawako katika Bibi-arusi wa Kristo? Inakuwaje kwao?

200 Vema, nafikiri tulielezea hayo, muda mchache uliopita. Unaona? Wanaingia katika ile Dhiki. Wanauawa katika ile Dhiki. Wanafufuka katika ule wa mwisho, baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu, wapate kuhukumiwa. Unaona? Kwa sababu, Biblia ilisema kuwa hao wengine walio hai. . . "Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu." Halafu kulikuwako na ufufuo, na kisha wakafufuka wenye haki na wasio haki, nao wakahukumiwa na Kristo pamoja na Bibi-arusi. Yeye alikuja ulimwenguni pamoja na elfu kumi mara elfu kumi ya watakatifu Wake. Sivyo? Bibi-arusi Wake.

201 Hukumu ikawekwa. Vitabu vikafunguliwa. Vitabu vikafunguliwa. Na Kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho kilikuwa ni Kitabu cha Uzima. Hapo Yeye akawatenga, mbuzi na kondoo. Sivyo? Hilo halikumhusu Bibi-arusi. Yeye alikuwa amesimama papo hapo hukumuni, pamoja na Malkia wake. . . Malkia na Mfalme, pamoja. "Yeye alikuja pamoja na watakatifu

Wake; kumi elfu mara elfu walimtumikia," mke Wake. Ndipo hukumu ikawekwa, ndiposa kondoo wakatenganishwa na mbuzi. Kumbukeni juzi usiku nilipoleta lile tafakari dogo, mpate kufahamu, lile tafakari la mchungaji? Unaona? Haya basi.

202 La, wao, wao ndio wananinii, ka—ka—kanisa, watu walio kwenye madhehebu, ambao—ambao ni Wakristo halisi, waliopokea Ujumbe nao hawataufahamu. Hautahubiriwa kwao. Na wale walio katika makundi yaliyochanganyikana, ambalo watahubiriwa Huo, utawapita tu, isipokuwa jina lao lilikuwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Naam. Lakini watakuwa ni watu wazuri.

203 Nao watafufuliwa tena na kuhojiwa, na kuhukumiwa na kundi lile lile lililowahubiria. "Au hamjui watakatifu watauhukumu ulimwengu?" Watahubiriwa, mnaona. Watahubiriwa, na watu wale wale waliowashuhudia Ujumbe, wa "Kutoka kwenye kitu hicho!" Mnaona? Natumaini hayo yanalielezea. Ninayo mengi sana hapa.

189. Ndugu Branham, je! yule Malaika wa Saba, aliye na roho wa Eliya, ndiye mtu yule yule akiwa ndiye Eliya anayetumwa kwa wale Wayahudi mia na arobaini na nne elfu katika kipindi kile kile cha miaka mitatu na nusu baada ya kule Kunyakuliwa? Wengine wetu tumechanganyikiwa, na jambo hili.

204 La. Si mtu yule yule. Unaona, ni watu wawili mbalimbali. Yule Elisha aliyekuja katika jinsi ya Eliya hakuwa Eliya. Na roho wa Eliya aliyekuja juu ya mtu aliyeitwa Yohana Mbatizaji hakuwa Eliya. Wala mtu yule aliye mjumbe malaika wa saba, mwishoni mwa Wakati wa Laodikia, hatakuwa yule Eliya mwenyewe hasa. Yeye atakuwa Mmataifa, kwa watu wake.

205 Eliya ataninii, ama Roho wa Eliya basi, akija ndani ya nanii. . .na kwa watu kule, yeye atakuwa Myahudi, unaona, kwa sababu wao wanatumwa kwa watu wao wenyewe. Huo ndio ufunuo wangu. Sababu ya mimi. . .Ya Tommy Osborn, tulipoongea naye kuhusu hayo, wakati ule, mimi na Tommy, sikujua kamwe. Nilikuwa tu nikiwaombea wagonjwa.

206 Ndipo nikaja pale, na kulikuwa na mama mmoja aliyekuja kumetoka Maskani ya Injili iliyoko Fort Wayne, mmishenari katika nchi za nje. Titi lake lilikuwa kubwa *hivyo*, lilikuwa limeliwa tu na kansa. Naye alikuwa papo hapo kwenye ile nyumba ndogo ambamo tulikuwa tukiishi, hapa uchochoroni. Nami nilimwombea dada huyo mpendwa. Naye aliponywa, na akarudi hudumani. Na ndipo. . .Alitokea huko Afrika. Naye alikuwa ameacha kitabu kidogo pale, kuhusu safari za misheni.

207 Ni—nikawazia, "Vema, wamishenari ni watu wazuri." Nami ni. . .sijawaza mengi kuhusu wamishenari. Na kwa hiyo nikawaza, "Vema, wao ni huduma ya Mungu nje huko. Kwa hivyo hiyo ni. . .Mahali pangu ni papa hapa, katika Barabara

ya Nane na ya Penn.” Kwa hiyo nilikuwa tu nikiendelea vizuri nilivyoweza.

208 Lakini siku moja, nikiwa nimeketi katika chumba cha kujisomea, nikakichukua kile kitabu. Nacho kilikuwa na picha ya—ya watu Weusi, baba mmoja mzee, naye alikuwa na mzingo huu mdogo wa nywele. Na chini yake imeandikwa hivi, “Mzungu, mzungu, baba yako alikuwa wapi? Unaona? Mimi sasa ni mzee na akili zangu zimefifia, nami sifahamu vizuri sana. Kama ningalimjua Yesu wakati nilipokuwa kijana, ningalimpeleka kwa watu wangu.” Vema, nilikisoma.

209 Na kitu fulani kilikazana kusema, “Kisome tena, kisome tana.” Niliendelea kusoma. Loo! mmekuwa na nyakati kama hizo. “Kirudie tena na tena. Kuna kitu fulani humo ndani.”

210 Kama juu kule siku ile kule Green Mill, nilipotoka mle pangoni, sikuweza kuelewa jambo hilo, jinsi watu wangeweza kunena kwa lugha na kupiga makelele, na wakiwa na Roho Mtakatifu halisi, na bado wewe ni mpinga-Kristo. Wanene kwa lugha, wanene kwa lugha halisi za Roho Mtakatifu, na hata hivyo wawe ni ibilisi. Hiyo ni kweli. Ninaweza kukuthibitishia jambo hilo. Ndiyo, kweli. Na halafu tazama . . . waliposimama pale.

211 Kwa hiyo, lugha si thibitisho la Roho Mtakatifu. Ni moja ya vipawa vya Roho Mtakatifu. Unaona? Na Ibilisi anaweza kuiga cho chote alicho nacho Yeye, uponyaji wa Kiungu na mengine yote.

Yeye alisema, “Wengi watanijia katika siku hiyo, na kusema, ‘Bwana, si nilitoa pepo? Si nili-. . .’” Hiyo ni kuhubiri Injili. “‘Si nilifanya kazi nyingi katika Jina Lako, na mambo haya yote pale?’ Nitasema, ‘Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Hata sikuwajua.’”

212 Biblia ilisema, ya kwamba, “Mvua hunyeshea wenye haki na wasio haki, vile vile.” Na gugu lile lile, lililo huko shambani, laweza kufurahi na kupiga shangwe vile vile, ya maji yale yale yaliyolishukia, kama mvua inavyotumwa kwa vyote viwili. “Lakini kwa matunda yao mtawatambua.” Maskini gugu hilo dogo linaweza kusimama hapo juu, na likiwa na furaha na kushangilia liwezavyo kushangilia, limejawa tu na mvua ile ile ambayo ngano inayo.

213 Ona basi. Kwa hiyo wao wanaweza kupiga makelele, wanene kwa lugha, na kuiga cho chote watakacho; katika siku hiyo, waitwe, “Watendao maovu.”

214 Kama nilivyowaambia, kitambo kidogo kilichopita, sikilizeni ninayosema! Sikilizeni kwa makini! Chunguzeni kule nyuma, jichunguze mwenyewe kwa Neno uone ulipo.

215 Ninyi wanawake mlio na nywele fupi, ziacheni zikue. Mkiwa mnavaa kaptula; zivueni. Enendeni kama wanawake wanaostahili heshima. Ninyi wanaume ambao mngali mnavuta

sigara, na kukimbia kwenda kwenye kumbi za kuchezea kamari, acheni. Sijali unakiri kiasi gani. Ikiwa ungali unashikilia madhehebu hayo, na kusema, "*Hili* ndilo la Kweli," na "*hili* ndilo la Kweli," heri uache. Angalia huko nyuma, ulichunguze na Neno. Tunatoka nje kabisa ya . . .

216 Tunapaswa kuwa tunaishi kupita mambo ya kuwa na nywele fupi na kadhalika. Wakati huu sasa, tumerudi kwenye Jambo fulani sasa, ambapo Mungu anafunua siri zilizofichwa, zilizowekwa kwenye kile Kitabu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na hao waliotii katika mambo haya madogo, watalipata katika mambo haya mengine. Kama hawakutii, yatawapita, kadiri mashariki ilivyo mbali na magharibi. Itakuwa tu . . .

217 Kama vile Gideoni, aliwatenganisha watu wake. Kulikuwako na maelfu na maelfu. Mungu akasema, "Hao ni wengi kupita kiasi. Wagawe tena." Akawapa jaribio lingine. Na, "Wagawe tena. Wagawe tena." Na kuendelea tu, mpaka akawa na kundi dogo sana. Akasema, "Hilo ndilo kundi ninalotaka litekeleze kazi hiyo." Hivyo ndivyo ilivyotendeka hasa.

218 Wanawake wa Kipentekoste (wakienda huku na huku) wameketi pale, wakisikia na kujua, kwa Neno, hilo ni kosa. Unadhani watalizingatia? La, bwana. Kila mwaka, ninapopitia hapa, kuna wengi zaidi wenye nywele zilizokatwa kuliko ilivyokuwa nilipoanza.

219 Sema, "Linakuhusuje . . . Unapaswa kuninii . . . " Mtu fulani alisema, "Mbona, Ndugu Branham, watu wanakuchukua wewe kama nabii." Sasa, sisemi mimi nilikuwa nabii. Hakuna mtu amenisikia nikisema hivyo. Lakini nitasema hivi, ya kwamba kama—kama ulifanya jambo hilo, kama unalichukua kuwa hivyo . . . Sema, "Mbona usiwafundishe watu jinsi ya kumpokea Roho Mtakatifu, na jinsi ya kupata *hili*, na jinsi ya kupata karama kuu za kiroho wakalisaidie kanisa?"

Nawezaje kuwafundisha alijebra hali hata hawatasikiliza ABC zao? Hiyo ni kweli. Timizeni mambo haya madogo. Rudini nyuma hapa mwanzoni na kuyapangusa, na mwanze vizuri. Amina. Vema.

220 Nilikuwa nikinena kuhusu nini, hata hivyo? Hebu tuone. Sikukusudia kuliacha somo hilo. Samahani, mnaona. Vema. "Wengine wananinii . . . wengine wetu tumechanganyikiwa. Je! yule Eliya ni yule yule . . . ?" Naam, en-hee, hiyo ni kweli.

La. Eliya huyu atakayekuja kwa Mataifa, atakuwa ni Mmataifa aliyetiwa roho huyo, kwa sababu Mungu alimtumia roho yule yule kuwatoa watu Wake kwenye mchafuko kila mara. Naye alitimiza kusudi Lake vema, kwa hiyo Yeye anamshusha moja kwa moja tena. Kwa sababu, mnaona . . .

Sababu, sasa, kama Yeye akimtumia mwenye akili nyingi sana, aliyesoma sana, angewapata watu wa aina hiyo.

221 Yeye anamleta mtu ambaye hata hajui ABC zake, na hawezi kutamka maneno yake vizuri, na kila kitu namna hiyo; kitu fulani cha kizee kutoka huko mbali jangwani mahali fulani, na anakileta na anakipenyeza kwa watu wanyofu. [Ndugu Branham anadata kidole chake mara moja—Mh.] Nao wanalipokea, namna hiyo. Wanalipokea, unaona. Kama lingekuja, na ukosi . . .

222 Kama Paulo alivyosema, "Sikuja kwenu na uthabiti wa elimu, lakini nilikuja kwenu kwa Nguvu za ufufuo." Ilimchukua Mungu miaka mitatu na nusu, huko Uarabuni kule, kuiondoa ndani yake, elimu yake. Ili—ilimchukua Yeye miaka arobaini kuiondoa ndani ya Musa. Unaona? Kwa hiyo, ndio hivyo. Hiyo . . .

Sisemi Mungu haninii . . . Siungi mkono kutojua kusoma sasa, lakini nina—ninajaribu kuwaambia haihitaji . . . Elimu haininii . . .

223 Hekima ya ulimwengu huu iko kinyume. Elimu imekuwa ni kipingamizi kikuu sana ambacho Injili imewahi kupata. Kama tusingekuwa na elimu, hatungekuwa na seminari hizi zote kubwa na mambo tuliyo nayo sasa. Ingekuwa ni watu, wanyofu, ndio ambao wangesikiliza Neno. Lakini watu wameerevuka sana na kufarakana, na kugandamana huko, pamoja na hayo yote, hayo madhehebu, mpaka hivi kwamba wataotea mizizi humo. Basi. Wao huchukua roho huyo. Je! umepata kuona mwanamke mwema mzuri, akiolewa na mwanamume mbaya sana? Aidha huyo mwanamume mbaya sana huwa mtu mzuri mwe—mwema kama yule mwanamke alivyo, ama mwanamke huyo anakuwa mbaya sana kama mumewe alivyo. Unaona? Hiyo ni kweli.

224 Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, "Tokeni kati yao, ninapojitayarisha kufanya huo Unyakuo." Yakubidi uwe na namna fulani ya imani itakayokuondoa hapa.

190. Ni lini lile Agano, la Danieli 9:27, lilipofanywa kwa muda wa juma moja?

225 Nusu yake ilifanywa, lile agano, wakati Yesu Kristo alipokuwa hapa duniani akiwahubiria Wayahudi. Yeye hakuwaendea Mataifa, kamwe. Naye aliwaambia wanafunzi Wake, "Msiwaendee Mataifa." Hilo lilikuwa kwa Wayahudi, peke yao. Unaona? Naye alihubiri kwa miaka mitatu na nusu. Hiyo ni nusu ya lile juma la sabini, sasa, kama vile Danieli alivyosema Yeye angefanya.

226 Sasa kumbuka, Yeye alithibitishwa mathubuti kwa Myahudi. Lakini macho yao yalipofushwa, kuleta hii nafasi ya Mmataifa. Je, huwezi kuona mpango huo mzima? Unaona? Naye alijithibitisha Mwenyewe, kwamba ni nabii, akatenda hasa yale nabii angelitenda, akawaonyesha ishara ya nabii. "Ambayo, Neno lenu wenyewe lilisema, 'Mtu akisema yeye ni wa kiroho, au nabii, chunguzeni anayosema; na yakitimia, yakiendelea tu kutimia, yale yeye aliyosema, sikuzote.'"

227 Kama vile, unaangalia katika Biblia, ilisema, “Bisheni, itafunguliwa; tafuteni, mtapata; ombeni, mtapewa.” Sasa, ukichunguza, ni “abishaye.” Anayendelea tu kubisha. [Ndugu Branham anaanza kugongagonga mimbarani mara ishirini na tatu—Mh.] Endelea kukaa papo hapo. Kama yule kadhi dhalimu, ambaye hangemsikiliza yule mwanamke; yeye aliendelea tu kubisha mlangoni pake. Akisema, “Mimi nimo mkononi mwako.” [Ndugu Branham anaacha kugonga.] Si kutafuta, useme, “Bwana, ningetaka kupata *hiki*. Amina.” Si hivyo. Kaa papo hapo mpaka ukipate. Unajua kitakuja. Kwa hiyo, Yeye aliahidi jambo hilo, kwa hiyo, kaa pa po hapo mpaka utakapolipata. Unaona?

Sasa, sasa, katika sehemu ya mwisho, lile juma la sabini, sehemu yake ya mwisho itakuwa katika wakati wa ile Dhiki, baada ya Kunyakuliwa kwa Kanisa. Ndipo hii hapa ile miaka mitatu na nusu hapa, ambapo litathibitishwa kwao tena na manabii, mnaona, Musa na Eliya, Ufunuo 11. Sasa, hebu na tuone hili lina nini:

191. Kama wewe ni mmoja wa wateule Wake, je! utanyakuliwa katika Bibi-arusi? (Ndiyo. A-ha. Ndiyo, bwana. Hilo ni rahisi.)

192. Ndugu Branham, ulimaanisha kusema elfu saba ambao hawakupiga goti lao kwa Mabaali, au mia saba?

228 Elfu saba, ndivyo nilivyokusudia kusema. Nisameheni kwa jambo hilo, unaona. Ninii tu . . . Ni ninii—Ni kuteleza kwa ulimi tu. Nilikuwa tu . . .

Kama vile, niliyosema muda mfupi uliopita. Je! mliniona nikisimama hapa, nilisema, “Na—nao wanashuhudia, wakimwona Mwana-Kondoo . . . ”? Unaona? Unaona? Mwana-Kondoo alikuwa duniani. Unaona? “Akashuhudia, nalimwona Roho wa Mungu akija juu ya Mwana-Kondoo.”

229 Sasa, ndani hapo, ilisema, “Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa naye.” Unaona? Sasa, hayo yameandikwa katika utaratibu halisi wa Kiyunani, kuweka kitenzi kabla ya kielezi. Lakini unaona hapa, kweli ni hivi. Sasa hebu chukua tu Neno hilo, unaona. Biblia inasema, katika tafsiri ya James Mt. hapa, “Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu, ninayependezwa kukaa ndani Yake.” Lakini, hasa, kama tungelilisema kama tunavyosema siku hizi, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, nipendaye kukaa ndani Yake.” Ungeipindua, unaona. Unaona? “Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa kukaa ndani Yake.” Unaona? Sasa, tungeyasema siku hizi, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa kukaa ndani Yake.” Unaona, neno lile lile, unaligeuza tu. Unaona?

230 Sasa, naam, nilikusudia . . . Samahani, tafadhalini. Mimi . . . Na—na, ndugu, ninyi mlio huko nje kwenye kanda, na marafiki, sikilizeni. Sikumaanisha kusema jambo hilo namna hiyo. Mi—

mi—mimi ni mhudumu wa Injili. Mimi, kadiri nilivyohubiri hilo mara nyingi, nilijua hao walikuwa ni elfu saba. Ilitokea tu kwamba nilisema mia saba. Sikumaanisha tu mia saba. Nilikusudia, ninyi . . . Sikulisoma tu kutoka katika Maandiko. Liliingia tu mawazoni mwangu nilipokuwa nikiongea, nami nikasema tu mia saba badala ya elfu saba. Nafanya makosa hayo kila wakati. Mmimi ni—hakika mimi nina kichwa kigumu, kwa hiyo mnisamehe. Unaona? Sikukusudia kufanya hivyo.

193. Je! Bibi-arusi wa Kristo na ule Mwili wa Kristo ni kitu kile kile?

231 Naam, bwana! Unaona? Sasa, hapa, sasa unaona, sitaki kuyaanza hayo, kwa sababu ningehu- . . . hubiri mahubiri juu yake, unaona. Lakini sitafanya hivyo. Lakini nataka kuwaonyesha. Mungu alipompa Adamu bibi-arusi wake, toka ubavuni mwake, alisema, "Huyu ni nyama katika nyama yangu, na mfupa katika mifupa yangu." Hiyo ni kweli?

232 Mungu alipompa Kristo Bibi-arusi Wake, Roho alimpa Bibi-arusi mwili, Yeye alitobolewa, alichomwa ubavuni chini ya moyo Wake, na maji, Damu, na Roho, vikatoka; huyo akawa "nyama katika nyama yake, na mfupa katika mfupa Wake." Sisi ni nyama na mifupa; Bibi-arusi atakuwa ni nyama na mifupa ya Kristo, sawa kabisa. Wao ni . . . Huyo ndiye Bibi-arusi Wake.

194. Je! Bibi-arusi wa Kristo atakuwa na . . . Je, Bibi-arusi wa Kristo atakuwa na huduma kabla ya Kunyakuliwa?

233 Hakika. Hiyo ndiyo inayoendelea hivi sasa, unaona, Bibi-arusi wa Kristo. Bila shaka. Ni Ujumbe wa wakati huu, unaona, Bibi-arusi wa Kristo. Hakika. Anao mitume, manabii, waalimu, wainjilisti na wachungaji. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."Mh.] Huyo ni Bibi-arusi wa Kristo. Hakika. Yeye ana huduma, huduma kuu, huduma ya majira haya. Itakuwa nyenyekevu sana.

234 Sasa, kumbuka. Ni wangapi waliokuwapo hapa, mara ya kwanza, wakati mimi . . . Jumapili iliyopita, unaona, mnakumbuka kile nilichohubiri? *Unyenyekevu.* Loo! msisahau jambo hilo. Nitasimama kidogo, kuwaonya hilo tena. Kumbukeni, Mungu anapotabiri jambo lo lote kuu kutokea, watu wanaangalia mbali sana, kwa hekima yao, mpaka wanapitwa na yanayotendeka. Mungu anaposema jambo lo lote ni kuu, ulimwengu unalicheka. "Hilo kundi la wajinga!" Hiyo ni kweli.

Lakini wakati watu wakuu, na lile kanisa kuu, limesema, "Jamani, hilo ni jambo tukufu mno!" Mungu anasema, "Kundi la wajinga!" Kwa hiyo, unaona, yakubidi uwe mwangalifu. Simaanishi huenda inaweza kuwa namna hiyo, namna hiyo kabisa, lakini hivyo ndivyo ilivyo.

235 Tazama! Hapa palikuwapo na kanisa kuu takatifu, la Kiorthodoksi, "Tunajua Neno. Tuna mashule. Tuna maseminari.

Mtu wetu ameelimishwa vilivyo! Mbona, kwa mamia ya miaka tumekuwa waaminifu kwa Yehova. Sisi ndio Kanisa halisi. Sisi ni Baraza kuu la Kiyahudi. Tuna Baraza la Makanisa hapa. Mafarisayo na Masadukayo pia, na madhehebu yote, yanakusanyika pamoja," kama inavyotendeka. Unaona? "Sisi sote tuko katika moja, Ba—Baraza la kanisa. Sisi ndio watu mashuhuri hapa. Tunayajua hayo Maandiko. Hiki kijitu kipumbavu chini huko mtoni, chenye ndevu zinazoning'inia usoni mwake, na kipande cha ngozi ya kondoo, kinatuambia nini?" Kwa kweli, wao hawangeyasikiliza.

236 Lakini Biblia ilisema, katika Malaki sura ya 4 . . . ama sura ya 3, "Nitamtuma mtumishi Wangu mbele ya uso Wangu, kunitengenezea njia." Miaka mia saba na kumi na miwili kabla ya wakati huo, Yohana . . . Loo! yule nabii mkuu Isaya alisimama pale, na kusema, "Kutakuwako na sauti ya mtu aliaye nyikani. 'Itengenezeni njia ya Bwana, na yanyosheni mapito Yake.'" Hiyo ni kweli. Kisha kasema . . . na Dau- . . . Loo! wengi wao! Sema, "Kila mahali pa juu patashushwa."

237 Loo! wao walisema, "Kutakuwako na . . . Mtu huyu ajapo, Yeye atanyosha kidole chake, na ataing'oa milima. Loo! na mabonde yote, mahandaki, yatajazwa. Ndipo mahali pote, yaani mahali pote palipoparuza, patalainishwa. Ndugu, tutapanda mahindi katika kila shamba hapa. Na, lo, tutafanya mambo makuu mtu huyu atakapokuja." Unaona?

238 Walikuwa wakimtarajia Mungu kuchukua kombo na kuizungusha, na kushusha ngazi, aseme, "Shuka chini, ewe mtangulizi mkuu wa Masihi Wangu." Na ndipo mara tu yeye aondokapo, wataivuta kuirudisha juu, na huduma yake imekwisha. Wanaizungusha tena, na kuiweka papa hapa chini kando ya seminari, na kusema, "Vema, Mwanangu mpendwa, shuka chini na ukawaambie." Unaona? Loo, jamani!

239 Tazama, Yeye alipokuja. Kitu cho chote kilitendeka? Hapa akaja mtu asiyejua shule yao yo yote. Hata hakuwa na kadi ya ushirika. Loo! Yeye hakuwa na vitambulisho vyo vyote. La. Hakuna mtu aliyepata kujua aliwahi kwenda shuleni hata siku moja maishani Mwake. Hata hungeweza kujua hayo kwa kuongea kwake. Yeye hata hakutumia istilahi ya nanii . . . ya makasisi. Aliongea kuhusu nyoka, mashoka, na majangwa, na—na—na mambo ya jinsi hiyo, unaona, miti. Hakuzungumza katika msamiati wa utaratibu wa kikasisi. Alizungumza si kwa msamiati wa kikasisi uliotumiaka katika siku hizo, wala wa siku hizi, wala wa siku nyingine zo zote.

240 Yeye alikuja "kishamba," kama tusemavyo hapa Indiana. Alitokea mwituni mahali fulani. Hata hakuwa amenyolewa, na nywele zake kichwani zimesimama. Sidhani yeye alioga; mara moja kila baada ya miezi miwili au mitatu. Vema. Usiku hakuvaa

pajama hata. Hakupanda gari hata kidogo. Hakupiga mswaki. Loo, jamani! Huyu alikuwa ni mtu wa namna gani! Hasha.

241 Huyu hapa anakuja, akitembea kwa kishindo akitokea nyikani, namna hiyo, na anasema, “Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani. Itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito yake!”

242 Baadhi ya waalimu walisimama na kusema, “En-hee! Aisee, aloo, una ninii yako. . .Hatuwezi kushirikiana nawe katika mkutano huu. Hapa, hatuwezi kufanya jambo hili. Vema, ninii yako iko wapi—kadi yako iko wapi? Kitambulisho chako kiko wapi?” Aliwapuuza tu. Alikuwa na ujumbe, kwa hiyo yeye aliendelea tu nao, unaona, aliendelea tu kuhubiri vile vile.

243 Wakasema, “Aha, ngoja! Vema, kama tukienda huko, tutampeleka askofu, leo, tuone yeye atasema nini juu ya jambo hilo. Tutashuka huko kama tunajua. Hao ni viongozi wa kanisa. Nasi tunajua ya kwamba itambidi kutambua jambo hilo. Kama yeye ni wa Mungu, yeye atawatambua maaskofu wetu.”

244 Akawapanga wote mstarini, na kuwasimamisha kule, hao watu mashuhuri.

245 Akasema, “Enyi uzao wa nyoka! Enyi nyoka nyasini!” Kosi zimepinduliwa, na “mababa watakatifu,” na kadhalika. “Ni nani aliyewaonya ninyi kuikimbia hasira itakayokuja? Mnajua saa yenu i karibu. Wala msiwazie kwamba. . .Mnasema, ‘Vema, sisi ni washiriki wa *hiki, kile*.’ Nawaambieni, Mungu nimtumikiaye anaweza kumwinulia Ibrahimu watoto katika mawe haya.” Loo! jamani!

246 Sasa atanena kinyume chake, kinyume cha usemi wa kikasisi. “Nasema shoka limewekwa penye shina la mti! Basi kila mti usiozaa matunda mema utakatwa na kutupwa motoni! Loo! mimi hakika nitawabatizeni kwa maji, kwa ajili ya toba, lakini Yeye yuaja nyuma yangu. Mwezi utageuzwa kuwa damu! Na, loo, jamani! Yeye atazisafisha sana nyanda Zake! Na atayachukua ma—makapi na kuyateketeza kwa moto usiozimika, na kuikusanya ngano ghalani. Atatenganisha magugu na ngano.” Lo, jamani! Ni Ujumbe wa jinsi gani!

247 Wakasema, “Ati jamaa huyu? Aa! Yeye anataka kusema nini, u—u—ulikuwa ni wakati gani? Loo, ujinga! Tuna mtu kule anayestahili, Ndugu Jones. Ndiye mtu atakayetenda jambo hilo, kama kuna mtu ye yote katika wakati huu. Askofu *Fulani* atatenda jambo hilo; Baba Mtakatifu *fulani*.” Loo, jamani! Mnaona?

Mungu katika urahisi, unaona, akitenda katika urahisi.

248 Ndipo, muda si muda unajua, huyo hapo amesimama siku moja, naye akasema, “Naam, Yeye amesimama kati yenu!” Alikuwa na hakika mno kwamba yeye alikuwa ndiye yule mtangulizi. Alijua yeye alikuwa ni nani. Hiyo ndiyo sababu yeye aliweza kuwatikisa kwelikweli. Kasema, “Sasa, msitetemeke,

lakini endeleeni tu na kuendelea. Ninyi askari, tiini wakuu wenu, na ikiwa mmetenda uovu wo wote, chukueni ile ninii . . . ”

249 “Tufanyeje? Tuache kutenda *hivi*? Tuache kutenda *hivi*?”

250 Akasema, “Endeleeni tu jinsi mlivyo. Endeleeni tu. Endeleeni tu. Songeni mbele. Kama mnalima viazi, limeni. Mnaona? Ninyi askari, msiwe wakatili. Na—nanyi fanyeni jambo hili. Na lo lote mtendalo, endeleeni tu jinsi mlivyo. Watiini wakuu wenu na mengineyo.”

“Rabi, tufanye nini?”

251 “Endeleeni tu jinsi mlivyo, unaona. Lakini kuna Mmoja miongoni mwenu, msiyemjua.” Yeye alijua hiyoo, saa ya Ujumbe wake. Alijua yeye alikuwa amtambulishe Mtu huyo. Alijua alikuwa yupo. “Mmoja kati yenu! Hammwoni. Mambo yanaendelea, ambayo hamjui lo lote kuyahusu hayo.” Na hivyo, basi, “Kuna—kuna kitu fulani kitakachotendeka,” yeye anasema, “mnaona, Naye atawasili. Nami nitamjua.”

252 Na hatimaye, siku moja, yeye akasema, “Tazama, huyo hapo! Huyo hapo ndiye Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!” Kasema, “Na wakati wangu umekwisha sasa. Nimewatambulisheni Kwake. Lazima nipungue sasa. Sina budi kuondoka jukwaani. Yeye ataendelea kuanzia hapa.”

“Ule Utawala wa Miaka Elfu utaanza, mara moja, mnaona, na wa—wakati umekaribia.” Ndipo wakati atakapokuja, wakati . . .

253 Hata Yohana alisema, “Yeye atafanya hivyo, loo! Yeye atawachuna ngozi. Ata—atatenganisha ngano na—na makapi, na atayachoma. Atazisafisha sana nyanda Zake, na pepeto Lake liko mkononi Mwake!” Lakini Yeye alikuwa nani? Maskini ninii mdogo sana . . .

254 Sasa, walikuwa wameyaorodhesha yote, “Loo, jamani! Yeye atakuwa na mkuki wenye urefu wa maili moja. Atasimama hapa nyuma katika Palestina, asimame tu kule juu na kuninii tu . . . kwenye moja ya mawingu haya meupe, na kuwachukua hawa Warumi wote, *hivi*, na kuwatupa kuzimu. Aendelee tu kufanya jinsi *hiyo*, unaona, mpaka amewapata wote.” Mbona, walikuwa wameyapanga hayo yote.

Na ilipotimia, Mwana-Kondoo mdogo akaja akitembea kati yao, mpole na mnyenyekevu, akisukumwa *hapa* na *pale*.

255 Ni kama tu alivyosema Yohana. Sasa, mtazame Yohana, yule nabii; yeye alisema, “Nendeni kamwulizeni. Je! Yeye kweli Ndiye hasa?” Mnyenyekevu sana, mpaka huyo nabii akalikosa. Kasema, “Je, Yeye ndiye Yule, au tumtazamie mwingine?”

256 Sasa, yeye hakumpa kitabu kwa ajili ya hao wanafunzi, katika—katika Mathayo 11. Walikuja wakamwuliza, wakati wale wanafunzi wa Yohana . . .

Yohana alikuwa gerezani. Kwa hiyo yeye alikuwa amehangaika sana hata yeye...Naamini Pember ndiye aliyesema, "Macho yake ya tai yalitiwa utando, kule alikokuwa," unaona. Yeye angeweza kuninii...A—alikuwa tayari ameshuka chini duniani; alikuwa huko juu hewani. Lakini unabii wake ulipokwisha, alishuka chini duniani tena, unaona, maana, walimfunga gerezani, unaona. Yeye hakuhitaji hayo mabawa makubwa tena, kwa hiyo alilala tu hapo chini. Lakini aliruka juu zaidi kuliko hao wengine wote.

257 Hebu niwaonyesheni jambo fulani. Mungu alimtumia. Na Yesu alijua, mnaona, kwa sababu huyo alikuwa ninii—huyo alikuwa ni Mungu aliyefanyika mwili akiwa hapo. Mnaona? Yeye alikuwa . . . Kwa hiyo, Yeye—Yeye alisema pale, Yeye alisema . . .

Sasa, Yeye hakumpa hata kidogo kitabu cha jinsi ya kujiadibisha gerezani; aseme, "Sasa ngojeni kidogo. Nitaandika kitini kidogo hapa, nanyi mumpelekee Yohana na kumwambia jinsi ya kuenenda katika tabia nzuri akiwa gerezani, kwa ajili Yangu." Unaona? La, Yeye hakusema hivyo hata.

258 Yeye hakusema, "Enendeni mkamwambie Yohana kuwa angepaswa kupata shahada yake ya Ph.D. kabla hajajitokeza." Unaona? Kama angaliipata, angalikuwa pamoja na hao wengine; angalikuwa mkataaji.

Yohana alikuwa mwaminifu na akauliza swali hilo.

259 Naye akasema, "Hebu ngojeni mpaka mkutano utakapokwisha, na ndipo mwende mkamwonyeshe Yohana yale yaliyotendeka, ndipo yeye atajua. Mkimwambia yale yanayotendeka, basi yeye atajua." Unaona? Unaona? "Nendeni tu mmwache...Mwambieni. Mwambieni ni...Yeye yuko gerezani na wala hangeweza kuwa hapa. Lakini—lakini ninyi mliketi mkutanoni, na mmeona yale yaliyotendeka. Nendeni mkamwambie."

Kwa hiyo, basi, hao wanafunzi wakasema, "Vema kabisa, Bwana."

260 Basi wakakwea kilima wakaenda zao. Yesu akiketi juu ya mwamba huu, akawaangalia mpaka wakavuka na wakakivuka kile kilima.

261 Akawageukia kusanyiko, akasema, "Mlitoka kwenda kumtazama na—nani, katika wakati wa Yohana?" Mnaona? Kasema, "Lakini mlitoka kwenda kuona nini? Je! mlikwenda kumwona mtu mwenye ukosi wake uliokunjwa, na mavazi mororo, na aliyeerevuka sana na mwenye elimu. Je! mlienda kumwona mtu wa aina hiyo?" Kasema, La. Je! mnajua watu wa namna hiyo walivyo? Wao hubusu watoto wachanga, na, mwajua, hufanya kazi katika majumba ya kifalme. Hao, Yohana ha—hakuwa mtu wa aina hiyo."

262 "Vema," akasema, "basi, kwa nini mlitoka mkaenda? Kumwona mtu ambaye amepewa huduma na ataifungamanisha na madhehebu, ama kitu kama hicho? Anayetikiswa na kila . . . Basi, kama ninii—kama wa Umoja hawamtaki, atakwenda kwa wa Utatu? Na ikiwa wa Utatu hawamtaki, yeye atakwenda kwa kanisa la Mungu, po pote pale? Je! mlikwenda kumwona mtu wa aina hiyo, anayetikiswa na unyasi wo wote? Loo! la. Si Yohana.

263 Yeye alisema, "Basi mlikwenda kuona nani? Nabii?" Akasema, "Nami nasema hiyo ni kweli. Lakini nitawaambia jambo fulani msilolijua; yeye alikuwa ni zaidi ya nabii. Alikuwa zaidi. Ikiwa mnaweza kukubali hilo, huyu ndiye Yeye aliyeandikiwa, katika Biblia, mnaona, huko nyuma, kwenye Maandiko, 'Mimi nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu,' Malaki 3, unaona, 'naye ataitengeneza njia mbele Yangu.'" Unaona?

264 Nao hawakuelewa. Hata wale wanafunzi hawakulipata, unaona. Hiyo ni kweli. Loo, jamani! Urahisi! Iweni wanyenyekevu, mnaona. Tafuteni kote . . . Mungu anapoahidi jambo fulani kubwa, mnaona, ni kubwa machoni Pake.

265 Basi mkitaka kuliweka hili moyoni daima, nawatakeni mu . . . Wekeni hili moyoni. Na jambo hili litakapotendeka, basi mwaweza kulibadili. Hebu inama chini uchume moja ya haya maua ya majira ya kuchanua majani yanayoota mwaka huu ujao, au ukachume jani lo lote la kawaida la nyasi ulishike mkononi mwako, na useme, "Nitalishika hili sasa, na nione kitu fulani hicho, rahisi sana, kilicholifanya *hili*. Kisha nataka kuona huo ubongo, unaoweza kutuma roketi mwezini, ukitengeneza jani hili la nyasi." Utalikumbuka jambo hilo daima. Unaweza kuwa na uhakika wa jambo hilo. Utalikumbuka nalo daima. Unaona? Huo unyasi una uhai ndani yake, unaona. Ni kitu rahisi sana na ni kinyenyekevu.

266 Mnaona, mtu akiwa ni mtu mkubwa, vema, lakini yeye akiwa ni mkubwa vya kutosha hata anaweza kuwa mnyenyekevu, unaona. Yeye atampata Mungu. Lakini asipojinyenyekeza, yeye hatamwona kamwe. Kwa hiyo huna budi kuwa mnyofu. Sasa kifungu . . .

195. Katika Ufunuo, aya ya 5:9, ni nani hawa wanaoonekana waki—wakiimba wakati Mwana-Kondoo anapokitwaa kile Kitabu toka katika—kutoka katika . . . anayekitwaa kile Kitabu? Je! hawa—hawa ni wale watakatifu walionyakuliwa?

267 La. Ufunuo 6 . . . 5:9, hasa. La. Kama ukiangalia, hawa si watakatifu. Wao walikuwa . . . Yeye hajadai mali Yake bado. Unaona? Hawa si watakatifu. Kama ukiangalia, hao ni wale wazee na wale Wenye Uhai, nao wanaimba.

268 Hebu na tupasome, ili mtu huyo . . . Na ndipo nitajaribu . . . Ninayo kama nusu dazani hapa zaidi, nami nadhani ninaweza

kuyafikia mnamo dakika chache. Hebu na tuone. Ufunuo 5:9. Sasa, hebu na tusome kidogo tu hapo juu. Ili, mtu huyu, sasa, ni mwaminifu kuhusu hili, nao wanataka kujua. Tazama!

> *Hata alipokitwaa kile—kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana-Kondoo, kila mmoja wao ana kinubi,. . .vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu.*
>
> *Nao waliimba wimbo mpya* (unaona, unaona,) *wakisema, Wastahili Wewe kukitwaa hicho kitabu na kukifungua* (unaona,). . .*umetukomboa*. . .
>
> *Na*. . .*kutufanya* makuhani na wafalme. . .

269 Hilo ni lile kundi la Mbinguni, lisilokombolewa bado. Vema, sasa.

> **Ndugu Branham, iwapo wale wote. . .**

Sasa hebu kidogo tu. [Ndgu Branham anatulia—Mh.] Nadhani, kile. . .Samahani.

> **Ndugu Branham, iwapo—iwapo watu wote wanaomcha Mungu,** (naam), **wanaomcha Mungu watanyakuliwa, je! Eliya na ninii. . .na Musa watatoka wapi?**

270 Kuna kasoro fulani. Kuna kasoro fulani. Ni hayo tu. Kuna—kuna jambo fulani limetukia. Mnaona? Kuna kitu fulani kisicho sawa mahali fulani. Kila mtu anajisikia yuko vema? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakuna. . .Hakuna ugonjwa, wala cho chote kile?

[Ndugu fulani katika kusanyiko anasema, "Soma hiyo aya ya 9 tena, katika Ufunuo 5."] Hebu tuone, Ufunuo. . .Ilikuwa wapi, ndugu? ["5."] 5. ["5."]

Masalale! lile swali! Loo, masalale! lile swali nililojibu sasa hivi. Sasa hebu na tuone. "Wewe. . ." Mahali sahihi.

> *Hata alipokifu-. . .kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana-Kondoo, kila mmoja wao ana kinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu.*
>
> *Nao* waliimba *wimbo mpya wakisema, Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa* ume-. . . *ulichinjwa*,. . .na. . .

Hili hapa! Hili hapa! Nilikosea hapo. Unaona?

> . . .*ukamnunulia Mungu kwa damu yako*. . .*wa kila kabila na lugha na*. . .

271 Hiyo ni kweli. Sasa, mnawaziaje kuhusu hilo? Loo! kama Uwepo wa Roho Mtakatifu hauko hapa, ni kitu gani? Yeye hangeruhusu. . .Unaona, nilisoma tu sehemu ya kwanza ya kifungu hicho. Unaona, ni—ni ninii tu. . .ama kitu fulani

kilichoandikwa hapa, nami nilikuwa nikijaribu kulimaliza upesi, nikitazama hiyo saa ya ukutani. Lakini mliona Yeye akinisimamisha kwenye jambo hilo? Utukufu! Unaona, sikusoma ile sehemu nyingine yake. Unaona, nilifika hapa, "Na. . . " Angalieni hapa. "Nao—nao waimba wimbo mpya," ndipo nikasimama, unaona. Lakini, angalia hapa, "Ule wimbo walioimba, wakisema, 'Umetununua kutoka katika kila jamaa na lugha na taifa.'" Hakika, ndio hao. Jamani! Loo, kumbe! Mnaliona? Na, jambo lingine, kuna swali lingine hapa chini, pia.

196. Je! waweza (k-u-t-o-f-a-u. . .) **kutofautisha wale waliopewa. . .Vema, kutofautisha "wale waliopewa nguo ndefu nyeupe," wa Ufunuo 6:11, na "wale waliofua mavazi yao katika Damu ya Mwana-Kondoo?"**

272 Sasa hebu na tuone, Ufunuo 6. Siwezi tu kuharakisha kwenye hili, jamani, namna hii hapa, unaona, kwa sababu itakuwa. . .Nitajibu vibaya. Sasa, Yeye hakutaka—hakutaka nifanye hivyo. Hiyo ni kweli, kwa hiyo na anisaidie. Roho Mtakatifu wa Mungu anajua hilo ni kweli. Unaona? Nilininii tu. . .Kuna kitu fulani tu. . .Mimi—mimi ndiyo kwanza nikiangalie. . .nilikuwa nikitazama ile saa ya ukutani, saa tano na nusu, ndipo nikafikiri, "Nisipoharakisha sasa, sitawaombea wagonjwa." Nami ninajaribu kufikia hapo. Kwa sababu nina-. . .Na akili zangu ni ninii sana. . .siwezi. . .

273 Mnakumbuka, itawabidi tu kuelewa sasa, mimi—mimi ni mwanadamu, unaona. Na ni—nimekuwa humo ndani kwa siku saba, na ninii yangu. . .Nami nina jambo fulani bado, alasiri ya leo, ambalo sina budi kulipata kutoka kwa Mungu.

274 Lakini, Yeye ameshikilia sana ya kwamba sitafanya kosa hilo, wakaniambia nisome tena aya hiyo iliyosalia. Nilikuwa tu. . .Nilijisikia tu kama Kitu fulani kilivingirika juu yangu pale, na kusema, "Rudia, rudia!"

Nikawazia, "Nirudie? Kitu gani? Nikome sasa hivi kisha nianze kuwaombea wagonjwa? Lakini ni—ni nini? Nimefanya nini?"

Na mara nilipoanza kufikia jambo hilo, mtu fulani akasema, "Soma kifungu kile tena." Nami nikakisoma tena. Na hapo, chini ya hili swali, ndilo hilo hapo, unaona, "Ufunuo 6."

275 Unaona, nilisoma cha kwanza. Hicho kinasikika kama ndicho, cha kwanza, unaona, "Nao waimba wimbo mpya."

Lakini hapa chini, unaona ilikuwa ni nini? Hiyo inayofuatia, tukitelemka, "Ametukomboa." Hakika, ilikuwa ni Bibi-arusi, wale watakatifu walionyakuliwa. "Waweza. . . " Na hapa, kweli, Mwa—Mwana-Kondoo alikuwa na kile Kitabu mkononi Mwake. Yeye tayari alikuwa amekiacha kile Kiti cha Enzi cha neema ya upatanisho. Unaona? Je! unaona jinsi Roho Mtakatifu anavyolitunza hilo? Kwa sababu, kweli kabisa, hilo ndio jambo lile lile nililolisema usiku uliopita.

276 Yeye alipokuwa amezungumza nami kule chumbani, nami nikashuka nikaja hapa na kuwahubiria ninyi nyote, ya kwamba, "Wakati Mwana-Kondoo alipoondoka mahali pale." Loo, jamani! Sasa naamini tutachukua tu somo. Mnaona, "Mwana-Kondoo alikuwa ameacha kiti Chake na akaja," unaona, kama nilivyoenda juu pale alipokuwapo, ile Nuru, ambayo ni Kristo; alipokuwapo, nikasema jambo hilo. Wakati Mwana-Kondoo atakapoondoka kwenye Kiti cha Enzi, akiwa Mpatanishi, anakuja huku, na Siku ya Ukombozi kwa kanisa imekwisha.

277 Ukombozi mwingine unafunguliwa, kwa ajili ya Wayahudi, wale mia na arobaini na nne elfu. Sivyo? Kwa sababu Yeye aliahidi angeukata huo mti, unanajua.

278 Sasa, hapa, sasa hapa Yeye anatoka, yule Mwana-Kondoo, na basi Siku ya Ukombozi imekwisha. Na wale wote watakaookombolewa, tayari wamekombolewa na kuandikwa kwenye kile Kitabu, naye yuko nje hapa akikifungua kile Kitabu. Hiyo ni kweli!

279 Loo! asante, Bwana. Unaona? Msamehe mtumishi Wako mwenye wasiwasi kwa kujaribu kuharakisha jambo fulani.

Sasa, ungeweza kuwatenganisha "wale waliopewa nguo ndefu nyeupe," wa Ufunuo 6:11 . . .

280 Sasa hebu na tuone, 6:11. Vema. Sasa tuko wapi kwenye jambo hili sasa? "Mavazi meupe," naam, hao ni wale—wale waliosulubishwa, chini ya madhabahu. Wale—wale Wayahudi, kati ya wakati huo, "Wao walipewa mavazi meupe."

. . . na "wale waliofua mavazi yao katika Damu ya Mwana-Kondoo," wa Ufunuo 7:14?

281 La. Sasa, hilo ni tofauti, bila shaka kabisa. Kwa sababu, unaona, hapa, tunaona *hapa*, ya kwamba "hawa walipewa mavazi meupe," upande huu katika wakati huu. "Walipewa nguo ndefu nyeupe," wao wenyewe, kwa neema. Na hawa *hapa*, "Walikuwa wamefua mavazi yao katika Damu ya Mwana-Kondoo," na katika Ufunuo hapa, hawa ni wale "makutano mengi waliokuja mbele za Mungu, wa jamaa zote, lugha, na mataifa." Na *hawa* wanalinganishwa hasa na wale wafia imani, wale Wayahudi, unaona. Sasa, sasa hiyo ni kweli, sasa.

197. Ndugu Branham, iwapo wale wote wanaomcha Mungu watanyakuliwa katika ule Unyakuo, je! Eliya na Musa watatoka wapi? Je! wao watakuwa ni Wayahudi, au je! Eliya wetu, tuliyepewa, a—atakuwa pamoja nao?

282 La. Yule—yule Mmataifa atakayetiwa upako kwa roho huyu, kuwaita Mataifa, ataondolewa. Kwa maana, unaona, Kanisa zima, lote, limetwaliwa juu. Na hawa manabii wawili, wa—wa sura ya 11, wanatelemshwa. Basi siku ya neema inakwisha kwa Mmataifa, na kupelekewa Wayahudi. La, hatakuwa ni mtu

yule yule. Sasa, nina—nina hakika sana na jambo hilo. Sasa kumbuka, haya ni kadiri nijuavyo mimi kwa uwezo wangu wote.

Hebu tuone hili lina kitu gani, linachosema hapa. Swali, "Je! ngano na divai . . ." Loo! "Je! . . ." N-g-a-n-o. La, nadhania li—lilimaanisha, "Je! . . ." Halina "nini" pale. Linasema tu:

198. Divai na ninii, ama ngano na divai, ninii ina-. . . . ya Ufunuo 6:6?

Hebu tuone ni kitu gani, ninapofikia hapa chini sasa, hili hapa.

> *Nikasikia kama sauti katikati ya hao wenye uhai wanne, ikisema, Kibaba cha ngano kwa nusu rupia,* na kibaba cha *shayiri kwa nusu rupia, wala usiyadhuru mafuta wala divai.*

283 Nadhani hiyo inamaanisha hivyo "ngano na divai." Hiyo ilikuwa ni moja, kwa ile nyingine.

Hasa, ni mfano, ile divai inayonywewa kwenye meza ya ushirika, ya Ufu- . . . ya Wakorintho wa Kwanza 11:24?

284 "Je! divai—divai . . ." La. Moja ya hizo ni mfano wa kiroho, unaona. Na hiyo nyingine hasa ni u—ufunuo wa Neno.

199. Inawezekana kwamba sababu ya watu wengi kuwa hawawezi, ni kwamba hatukupambanua ule Mwili wa Bwana? (Sawa!)

. . . lakini sasa jambo hilo limefunuliwa kwa kufunguliwa kwa Muhuri wa Sita?

285 Sasa, hebu tuone. Hebu tu nione kama naweza kuipata hilo sasa. Si wewe; ni mimi. Hukuninii . . . Ulilliandika vizuri; ni mimi tu.

Inawezekana kwamba sababu ya watu wengi kuwa hawawezi, ni kwamba hatuupambanui Mwili wa Kristo? (Hilo lina alama ya kuuliza, mwishoni mwake.)

286 Vema, Maandiko yanasema, ya kwamba, "Wengi hawawezi na ni wadhaifu kati yenu, kwa sababu ya kule kutoupambanua Mwili wa Bwana." Hiyo ni kweli kabisa. Kwa sababu, unaona, Mwili wa Bwana ni Bibi-arusi. Na wengi wao hukosea, hawachukuani Nao. Hiyo ni kweli. Mnaona, hawajui jinsi ya kuenenda ipasavyo. Wanaishi maisha ya aina yo yote; na wanapokea ushirika na kadhalika. Hilo si sawa. Unaona? Watu wanapopokea ushirika, ambao hudanganya na kuiba na kunywa pombe, na, hilo—hilo—hilo ni jambo baya sana. Hampaswi kutenda jambo hilo. Mnaona?

. . . lakini sasa jambo hilo limefunuliwa kwa kufunguliwa kwa Muhuri wa Sita?

287 "Kule kufunguliwa kwa Muhuri wa Sita." Hebu tuone sasa. La. Sasa, utaona, ule Muhuri wa Sita ulipofunguliwa hapa, ulikuwa ni kwa Wayahudi. Unaona, Ka—Kanisa tayari

limeondoka. Huu ni wakati wa ile Dhiki. Kwa hivyo haingekuwa ni kitu kile kile. La. La. Sivyo.

288 Kimojawapo cha hivyo ni divai ya kiroho, huo ni ufunuo wa Neno, kwa hiyo mwa—mwamini huchangamshwa na ufunuo wa Neno. Na kingine ni mfano wa Damu ya Yesu, inayotumiwa kwenye meza ya Bwana. Sasa, sana sana hivyo ndivyo kadiri ninavyofahamu jambo hilo.

200. Je! mtu ye yote asiyekusudiwa tangu zamani atampokea Bwana? Kama watampokea, wataanguka?

Sivyo, kama wamechaguliwa tangu awali. La. unaona, hawangeweza kuanguka.

201. Liko wapi Andiko linaloonyesha ya kwamba nanii... ya kwamba Ukatoliki utawadanganya Wayahudi na kuchukua mali yao?

289 Sasa, "Ni wapi hasa inaposema ya kwamba—ya kwamba—ya kwamba yule mnyama atadanganya kwa ajili ya kupata utajiri?" Haisemi hivyo. Lakini tunadhania kuwa hiyo ilikuwa...Sasa, juzijuzi usiku, mnakumbuka. Chunguzeni hiyo kanda kwa makini sana. Sikusema kamwe ndilo wangetenda. Nilisema... Unaona, Wakatoliki ndio kundi tajiri kuliko yote ulimwenguni. Hakuna mtu aliye kama wao. Na kile hawana, Wayahudi wana yote yalivyosalia.

290 Hapo ndipo ulipo uchumi wa nchi hii sasa...Hivi sasa tunaishi kwa pesa za kodi, kulingana na *Lifeline*, ambazo zimetolewa kwenye kodi (inayotoka moja kwa moja kutoka Washington, D.C.) itakayolipwa miaka arobaini kuanzia leo. Hizo ndizo tunazotumia sasa. Hivyo ndivyo tulivyo nyuma, kutoa noti, unaona, kwa kodi zitakazolipwa miaka arobaini kuanzia sasa. Taifa hili limefilisika. Limekwisha.

291 Sasa, Castro, jambo pekee la busara alilowahi kufanya, ilikuwa ni wakati alipoziondoa sarafu za uongo na kulipia noti zote, na hati za mikopo, na kuzichoma moto, kisha—kisha akabadili sarafu. Hilo ndilo jambo pekee angaliweza kufanya.

Na kuna jambo moja pekee lililosalia kwa hii nchi ya Marekani kufanya. Sasa kumbuka, huyu ni William Branham, unaona, anenaye. Hili ni wazo langu. Ni kudhania tu, kuliangalia tu katika msimamo wa kawaida, ambapo huenda likawa limeenda mbali kwa maili milioni moja. Ninaamini ya kwamba papo hapo, katika ninii hilo la... "Shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha." Nami naamini ya kwamba mahali fulani katika jambo hilo hapo ndipo mambo yatakapoanza.

292 Sasa, kanisa Katoliki nyuma huko, kutokana na kutoza pesa kwa ajili ya misa, na mengineyo, linashikilia utajiri wa ulimwengu. Mnakumbuka, Biblia ilisema, "Alikuwa tajiri," na jinsi alivyokuwa. Na kumbuka, sio tu kutoka katika taifa moja. Ni tajiri katika kila taifa lililoko chini ya Mbingu. Limeenea kila

mahali. Lina pesa. Sasa, kile wasicho nacho, Wall Street inacho, ambayo inamilikiwa na Wayahudi.

293 Sasa, nanyi mnakumbuka, Yakobo alikuwa na pesa wakati aliporudi (tuliona jana usiku) na akawa Israeli. Kweli alikuwa na pesa. Lakini pesa zake hazingemnunulia cho chote, unaona, kwa Esau. Esau alikuwa nazo, pia. Unaona, wote wanapingana, na—na yule . . . Unaona, linalingana barabara kabisa.

294 Sasa angalia hapa. Nilisema labda watataka kuungana pamoja kwa ajili ya pesa, na ninii—na mamlaka ya Kirumi itwae mamlaka ya Kiyahudi, na ya fedha, wakivunja lile agano. Hilo laweza lisiwe hivyo. Unaona, najua watalivunja, lakini si—sijui sababu yake, kwa sababu jambo watakalofanya halijafunuliwa kwangu.

295 Lakini angalia. Sasa, kama leo, sasa vipi kama leo, jambo pekee tunaloweza kufanya, tungefanya nini? Kama tunatumia kodi (ikiwa tamshi hilo la kweli) kutoka kwenye sarafu, kutoka kwenye fedha za kodi za miaka arobaini kuanzia sasa, unaona, dhahabu yetu ni . . . Tumeitumia tayari. Tumefilisika. Hatuna pesa zo zote. Nasi tunaishi tu kwa sifa za siku zilizopita.

296 Hayo ndiyo linayofanya kanisa leo, kanisa; si Bibi-arusi. Kanisa linaishi kwa sifa zake zilizopita lilizopata huko nyuma chini ya huduma ya wakati wa simba. "Sisi ndio Kanisa halisi! Sisi ndio Kanisa mama! Tulianzia . . . " Hiyo ni kweli. Unaona? Linaishi kwa sifa za siku zilizopita!

297 Wemethodisti wanaishi kwa sifa za siku zilizopita. Wabatisti wanaishi kwa sifa za siku zilizopita. Na Wapentekoste wanaishi kwa zao. "Utukufu kwa Mungu! Zamani za kale, wakati watakatifu walipokuwa wakicheza katika Roho, na jinsi wao . . . Bwana alifanya *hivi* na *vile*." Hilo, hilo ni jambo lililopita. "Sote tumekuwa wakubwa sasa, ndugu." Loo, jamani! Unaona? Yote kwa sifa zilizopita!

298 Taifa hili linaishi—linaishi kwa sifa zilizopita za vile babu zao walivyokuwa, unaona, na hiyo ndiyo sababu tunadhani tutaokolewa. Mungu hakuwaheshimu Israeli kamwe kwa yale waliyokuwa hapo zamani, kile walichoishi zamani; ni kile walichokuwa wakati huo! Angalia.

299 Lakini, sasa, haya ndiyo ninayofikiria, yale ni—ninayodhania yatatukia. Sasa, labda sivyo. Ninaamini wakati unakuja ambapo tutalazimishwa kutoa uamuzi juu ya ukweli wa mambo. Basi wakati itakapofanyika hivyo, ni kwamba, badala ya sisi kubadilisha sarafu . . . Hilo lingesababisha nini kwa Philip Morris? Hilo lingesababisha jambo gani kwa ma—makampuni ya wiski? Hilo lingefanya nini jambo gani kwa viwanda vya chumapua? Hilo lingesababisha nini kwa uchumi wote? Hilo lingeleta nini? Lingevifilisi. Vingefilisika. Lakini, kama, "Tunaweza kukopa pesa hizo." Unaona jinsi alivyo mwerevu?

300 Ndipo taifa litajiuza kwa kanisa. Halafu kanisa na taifa vitaungana tena, na ndilo hilo hapo linakuja. Unaona? Hivyo ndivyo ilivyo. Angalia. Vema. Sasa, katika hili:

202. Kama mtu yuko kwenye shirika la madhehebu kwa kupitia serikali yetu, na anaweza kutoa maoni ya moyo wake; ama yuko katika Ukweli wa siku ya mwisho, je! yeye atahesabiwa kama mmoja wa wale "makahaba"?

301 Hebu tuone. "Kama mtu akiwa yuko katika shirika la kimadhehebu . . . " Vema, unaona, shirika la kimadhehebu; ma—madhehebu, yamepewa haki na serikali, kunena. Unaona, hilo halina uhusiano wo wote na moyo wake. Unaona? Sasa, kama yeye ni mwamini halisi, na amezaliwa na Roho wa Mungu, siku moja yeye atachekiwa. Unaona? Haliwezi kuwa dhahiri sana naye asilione.

302 Sasa, nawatakeni . . . Unaona, inakupasa kukumbuka jambo hili, ewe rafiki, ya kwamba Mungu—Mungu kamwe hatendi kitu, au amewahi wakati wo wote, kadiri niwezavyo kukumbuka, unaona, ila kile . . .

303 Angalia, Yesu alikuwa—alikuwa ni moyo wa hayo yote, kwa sababu Yeye alikuwa Mungu, Imanueli, aliyefanyika mwili. Sasa, mtazame huyu—Mtu huyu, Yesu. Wakati . . . Je! ulijua, Yeye alipokuja duniani, hapakuwapo, nadhani, mmoja kati ya kumi ya watu wa walimwengu waliojua Yeye alikuwa hapa?

Je! mnajua wakati yule mtangulizi alipokuja, wakati "milima yote," na mengineyo yangetendeka, hapakuwapo na mmoja kati ya mia ya wenyeji wa Israeli, nadhani, waliopata kujua? Si ni ajabu hiyo?

304 Mbona, kulikuwako na Wayahudi na kadhalika, na watu ulimwenguni kote. Sasa, kumbukeni, Yesu alikuja kuwa shahidi, kama Mwokozi wa ulimwengu. Sivyo? Mbona, kulikuwako na watu tu, baada ya watu, baada ya watu, baada ya jamii, baada ya watu, ambao hata hawakujua cho chote kuhusu jambo hilo. Waliendelea tu moja kwa moja, kama kwamba tu ulimwengu haukujua cho chote kuhusu jambo hilo; lakini, wakati wote, jambo hilo lilikuwa likiendelea ulimwenguni. Unaona?

305 Mbona Yeye hakuwaruhusu wajue? Yeye alikuja, na wale waliochaguliwa kwa Uzima wa Milele tangu zamani ndio waliompokea. Haingefaa kitu kuwaambia cho chote hao wengine, kwa sababu Yeye hawangeweza kuwakomboa, kwa sababu hata hawangeweza kukomboleka. Ni kwa nini, wakati wale makuhani waliosimama pale? Wakati, ilimbidi Yeye kufikia mahali pale kwa sababu wale waliochaguliwa tangu awali walitawanyika mle, kila mahali, kwa hiyo ilimbidi kuwahubiria kama kundi.

306 Na wale wanavyuoni mashuhuri ambao walipaswa kumjua, walisema, "Mtu huyu ni Beelzebuli. Hatumtaki mtu huyu atutawale," na mengineyo, unaona. "Hatutakubali."

Lakini maskini kahaba mmoja mchafu, akiwa na Uzima ndani yake, aliyechaguliwa tangu awali apate Uzima wa Milele, na jina lake liko hai milele katika Neno la Mungu hapa. Alienda kule, na, mara ya kwanza tu ile Nuru ilipogusa hiyo punje ya mbegu, upesi yeye akalifahamu. [Ndugu Branham alidata kidole chake mara moja—M.]

307 Angalia, maskini huyo mzee mvuvi akapitia pale. Huyu hapa amesimama pale, akifanya ishara na maajabu, na—na kuwaambia watu mbalimbali siri za mioyo yao, na kujifunua Mwenyewe.

Na, jamani, kulikuwa na Mafarisayo wamesimaam pale, na kusema, "Mtu huyu ni Beelzebuli." Iliwabidi wawajibu kusanyiko lao.

308 Wote hao wamesimama hapo, "Dk. Jones, je! utashuka uende ukamsikilize Mtu huyu? I—inaonekana kama Yeye anajua yale anayonena. Yeye haneni kama wa mtu wa kawaida."

309 "Nitamsikiliza." Akashuka akaenda kule, unaona. Naam, Mungu—Mungu hangeweza kamwe kumfikia.

Naye huyo amesimama kule, na akasema . . .

Wao walisema, "Sasa angalia kule. Angalia kule. Kuna mtu anakuja kule. Yule pale mmoja wa wanafunzi Wake. Kuna mtu anakuja sasa. Sasa, jina la yule jamaa, yule ni Andrea. Mnakumbuka. Loo! mnamkumbuka yule mzee—wale wazee wavuvi hapa? Ndio hao. Ndiyo, yule pale—yule pale Simoni, ndugu yake. Unaona? Na hao—hao ni wana wa mzee Yona. Sasa hao hapo . . . Angalia, a—anampeleka mtu Kwake. Ni nani? Naam, angalia atakachotenda sasa. Yeye—yeye ndiye anayefuatia pale." Naye anasogea pale.

Ndipo Yeye akasema, "Jina lako ni Simoni, nawe u mwana wa Yona."

310 "Mtu huyu ni Beelzebuli! Unaona, yeye ana aina fulani ya roho juu Yake. Yeye ni Jamaa wa ajabuajabu. Unaona? Piteni moja kwa moja, msisikilize kitu kama hicho, unaona. Kaeni mbali na hapo. Mimi nisingehudhuria tena mikutano hii, hata kidogo, unaona. Mara tu kitu hiki kiishapo, tutatoka hapa. Hatutaondoka tena, kurudi hapa tena." Unaona? Kwa nini? Sasa, hivyo ndivyo alivyowazia, na hata hivyo alipaswa kuwa ndiye yeye. Angalia, watu wale wenyewe kabisa aliowajia ndio waliomsulubisha. Unaona?

311 Lakini palikuwapo na maskini kahaba mmoja ambaye kila mtu alikuwa amemfukuza! Siungi mkono ukahaba. La, kwa vyo vyote vile! Lakini ninawaonyesha tu hiyo Mbegu iliyochaguliwa tangu awali.

312 Mwangalie mtu huyu hapa, huyu mzee mvuvi, hata hangeweza . . . Biblia ilisema yeye hakuwa na elimu. Ni kweli? Isitoshe, lakini alikuwa asiye na maarifa. Sasa, hiyo ni kweli

au si kweli? Loo! laiti tungalikuwa wajinga kwa vitu hivi vingi tunavyowazia kuwa tunajua. Unaona? Vema. Unaona, alikuwa asiye na elimu wala maarifa. Na ndipo yeye akaenda pale mbele za Uwepo wa Bwana Yesu, naye akamwambia yeye alikuwa ni nani. Papo hapo mambo yakaisha.

313 Sasa, hoja ya mtu huyu mwingine kulipinga jambo hilo ni nini? "Vema, tazama, yeye aliliamini. Angalia yeye yu nani. Mnajua huyo ni nani. Vema, mtu huyo hakuwahi kamwe. . . Mbona—mbona, yeye ni mvuvi. Mbona, hazijui ABC zake. Nilinunua samaki kutoka kwake; hata hakuweza kuniandikia risiti. Hiyo, unaona, ni takataka za aina hiyo! Watu kama hao ndio wanaosikiliza kitu kama hicho." Bwana ashukuriwe. Amina. Unaona? "Mbona—mbona, yeye ha-. . .Mwangalie babaye; alikuwa asiye na maarifa. Hata hakuwapeleka shuleni." Lakini huyo ndiye Yeye aliyempeleka shuleni; akamfundisha njia aliyoitaka awe yeye afuate.

314 Sasa, siungi mkono kutokwenda shuleni, sasa. Natumaini mnafahamu. lakini huo hapo ni mfano tu, unaona, kile unachopata katika hilo. Ni watu wa namna hiyo, na sababu ya wao kupitwa na hayo.

315 Na hivi mna habari? Hakuna hata mmoja. . .Ningeninii, ningesema hakuna hata theluthi moja ya Wayahudi wote nchini waliojua cho chote kuhusu kuja Kwake. Na—na, basi, moja—moja tano ya theluthi moja walimsikiliza. Na, halafu, moja ya mia ya hao moja kwa tano walilipokea. Mnajua Yeye alikuwa na wangapi. Alikuwa na kumi na wawili waliosimama pale msalabani, kati ya kundi hilo lote. Hao wengine wako wapi? Unaona? Wale sabini waliondoka.

316 Sasa, Yeye alipokuwa akiponya wagonjwa, na kuendelea tu, bila kusema cho chote kuhusu Mafundisho Yake; Yeye aliendelea tu, kuponya wagonjwa na kila kitu. Loo, jamani! Huyo, huyo alikuwa ni Roho wa Mungu juu Yake. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Alipokuwa akiwaponya wagonjwa, "Huyo ni Rabi mzuri sana. Aisee, ninyi ndugu wote, nyota mnapaswa kumwalika kanisani mwenu. Jamani, mwanena kuhusu uweza, jamaa huyo anaweza kuponya wagonjwa kwelikweli! Inawapasa kuona. Yeye ana kipawa cha uponyaji."

317 Vema, bila shaka, tutapata waigaji wa jambo hilo. Hawa hapa wanakuja, kwa sababu kila kundi halina budi kuwa na mtu wake lenyewe.

Huyu hapa anakuja. Halafu basi, muda si muda unajua, siku moja akaketi chini.

"Loo, hakika, Rabi, tutakufuata uendako.

318 "Vema, ketini. Twendeni." Vema, Yeye akawatuma wale sabini, na kadhalika.

Ndipo siku moja, baada ya mwujiza mkuu kutendeka, Yeye aliketi chini na kuanza kuwaambia Neno, unaona. "Mwanzoni mwa kupigwa kwa ile baragumu ya . . . " Vema. Yeye akaanza kuwaambia Neno, ile Kweli . . .

Wao wakasema, "A-haa, sasa, ngoja kidogo! En-he! Sijui juu ya jambo *Hili*." Ni kinyume cha mafundisho yao. Kasema, "Vema, najua tuliacha sinagogi na kila kitu namna hiyo, lakini labda tu—tulikosea, ndugu zanguni. Afadhali turudi, kwa sababu mtu huyo hunena kwa vitendawili. Ni Mtu aliye wa namna ya kipekee. Siwezi kuyaelewa wa kipekee. Siwezi kuyaelewa jambo *Hayo*." Unaona? Ilikuwa ni nini? Hiyo mbegu haikuwa imechaguliwa tangu awali.

319 Ndipo, muda si muda unajua, alikuwa na kundi dogo la wahudumu, na akazungumza na hao wahudumu. Wakasema, "A-ha! kumbe! Afadhali turudi, na sisi pia, na turudi na kuingia kwenye madhehebu, tuchukue makaratasi yetu tena, unaona. Maana, Jamaa huyu, mbona, ni nani anayeweza kumwelewa Mtu kama huyo? Yeye anasema *hivi* hapa na kusema *hivi* hapa upande huu. A-ha!

320 Hao wengine hawakulielewa namna hiyo. Yeye alikuwa akionyesha mafumbo kwa baadhi yao lakini si kwa wengine.

Kwa hiyo wakaondoka. Ndipo akageuka na kuwatazama wale thenashara wamesimama pale. Kasema, "Nanyi mnataka kwenda, pia?" Unaona?

321 Sasa tazama. Petro akasema, "Mwajua nini? Nilihudhuria mahali hapo pa siku nyingi wakati huo wote. Ningeenda wapi hata hivyo? Ningekwenda wapi? Ningeweza kwenda wa—wapi? Baada ya kufanya kazi hapa . . . Nami siwezi kurudia lile pipa la taka hizo tena, ambamo mna kila aina ya koga la ulimwengu. Unaona? Ni—ni . . . Ningekwenda wapi? Si—siwezi kufanya hivyo."

322 Yeye akasema, "Basi, vema, njoni, endeleeni." Sasa, haya basi. Unaona? Kwa nini ilikuwa hivyo, basi? Kumi na wawili kati ya kama milioni mbili na nusu. Na ni Mwokozi wa ulimwengu, kutoka katika mabilioni, hata hivyo ni mnyenyekevu, unaona. Udumu tu mnyenyekevu. Angalia.

Sasa, kukiwako na hao Mafarisayo wote; na maskini yule kahaba alikuja pale. Akasema, "Aisee, huna budi kuwa nabii! Sasa, tunajua ya kwamba yuaja Masihi, Naye ajapo atatenda hayo."

Akasema, "Mimi Ndiye."

323 Huyo mwanamke akasema, "Ni kweli kabisa," na huyoo akaenda. Ati ujaribu tu kumzuia? Hungeweza kufanya jambo hilo.

203. Ndugu Branham, salamu katika Jina la Bwana Yesu. Tafadhali elezea mtu huyo ni nani, katika Mathayo 22:11,

yule mtu ambaye hakuwa na vazi la arusi, hakuvaa vazi la arusi. Najua mtu huyu hangeweza—hangeweza kuingia Mbinguni pasipo kuvaa vazi la arusi. Huyu alikuwa ni mgeni, najua, si Bibi-arusi.

324 Naam, hiyo ni kweli. Yeye angekuwa ninii . . . Naam, alijipenyeza kisiri tu. Unaona? Sasa tazama. Sasa, mimi . . . Jambo hilo lingechukua mahubiri ya ibada nzima.

Sasa nina dakika kumi, kuwaombea wagonjwa na kumalizia jambo hili. Nami nimemaliza nusu ya hayo, nadhani. Angalia. Lakini nita—nitaharakisha, kweli, kweli kabisa, baada ya hili. Unaona?

325 Hivi ndivyo ilivyotendeka, kama unajua desturi za kimashariki. Unaona? Bwana arusi anapotoa mialiko ya arusi yake, yeye hualika tu watu kiasi fulani. Na kwa kila mwalikwa aliyealika, alikuwa na bawabu aliyesimama mlangoni, kumvika vazi. Iwe kama alikuwa maskini, au cho chote kile alichokuwa, ilimbidi . . . kama alikuwa tajiri ama maskini, cho chote kile alichokuwa, yeye, wote, ilibidi kuvaa vazi hili la arusi.

326 Waliposimama mlangoni, walimvika hili, lilifunika yale aliyokuwa ameyavaa. Yeye amealikwa, awe yeye ni milionea ama ni hohe hahe, kama ni mkulima, mchimba mitaro, au cho chote kile alicho, au kabaila, yu—yuko hapa amevikwa vazi hilo sasa. Kwa sababu, mtu huvikwa hilo vazi mlangoni, aingiapo mlangoni.

327 Sasa, chukua Injili ya Yohana Mtakatifu 10, naamini ndipo lilipo, Yeye alisema "Mimi ndimi mlango." Unaona? "Mimi ndimi mlango unaoingia . . . unaoingilia." Sasa huyo hapo amesimama mlangoni, na huyu hapa Mtu atakayemvika vazi, Roho Mtakatifu, kumpa yeye Vazi la Haki aingiapo.

328 Basi, mtu huyu alikuja kupitia kwenye madhehebu fulani, hapa nyuma dirishani, tundu fulani la kuingilia kisiri. Naye akafika mezani na kuketi. Basi Bwana-arusi alipokuja na kutazama huku na huku, yeye alikuwa ninii . . . yeye . . . *Hawa* walikuwa watu wa kipekee, hapo awali, sasa *yeye* ndiye mtu wa kipekee. Unaona? "Unafanya nini hapa namna hiyo, pasipo ubatizo wa Roho Mtakatifu na mambo haya yote? Uliingiaje humu ndani?" Vema, yeye aliingilia mahali pengine mbali na mlangoni. Na alikuja pasipo mwaliko maalum. Unaona? Yeye alipitia katika mfumo fulani wa kielimu, unaona, ama kitu kama hicho. Akaingia ndani.

329 Naye akawaambia, "Mfungeni, mikono na miguu; mwondoeni hapa, mkamtupe kwenye giza la nje, ambako kutakuwako na kilio, na kuomboleza, na kusaga meno." Unaona? Yeye aliingia katika wakati wa ile Dhiki. Unaona? Hakupitia mlangoni. Kwa hiyo, sawa. Swali.

204. Je! yule Eliya wa Malaki 4 atakuwa ni Eliya yule yule aliyetajwa katika Ufunuo 11:3? Na mashahidi wengine . . .

je! yule shahidi mwingine...Je! na wale mashahidi wengine wawili ni watu tofauti, tofauti?

330 Ndiyo. Eliya wa Malaki 4 hatakuwa Eliya wa Malaki 3. Tulieleza hayo, usiku uliopita. "Na je! yule shahidi mwingine ni tofauti, hao wawili?" Ndiyo, bwana, Musa na Eliya; kulingana na ufunuo wetu. Sasa, sitaki kuwakawisha hapa kwa muda mrefu sana.)

205. Wafalme wa Kwanza 19, Ndugu Branham, ninaamini kuwa hesabu ya wale ambao hawakusujudu ilikuwa ninii sa-. . .

331 Naam, hiyo ni kweli. Mia saba badala ya...Asante. Hiyo ni sahihi. Ilikuwa mia saba badala ya elfu saba..."Ndugu Branham. . . " Elfu saba badala ya mia saba. Sasa, unaona hilo?

332 Mnajua, kwa kweli, mtu anapokuja namna hii, ku—kuhubiri...Nataka kuwaulizeni jambo fulani, sasa, mpate kuelewa.

Eliya alipotoka jangwani, yeye alikuwa na Ujumbe mmoja. Alitoka moja kwa moja kule jangwani hilo, na akaja moja kwa moja na kumwambia mfalme yule, "Umande hata hautaanguka toka Mbinguni hadi niuagize." Hayo ndiyo maneno aliyokuwa nayo. Kisha akatoka akarudi, wala hakusema cho chote kwa ye yote. Unaona?

333 Alipokuwa na Ujumbe mwingine, alishuka moja kwa moja na kutoa Ujumbe huu. Kisha akageuka moja kwa moja, akarudi jangwani. Unaona?

334 Sasa, ukichunguza, nilipoweka jiwe lile la pembeni chini ya hiyo Maskani, Yeye alisema, "Fanya kazi ya mhubiri wa Injili." Na sasa saa yaja ambapo hiyo kazi itajigawa. Kuna jambo lingine linalotendeka. Ndipo mimi niko ninii sana. . . Unaona, ninatoka hapa na kujaribu kufanya kazi ya kuhubiri Injili na jambo fulani lingine, basi unaona mahali ulipo? Unaona? Unaninii...Loo! ni—ninatarajia kanisa liwe la kiroho vya kutosha kufahamu.

206. Ndugu Branham, nafahamu kwamba Eliya hana budi kuwapo mara tatu. Unatwambia ya kwamba amekuwapo mara mbili tayari, na atarudi tena. Sasa, je! mtu huyo, ambaye roho ya Elia itakuwa juu yake, atakuwa pia mmoja wa wale mashahidi wawili wa Musa na Eliya kule.

335 La. La. Yeye atakuwa Mmataifa, unaona, kwa Kanisa la Mataifa. Mungu hutuma, daima, kwa watu wake mwenyewe, unaona. "Alikuja kwa walio Wake; walio Wake hawakumpokea." Yeye daima hutuma Wake, Ujumbe wa wakati huo.

336 Mungu alipokuwa akishughulika na Wayahudi, hapakuinuka manabii wo wote wa Mataifa. Mungu anaposhughulika na Mataifa, hakuna manabii wa Kiyahudi. Mungu anapowarudia Wayahudi, hapatakuwapo na manabii wa Mataifa. Unaona? Unaona ninayomaanisha? Vema.

Baada ya Kunyakuliwa . . .

337 Sasa, kutakuwako na wakati wa kupokezana, bila shaka, Ujumbe mmoja ukipokezana na mwingine. Hauna budi kuja moja kwa moja namna *hii*, unaona, kama nilivyoeleza hilo, unaona; kama Paulo kwa Mataifa, na kadhalika. Vema.

207. Baada ya Kunyakuliwa, je! kuna ye yote wa kanisa atakayeokolewa mwishoni, ambaye hakuchukuliwa katika kule Kunyakuliwa?

338 La. En-hee. Maana, Damu imeisha ondoka. Unaona, hakutakuwako na upatanisho. Wakati wa Mataifa umekwisha. Hakuna mtu atakayeokolewa baada ya Kunyakuliwa, ama hakuna ye yote wa kanisa, en-hee, kanisa. "Mwenye uchafu, azidi kuwa mchafu; aliye mtakatifu, azidi kutakaswa." Unaona? Hilo halitatendeka, unaona, si baada ya Kanisa kuondoka.

208. Ndugu Branham, niliona, ukirejea kwenye yale majuma sabini ya Danieli katika ule Ujumbe wa ule Muhuri wa Kwanza. Nafahamu, katika Danieli, kwenye kanda ya Danieli, Injili itakapowarudia Wayahudi, yale majuma sabini yataanza. Je! kuna sabini moja . . . juma moja, miaka saba, lililosalia kwa Wayahudi? Ama, bado, kuna nusu moja tu ya juma, miaka mitatu na nusu iliyosalia kwa ajili yao?

339 Ni nusu moja tu ya juma. Yesu alitoa unabii, kwa nusu ya kwanza ya hilo juma, kama iivyotabiriwa. Ni nusu moja tu ya juma iliyosalia kwa ajili yao.

Ndugu Branham, kwa kuwa hukuwaombea wagonjwa juma hili, je, u- . . . (Hilo ni ombi tu la jambo hilo).

Ndugu Branham, waweza kuniona baada ya iba- . . .? (Hilo ni ombi, unaona, pale.)

209. Waweza kueleza kuhusu kufungwa kwa Shetani miaka elfu, na kufunguliwa kwake kwa ajili ya vita vya—vita vya Ufunuo 20:8? Haya yana uhusiano gani na vile vita vya Har-Magedoni kama ilivyotajwa katika Muhuri wa Nne? Je! Gogu na Magogu watakusanywa kutoka kwa watu wa nchi mpya?

340 Vema, hili ni refu, nami—nami itanibidi tu kugusia mambo muhimu yanayolihusu, unaona. Sasa, jambo la kwanza, "Je! . . ." Sasa, labda siwezi kulielezea. Nitafanya niwezavyo.

Waweza tafadhali kuelezea vile Shetani anavyofungwa miaka elfu, na kufunguliwa kwake tena kwa ajili ya vile vita vya Ufunuo 20:8?

341 Hivyo si vita vya Har-Magedoni. Vita vya Har-Magedoni vinazuka upande huu, unaona, vema, wakati ile Dhiki itakapokwisha.

Sasa, haya yana uhusiano gani na vile vita vya Gogu na Magogu?

342 Hayana uhusiano. Moja ni miaka hii elfu moja, na hivyo vingine ni mwisho wa—mwisho wa ile miaka elfu.

. . . kama ilivyotajwa katika Muhuri wa Nne? Je! Gogu na— Je! Gogu na Magogu watakusanywa kutoka kwa watu wa nchi mpya?

343 Shetani alifunguliwa toka gerezani mwake, na akaenda akawakusanya watu wote, walio waovu, awalete mahali hapa. Ndipo Mungu akanyesha moto na kiberiti kutoka mbinguni, nao wakateketezwa, unaona. Vita viwili, kwa jumla. Swali:

210. Kuhusu wale milioni sitini na nane waliouawa na kanisa la Romani Katoliki, haya yalitendeka katika wakati gani wa historia? Na jambo hili lilichukua muda gani?

344 Chukua kitabu cha Schmucher kiitwacho *Glorious Reformation*. Nadhani baadhi ya hawa wanavyuo wanacho. Na ni historia ya kanisa. Nami ninasahau sasa yamo kwenye ukurasa gani hasa, lakini yalitendeka tangu wakati wa—wa . . . jambo lile lilianzishwa au lilitolewa kwa kanisa, na Mtakatifu Agostino wa Hippo, Afrika. Huo ulikuwa mwaka wa 354 B.K. Na ulidumu hadi mwaka wa 1850, yale mauaji ya Ireland, unaona. Kwa hiyo wakati huo ni tangu 33 B.K. ama 30 B.K. . . . 354. Hebu nipate hilo vizuri, sasa, unaona. Tangu 3-5-4 B.K. hadi— hadi 1-8-5-0 B.K., 1850, kulingana na historia, kulikuwako na Waprotestanti milioni sitini na nane waliouawa kwenye orodha ya wafia imani ya Kirumi, kwa kutokubaliana na papa wa Rumi. Hiyo ni historia. Ukitaka kusema si sahihi, vema, basi, labda George Washington hakuwepo hapa, au Lincoln. Mnajua, hakuna mmoja wetu aliyeishi kule nyuma kuona jambo hilo. Lakini naamini walikuwa hapa, kwa vyo vyote. Ninaona dalili ya kwamba walikuwapo hapa.

211. Ndugu Branham, ile sura ya 19 ya . . . na aya ya 18, "Pamoja na hayo nimejisazia elfu saba, watu elfu saba katika Israeli, kila goti lisilomwinamia . . . lisiloinamia Mabaali, na kila kinywa . . . ama—ama kisichomwinamia Baali, na kila . . . kisichombusu, kinywa kisichombusu." Tafadhali nielezee haya, kuhusu—kuhusu wale mia saba.

345 Ilikuwa ni elfu saba. Unaona? Na huko, "kumbusu Baali," je! hamjui . . . Ni wangapi hapa ambao hapo awali walikuwa ni Wakatoliki? Hakika. Unaona? Mnabusu sanamu. Unaona?

346 Pia, kumbukeni, katika wakati wa Babeli na Nebukadreza, ufalme wa Mataifa ulipoanzishwa, unaona; wakati ufalme wa Mataifa ulipoanzishwa, ulianza kwa kumwabudu mwanadamu. Nebukadreza alitengeneza sanamu ya mwanadamu. Na kama una mawazo ya kiroho, sasa sikiliza ufunuo huu. Roho yule, mtu huyo ambaye alimfanyia ufunuo, ama ambaye alitengeneza sanamu yake, kwa ufunuo wake, alikuwa ni Danieli, mtu wa

kidini akiabudiwa. Unaona jambo hilo? Kwa sababu, alimpa jina la Beltesheza, sivyo? Ama Belteshaza, ambalo lilikuwa ni jina la mungu wake. Naye akafanya sanamu ya mungu huyo, ambayo ilikuwa ni sanamu ya Danieli. Naye Danieli akakataa kuabudu sanamu yake mwenyewe. Unaona? Unaona?

347 Na hapa limetokea tena, unaona. Sasa tazameni. Ufalme wa Mataifa ulianzishwa, katika siku za Babeli, na Mfalme Nebukadreza; mfalme Mmataifa, akiunganisha kanisa na taifa pamoja, kwa kuchukua sa-. . .takatifu ama samu ya mtu mtakatifu, na kuamuru iabudiwe. Ufalme wa Mataifa unaishia miguuni, kwa yale Maandiko ya mkono kwenye ukuta, kwa nguvu za siasa ambazo zimeunganisha kanisa na taifa pamoja; kuamrisa kubusu tena sanamu, mnaona, jambo lile lile, sanamu ya mtu mtakatifu. Hakika.

212. Ndugu Branham, huku Kunyakuliwa kutakapotukia— Kunyakuliwa kutakapotukia, je! watoto wadogo wasiojua mema wala mabaya watanyakuliwa?

Kama majina yako katika kile Kitabu. Naam. Hiyo ni kweli. Unaona? Vema.

213. Ndugu Branham, ulisema usiku uliopita kuwa wale. . . kulikuwa na watu mia saba watakaookolewa, wangeokolewa kutokana na mahubiri ya Eliya. Ulikusudia elfu sa-. . .?

348 Naam. Hiyo ni kweli. Tafadhali nisameheni kwa jambo hilo, unaona. Hilo ni sawa, unaona, nilisema hivyo.

Ndugu Branham, tafadhali tafsiri. . . Ukishafungua. . . Ndugu Branham, je! je! kile—kile (k-i-p-i-. . .) **kipindi cha wakati. . .**

Samahani. "Je, kile kipi-. . ." Sasa, si wewe. Ni mimi, unaona.

214. Je! kile kipindi cha wakati wa neema kitakwisha baada ya wewe kufungua ule Muhuri wa Saba?

349 Natumaini sivyo. La. La. Marafiki, msiingize hilo mawazoni mwenu sasa, unaona. Endeleeni moja kwa moja. Limeni viazi, na mwende kanisani, na mwendelee tu. Kama jambo hilo likitendeka asubuhi, wewe ukutwe tu ukifanya yale hasa unayopaswa kuwa ukifanya. Msi—msianze. . .

350 Unaona, mkifanya hivyo, mnapotosha jambo hilo na ku—kusudi lililokusudiwa. Mnapata mawazo madogo ya ajabu ajabu, na unapata mawazo yako mwenyewe kuhusu mambo fulani. Usichukue wazo lako mwenyewe. Mara unapoketi na kusikiliza mambo kama hayo, sema, "Asante, Bwana. Nitatembea tu karibu zaidi na Wewe." Unaona? "Nitatembea. . ." Usiache kazi na kusema, "Nitauza kila ktu."

351 Mtu fulani alikimbia kuja, hapa juu, hivi majuzi, kutoka Carolina ya Kaskazini, kabla tu hatujaondoka. Naye akasema,

"Mungu atukuzwe. Waweza kuniambia alipo *mtu fulani* mashuhuri?"

Nami nikasema, "La."

352 "Loo! ndiyo, bwana," kasema, "mtu huyu ana . . . " Kasema, "Mtu huyu ni raisi wa Misheni ya Kanda."

Nikasema, "Ati nini?"

Akasema, "Misheni ya Kanda."

Nikasema, "Sielewi."

Ndipo akasema, "Ee," kasema, "mtu huyu ni rais."

Nikasema, "Ulisema jina lake lilikuwa nani?"

353 Akasema, "Branham, ninadhani. Kitu kama hicho, Brown au Branham."

Nikasema, "Vema, jina langu ni Branham."

Yeye akasema, "Je, wewe ni rais wa Misheni ya Kanda?"

Nikasema, "La, bwana."

Akasema, "Vema, uko wapi ule Utawala wa Miaka Elfu?"

Nikasema, "Sijui."

354 Akasema, "Mbona, wewe u-. . . U—unataka kusema hu—hu—huo kwamba unaendelea papa hapa, nawe huna habari za hayo?"

Nikasema, "La, bwana, sina."

355 Akasema, "Vema, Mungu atukuzwe! Kasema, "Nina—nina baadhi ya marafiki fulani waliokuja wakaniambia," na wakasema, "nimeacha kazi." Alikuwa yungali amevaa nguo zake za kazi. Kasema, "Ndugu, nataka huo Utawala wa Miaka Elfu."

356 Nami nikasema, "Vema, ni—ninaamini umechanganikiwa kidogo, sivyo, ndugu?"

357 Kwenye kama wakati huo gari moja likaja, teksi. Mwanamke akasema, "Simama! Simama! Simama!" Maskini mwanamke mmoja akaja pale, akasema, "Sasa utamwombea mume wangu."

Nikasema, "Ndiyo, mama. Kuna—kuna nini?"

358 Akasema, "Vema, nasikia inakubidi ungoje mwezi mzima kwa mtu kuwa na mazungumzo ya faraha, unaona, upate kuombewa."

Nami nikasema, "Ati nini?"

359 Naye akasema, "Ndiyo, bwana." Kasema, "Lakini mimi nimedhikika tamaa. Huna budi kumwombea mume wangu."

Nikasema, "Hakika. Yuko wapi? Mlete."

360 Jamaa huyu akiwa amesimama pale, akitazama, akasema, "Je! unawaombea na wagonjwa, pia?"

Nikasema, "Naam, bwana."

361 Kasema, "Ulisema jina lako lilikuwa ni nani, Branham?" Nikasema. . . "Nawe hujui lo lote kuhusu ule Utawala wa Miaka Elfu?"

362 Nikasema, "Vema, mimi. . . La, sijui." Nikasema, "Si— sielewi na jambo hilo. Uko tu hapa katika Biblia."

363 Akasema, "La, uko unaendelea sasa hivi. Watu wamekuja kutoka kila mahali."

Nikasema, "Uko wapi?"

Akasema, "Jeffersonville, Indiana, papo hapo chini ya daraja."

364 "Bwana, umenishangaza sana." Ndipo nikasema, "Sijui lo lote juu yake." Nikasema, "Hebu tuingie ndani na tuketi chini. Labda tunaweza kutatua jambo hili." Tukalitatua, unaona.

365 Msininii, msininii, mnaona, enyi wapendwa, msitamani huduma kamwe. Mnajua ninalomaanisha. Unaona? Utakuwa na furaha zaidi tu ukiwa mahali ulipo. Unaona? Endelea tu kusonga mbele.

215. Baada ya kule Kunyakuliwa kwa Bibi-arusi, je! ni lini kanisa, ambalo ilibidi lipitie katika kipindi cha ile Dhiki, litakaposimama hukumuni? (Halitasimama hukumuni. . .) **Je! ni kabla au ni baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu?**

Kwa ajili ya "kanisa." Loo! samahani. Niwie radhi, wewe uliyeliandika hili. "Ni lini kanisa ambalo. . . "

Baada ya kule Kunyakuliwa kwa Bibi-arusi, je, ni lini kanisa, ambalo lililolazimika kupitia katika wakati wa ile Dhiki, litakaposimama hukumuni? Je! ni baadaye ama ni kabla. . .?

366 Baadaye! "Hao wafu waliosalia hawakuwa hai hata itimie ile miaka elfu," wale ambao hawakwenda pamoja na Bibi-arusi. Hebu tuone.

216. Umesema mara nyingi ya kwamba Ukomunisti uliinuliwa na Mungu, kutimiza kusudi Lake, kama vile Mfalme Nekadreza. Sasa je! ukomunisti unaingiaje kwenye picha ambayo ita-. . . hatimaye utaninii. . . utafanya hivyo? Mwisho wake ni nini? Wanachuoni wengi wanaamini ya kwamba katika Ufalme wa Kaskazini, Gogu na Magogu uliotajwa katika Maandiko, utashuka kupigana na Israeli katika ninii—katika ninii. . . (siwezi kusoma hayo. Naam. Naam.) **Naamini, kati ya. . . baadhi ya kanda zilizorekodiwa, zilisema, ulisema mwishowe huo utaangusha ninii. . . ya kwamba Ukomunisti mwishowe utaangamiza Ukatoliki, au Vatican, kwa mlipuko. Hiyo ni kweli?**

367 Ndiyo. Ufunuo 16, utapata jambo hilo, na ufunuo 18:8 na 12. Ikiwa mtu huyo yuko hapa, anataka kuchukua kipande hiki

cha karatasi, kuhusu jambo hilo, unaweza kulichunguza moja kwa moja. Naam. Unaona, "Ole, ole, mji ule ulio mkuu! Kwa kuwa katika saa moja mwisho wake umekuja." Unaona, wafanyi biashara, na wengine wote, walioleta bidhaa. Itatendeka. Hiyo ni kweli. Na usi-. . .

368 Acha tu, sahau tu kuhusu Ukomunisti. Unaona? Si kitu cho chote ulimwenguni ila kundi la—la watu ambao si kitu ila washenzi wasio—wasiomcha Mungu. Ni mfumo fulani. Hebu niwaonyeshe jambo fulani, niwaonyeshe tu jinsi ilivyo rahisi. Mbona, ni asilimia moja tu ya Urusi iliyo Ukomunisti. Wanahitaji mjumbe. Unaona? Asilimia moja; basi, asilimia tisini na tisa yao wangali upande wa Ukristo. Asilimia moja, basi asilimia moja wanawezaje kuwatawala asilimia tisini na tisa? Hilo lapaswa kukuelezea wewe, papo hapo. Kama Mungu hakuruhusu jambo hilo, mbona, vema, wangelipinduliwa zamani sana. Unaona? Hakika.

217. Ndugu Branham, ulisema kwamba Rumi ingeitwaa serikali ya Wayahudi katika ile maiaka mitatu na nusu ya mwisho. Hiyo itakuwa ile—ile miaka mitatu na nusu ya kwanza ya ile Dhiki, au itakuwa ile mitatu na nusu ya mwisho? Hii ni kweli?

369 Itakuwa ni ile miaka mitatu na nusu ya mwisho. Hiyo ni kweli. Si ya kwanza, kwa sababu imekwisha pita.

Nina moja zaidi baada ya hili:

218. Ndugu yangu mpendwa, je! yule Eliya wa Malaki 4:5 atakwenda jangwani, kama vile Wafalme wa Kwanza 17 inavyotwambia yule Eliya Mwingine alifanya?

370 Vema, nisingesema hasa kuwa yeye angeenda, ya kwamba angeenda jangwani. Lakini yeye atakuwa hili, unaona, Yeye alikuwa. . .Elisha na Eliya, je! umetambua? Watu wengi kama hao ni watu wanaojitenga; wao, wanajitenga na watu. Wao ni wa kipekee sana. Hawashirikiani sana na watu.

371 Unatambua jinsi Elisha alivyokuwa, na Eliya, na Yohan Mbatizaji, na tabia ya roho hiyo, unaona. Nao hawaninii. . . Yeye—yeye, ninaamini mtu huyo atakuwa mpenda nyika, na labda atakaa nyikani. Lakini, sasa, kusema tu yeye atakuwa anayeishi peke yake na kuishi mwituni, sijui kuhusu hilo. Wakati mwingine walikaa huko. Elisha hakukaa, lakini Eliya alikaa. Na halafu tena, Yohana, yeye—yeye aliishi nyikani.

372 Na, ni vigumu kusema, manabii hawa wengine, watakapotokea huko Uyahudini, sijui watakaa wapi. Huenda wakapiga kambi huko mlimani mahali fulani. Ama—ama, yale watakayofanya katika siku za unabii wao, si—sijui watakayofanya.

Lakini ninyi. . . Yale ninayojaribu kusema ni haya. "Wao, wao wataninii, wao watakuwa wa—wa—wa-. . . " Wanajaribu kuuliza, "Je! watakuwa tu ni watu wanaoishi nyikani?"

373 Vema, itawabidi waende kaskazini mwa British Columbia wapate nyika ya kutosha kuishi huko basi, mahali fulani, unaona. Kwa hiyo itakuwa ni mtu fulani. . . Misitu yote imekatwa. Unaona? Hakuna misitu mingi sana. Unaona? Kwa hiyo, jambo pekee, wao—wao wanaweza kuwa wapenda nyika, unaona, na wakae labda wakati mwingi nyikani, watakuwa. . . Waweza kutambua tabia yao, ni ile ya kutokupatana, unaona, na u—utajua jambo hilo hapo litakapokuja. Unaona? Utaliona; ukiwa—ukiwa tu macho sana.

374 Sasa, hapa hapa kuna moja, sijui jinsi ya kuligusia. Na nina lingine kabla tu ya hili, na halafu nitawaomba wafunge kinasasauti kwa muda kidogo.

219. Ikiwa Mungu yu nafsi moja, mbona au angewezaje kujizungumzia Mwenyewe katika ule Mlima wa Kugeuzwa Sura?

375 Vema nimekwisha kueleza hilo, unaona. Unaona? Ningependa kukuuliza hili. Nita-. . . Wakati Yesu alipoomba kwa Baba, unaona.

[Ndugu Branham anaanza kuzungumza na ndugu fulani katika kusanyiko—Mh.] Ninaamini una Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sivyo, ndugu? Je! waweza kusimama kidogo? Unadai kuwa una Ubatizo wa Roho Mtakatifu? [Huyo ndugu anasema, "Ndiyo, bwana."] Na mimi ninao, pia. Basi, hicho ni nini? Basi sidai kwamba nina—nina nguvu ndani yangu ya kufunua siri hizi. Sina nguvu za kuwaponya wagonjwa. Ni Mungu.

376 [Ndugu Branham anaendelea kuzungumza na ndugu huyo katika kusanyiko—Mh.] Ninaamini wewe ni Mhudumu. Kama sijakosea, umetoka Arkansas. Vema, sasa. Na ndani yako-, una, mna—mna kuhubiri Injili. Kwa ujumla, wewe ulilelewa shambani na mahali kama hapo. Hujui cho chote kuhusu jambo hilo; lakini kitu Fulani kiliingia ndani yako, kuhubiri Injili. Hudai kwamba hicho ni wewe, hata kidogo. Hicho ni Mtu mwingine, aitwaye Roho Mtakatifu. Sivyo? ["Ndiyo, bwana."] Sawa.

377 [Ndugu Branham anaendelea kuzungumza na ndugu huyo katika kusanyiko—Mh] Sasa nataka kukuuliza. Huyo. . . Roho Mtakatifu huyo hukaa ndani yako. Ni kweli? [Huyo ndugu anasema, "Hiyo ni kweli."] Je! wewe huongea Naye? ["Naam, bwana."] Unanena naye? Unamwomba? Vema. Hayo tu ndiyo ninayotaka. Asante, sana.

Sasa, mna lipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."]

378 Nitawauliza kitu kimoja. Ilikuwaje ya kwamba wakati. . . Yesu, katika Injili ya Yohana 3, alisema, "Mwana wa Adamu

atakapokuwa, aliyeko sasa Mbinguni." Unaona? "Sasa yu Mbinguni; ataru-. . .atakuja duniani." Unaona? "Mwana wa Adamu aliye sasa Mbinguni," naye alisimama papa hapa akinena na yule mtu. Sasa nijibu hilo. Yesu na Baba walikuwa ni Mtu yule yule mmoja.

379 Ni sawa sawa tu na vile Roho Mtakatifu alivyo ndani yangu; mnaniangalia mimi nikihubiri, lakini si mimi.

Si mimi ninayeweza kunena neno linaloweza kuleta, kama mjuavyo, mnyama fulani; niketi pale na kumwangalia, na kumwua yule mnyama na kumla. Hiyo ni nguvu ya uumbaji. Haliko katika uweza wa binadamu

380 Si mimi ningeweza kumchukua mvulana mdogo hapa, anayelala . . . Madaktari wamemlaza chali, akiugua ugonjwa wa moyo, usiku huu. Na kusema, "William Branham asema hivi"? La! "BWANA ASEMA HIVI, imekwisha." Na kumrudisha kwa daktari, kesho yake, na umekwishaondoka kabisa.

381 Mtoto aliye na lukemia, mpaka macho yake yamebenuka, na ni manjano mwili mzima, na tumbo lake; mpaka wanampeleka hospitalini, kumpa damu na kadhalika, wapate hata kumfikisha hapa. Na katika muda wa dakika tano, alilie sambusa! Na kumrudisha tena kwa daktari, kesho yake, na hata asiweze kupata dalili yake yo yote. Je! hilo ni "William Branham asema hivi?" Hilo ni "BWANA ASEMA HIVI!" Hata hivyo, Yeye yu nafsi tofauti na mimi, lakini njia pekee anavyojidhihirisha ni kupitia kwangu. Unaona?

382 Hivyo ndivyo Yesu na Baba walivyokuwa. Yesu alisema, "Si mimi nizitendaye hizo kazi; ni Baba Yangu aishiye ndani Yangu."

Sasa, "Mwana wa Adamu atapaa kutoka Mbinguni, ambaye sasa yuko Mbinguni." Unaona? Ilikuwa ni nini? Yeye alikuwa yuko kila mahali kwa sababu Yeye alikuwa ni Mungu.

383 Sasa, hili lingine, mimi . . . [Ndugu Branham anadata kidole chake mara moja—Mh.] Nataka kusema maneno haya.

Eleza ulichokuwa unazungumzia . . .

[Nafasi tupu kwenye kanda. Ndugu fulani anazungumza katika kusanyiko.]

Asante, Ewe Baba Mungu. Twakushukuru kwa ajili ya Roho, ya kuwaepo Kwako hapa. Nasi tunaambiwa, Baba, ya kwamba wakati mmoja, a—adui alipoingia, na Roho alimshukia mtu fulani na akamtabiria, na kumwambia. Iliweka mambo sawasawa, mahali ambako ambapo walijua jinsi ya kwenda na kumshinda adui, na ambapo wangempata adui.

384 Nami nakushukuru, Baba, ya kwamba Wewe unadumu Mungu yeye yule ambaye umekuwa daima. Ungali u yeye yule. Sisi hubadilika, na nyakati hubadilika, na majira hubadilika, na watu. Lakini Wewe hubadiliki kamwe. Taratibu Zako ni zile

zile. Neema yako ni ile ile. Kazi zako ni zile zile, kwa maana ni za ajabu, na zimepita sana maarifa yo yote ya mwanadamu kufahamu kamwe.

385 Kwa hiyo twakushukuru, Bwana, ya kwamba siri Zako zimefichwa mioyoni mwa watumishi Wako. Nasi tunafurahi sana kwa ajili ya jambo hili, Bwana. Na jalia twende kama Mianga inayong'aa, ku-. . .toka mahali hadi mahali, na kujaribu, kwa upendo, ku—kuwaleta wengine; ili tupate kuvua kila pembe iliyo ndogo, na kushusha wavu, tupate kuwa na hakika tutapata kila samaki aliye Wako. Ndipo Mwana-Kondoo atamchukua Bibi-arusi Wake, awe daima ubavuni Pake. Tunaungojea wakati huo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

386 Ni wagonjwa wangapi walio humu, hebu tuone mikono yenu. Vema, inaonekana kuwa kama . . . Inueni mikono yenu juu tena. Ni kama moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini . . . [Ndugu Branham na mtu mwingine wanaendelea kuhesabu polepole mikono iliyoinuliwa—Mh.] Arobaini na saba, kama arobaini na saba. Vema.

387 Ni saa tano na nusu. Tunaweza kuwaombea wagonjwa sasa hivi; kufanya usiku huu uwe—uwe . . . Hivi mngetaka, kufanya jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

388 Ninaamini wakati huu sasa ungekuwa unaofaa wa kufanya jambo hilo. Nitawaambia kwa nini: Roho Mtakatifu, anayesimama papa hapa ndani, anatutia mafuta. Sasa, kulingana na vile tumeingia katika Roho huyo sasa, naona, nanyi unaona kwamba kitu Fulani, mnajua ya kwamba kitu Fulani—kitu Fulani kiko hapa, manaona. Na kama tu ungaliweza kupata kuamini, unapaswa kuamini sasa hivi. Unaona? Kama kuna uwezekano wa wewe kuamini, ni sasa.

389 Sasa, tunataka mje kwa utulivu sana. Na hebu wale walio katika marefu yale ya kanisa *pale*, walioinua mikono yao, waingie katika marefu *haya* ya kanisa, kisha waende *hivi*. Na ndipo tutawachukua, marefu ya kanisa kwa marefu ya kanisa. Nao ni arobaini na tano tu—arobaini na tano, arobaini na saba kati yao; haitachukua muda mrefu sana.

390 Nitamwomba Ndugu Neville kama atakuja, asimame papa hapa pamoja nami, na tutawaombea.

391 Kwanza, wale wanaoingia sasa katika marefu ya kanisa, hebu simameni tu kwa muda kidogo sasa, ili tuweze kuwaombea ninyi hapa, na kumwekea mikono kila mtu. Sasa, hiyo ni kweli, kila mtu tu atakayeingia katika mstari wa maombi, unaona, hao watakaoingia katika mstari wa maombi. Unaona? Sasa—sasa, unaona, kuokoa wakati, ili tuwe na hakika ya kulipata, tutawaombea sasa.

392 Angalieni, enyi marafiki. Sasa hebu niwaelezee. Yesu Kristo alisema hivi, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Sasa angalia. Yeye hakusema kamwe, "Kama wakiwaombea." "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya!" Na kama Mungu aweza kuchukua ugonjwa usiotibika wa lukemia, na msichana mdogo asiyeweza kuwa na imani kwa ajili yake mwenyewe, na kufanya kitu hicho kizima kabisa; kama anaweza kuchukua ugonjwa huo mwingine, mvulana mdogo mpenzi, na kumponya kabisa hata madaktari hawawezi kupata homa ya yabisi baridi katika damu yake ama cho chote kile; Yeye anaweza kukufanyia nini? Sasa, hawa watoto wadogo, hawaelewi maombi yangekuwa ni nini. Lakini niliwawekea tu mikono, na ikatendeka. Tunaweza kulielewa.

Sasa, wakati mnaposimama, kuomba sasa.

393 Baba wa Mbinguni, uwepo Wako mkuu ukiwa hapa, yule Roho Mtakatifu mkuu, Yule tuliye na picha Yake, Yule tunayesoma habari Zake katika Biblia, Yeye yuko hapa hivi sasa. Anajifunua Mwenyewe katika mwili wa mwanadamu.

394 Jinsi tumemwona Yeye pasipo kukosea hata wakati mmoja, kwa miaka mingi, kuweza kufunua mawazo hasa ya moyo wa mwanadamu, kufunua dhambi waliyotenda, kuwaambia hasa yale yaliyotendeka na itakavyokuwa, pasipo kukosea hata wakati mmoja! Ndipo, tunajua ya kwamba Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na wa Israeli, yungali ni Mungu, katika utu wa Yesu Kristo.

395 Na sasa kwa Roho Wake anayeshuka kutoka Mbinguni, chini ya Damu iliyomwagika Kalvari, akishuka kati ya watu, ili kujidhihirisha Mwenyewe katika mwili wa kibinadamu kabla tu ya kuteketezwa kwa ulimwengu; Roho Mtakatifu aliye mkuu akiwakilishwa katika mwili wa kibinadamu. Wale watu wa thamani ambao wameukubali ule upatanisho wa ile Damu, na Roho Mtakatifu anatwaa nafsi zao; Mungu, aliyewakilishwa katika mwili wa kibinadamu.

396 Kwa hiyo, haitakuwa ni mwili wa kibinadamu, kutenda tu lile tendo, kama katika ubatizo au mengineyo, kwa agizo ya kwamba, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Kwa kuweka mikono juu ya wagonjwa, Roho Mtakatifu angehakikisha ya kwamba wamepona, kama wakiamini. Sasa, Baba, tunajua ya kwamba mambo haya ni kweli.

397 Watu hawa wanaosimama, watapitia chini ya mikono ya wahudumu ambao wamempokea huyu Roho Mtakatifu, nao wako tayari, Bwana, kuweka mikono yao juu ya wagonjwa. Nasi tunajua, Baba, ya kwamba kama watu hawa wataamini tu! Kama tu vile ulivyoahidi katika kila Neno, halina budi kutukia, vivyo hivyo . . . Na haliwezi kutukia pasipo imani, kwa kuwa haiwezekani kumpendeza Mungu pasipo imani. Kamwe hatuwezi kumpendeza.

398 Na sasa kwa imani, na tukiamini, kukiwako na ahadi hii mbele yetu, na huku Mihuri ya Biblia ikifunguliwa kwetu, ya kwamba Mungu hutimiza Neno Lake! Jalia hawa watu wapendwa, walio wagonjwa, Bwana, . . . na kuwahurumia kwangu, kama mwanadamu katika mwili unaopatikana na mauti kama miili yao ilivyo. Na sasa ninii yao . . . Roho Mtakatifu yule yule aishiye ndani yetu, Bwana, anakaa ndani yao. Nasi tunahurumiana. Na tukijua ya kwamba lile agano jipya katika Damu mpya . . . Kama lile la kale lilitoa uponyaji, litafanyaje zaidi sana hili "jipya na lililo bora?" Baba, na iwe hivyo, ya kwamba watu hawa hawatakosa, bali watapata uponyaji wao wanapopitia chini ya mikono ya watumishi Wako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

399 Sasa—sasa, tutaninii, upande *huu* utaketi, wakati upande *huu* unakuja. Na ndipo upande *huu* utarudi, na upande huo mwingine . . . Sasa, baadhi yenu ninyi ndugu hapa, mtakaosimama. Ninaamini ninyi mlio upande huu ni wahudumu, ninyi nyote upande huo.

Yuko wapi Daktari, Ndugu Ned? Ulikuwa unataka kuingia kwenye mstari wa maombi, Ndugu Ned? [Ndugu Ned Iverson anasema, "Ndiyo. Ninaingia kusimama kumwakilisha mtu mwingine."—Mh.] Vema, Ndugu Ned. Vema. Mara tu utakapokwisha kuombewa, ingia mstarini moja kwa moja.

400 Sasa, hebu hawa walio upande huu *hapa*, waketi tu kidogo, nami nitawachukua wale walio upande *huu*. Ndipo, ndipo tutashuka na kuchukua marefu ya katikati ya kanisa, na kuwarudisha kwa upande *huu*. Ndipo tuchukue marefu *haya* ya kanisa, na kuwarudisha kupitia upande *huu*, nasi tutamwombea kila mtu.

401 Nitamwomba Ndugu Teddy . . . Yuko wapi? [Ndugu Teddy Arnold anasema, "Papa hapa."—Mh.] Vema. Nataka upige kinanda hapo, "Ni Tabibu wa Karibu." Na wapiga piano, po pote walipo, waungane naye, ikiwezekana."

402 Sikilizeni, mnakumbuka ule wakati ambapo huo ulikuwa unapigwa, na mvulana mmoja mdogo akaletwa jukwaani? Yule msichana mdogo wa Kiamishi akipiga, "Ni tabibu wa karibu." Alikuwa na nywele ndefu, nyeusi; au—au nywele za rangi ya shaba, hasa, msichana wa Kimenonaiti au Kiamishi, mojawapo, zimelala nyuma ya kichwa chake.

403 Ndipo Roho Mtakatifu akamshukia mvulana huyo mdogo, kwa kumwekea tu mikono; miguu imelemaa. Ndipo akaruka kutoka kwenye mikono yangu, na kukimbia katikati ya jukwaa. Mama yake akasimama, kisha akaanguka chali; jambo la kwanza, yeye, ninaamini ni Mmenonaiti.

404 Ndipo Roho wa Mungu akamshukia msichana huyu mdogo wa Kimenonaiti, ama wa Kiamishi, cho chote alichokuwa. Baba yake pamoja na hao wengine wakiwa wameketi pale,

wamevaa. . .wamevaa nguo zao, kama Wamenonaiti, ama vyo vyote vile ilivyokuwa. Naye akaruka kutoka kwenye lile piano, ameinua mikono yake juu hewani. Ndipo nywele nzake zuri zikamfunika usoni; alionekana kama Malaika. Akaanza kuimba katika Roho; na alipokuwa akifanya hivyo, lile piano likiendelea kupiga, "Ni Tabibu wa karibu, Tabibu wa ajabu."

405 Kila mtu amesimama hapo, maelfu, wakitazama na kuona dota za kinanda zikienda juu na chini, "Ni Tabibu wa karibu, Tabibu wa ajabu." Watu walisimama kutoka kwenye viti vya kusukumia wagonjwa, wakatoka kwenye susu, machela, wakaanza kutembea.

406 Bwana Yesu yuyo huyo yuko papa hapa, asubuhi ya leo, kama tu vile alivyokuwa wakati ule. Aminini tu sasa.

Piga wimbo huo, tafadhali: *Ni Tabibu wa Karibu*.

Sasa hebu kila mtu na aombe.

Hebu wao watembee kupitia katikati ya chumba, waende moja kwa moja upande *huu*, na moja kwa moja hadi kwenye kiti chako ama po pote unakotaka kwenda, unapoenda zako. Huko nyuma ni wazi? Vema. Kwa hiyo, rudini moja kwa moja kwenye kiti, halafu tutasimama.

407 Sasa sikilizeni. Hawa wanapoombewa, waombeeni. Ndipo utakapokuwa unaombewa, watakuombea.

Sasa, ninyi wahudumu mlio hapa, simameni. Nami nawatakeni mwawekee mikono hawa wanapopita.

408 Sasa, kila mtu, huku vichwa vimeinamishwa, na mwendelee kuinamisha vichwa vyenu. Endeleeni kuomba. Na mnapopita, ndipo mnawekewa. . .mikono. Kumbukeni, ni ahadi ya Mungu inayofunua zile siri za Kitabu Chake, siri za moyo wa mwanadamu. Yeye ni Mungu atakayethibitisha hayo, mkiamini. Unaona? Sasa kila mtu aombe.

Sasa ninyi ndugu wahudumu simameni hapa, mkitaka.

Vema, na tuinamishe vichwa vyetu.

409 Sasa, Bwana Yesu, watu hawa wanapokuja, nguvu za Mwenyezi Mungu na zihuishe imani yao mara wanapopitia hapa, yote katika Jina la Yesu.

410 Sasa, sawa, hebu mstari na uanze namna *hii*. Mwulize kila mtu, wawekeeni mikono, ninyi wahudumu, wanapopita.

411 [Ndugu Branham na wahudumu wanaanza kuomba na kuweka mikono yao juu ya kila mtu anayepitia kwenye mstari wa maombi, huku mwenye kinanda akiendelea kupiga *Ni Tabibu wa Karibu*—Mh.]

Katika Jina la Bwana Yesu!

Naiweka mikono yangu, katika Jina la Bwana Yesu, ndugu yangu.

Katika Jina la Bwana Yesu!

Mungu, mjalie dada yangu, Rosella, katika Jina la Yesu.

Katika Jina la Yesu Kristo!

Katika Jina la Yesu Kristo!

412 [Ndugu Branham anazungumza na mtu fulani, "Wewe ngoja, angalia jambo hilo mpaka mstari utakapokwisha."—Mh.]

Katika Jina la Bwana Yesu! . . .?. . .

Kumbukeni, Yeye ni mnyenyekevu. Njoni kwa unyenyekevu.

413 [Maneno ya Ndugu Branham hapa yanasikika tu kwa sehemu, wala hayatoshi kuchapisha wazo kamili lililotamkwa. Mstari wa maombi unaendelea hapa kwa dakika sita na sekunde ishirini na tano—Mh.]

414 [Mahali patupu kwenye kanda. Ndugu Billy Paul Branham anaenda kwenye maikrofoni na kusema, "Enyi watu mwaweza kusonga nyuma, tafadhalini? Ninyi watu mnaosimama kwenye marefu *yale* ya kanisa, mwaweza kuondoka kwenye marefu hayo ya kanisa hapo na mrudi nyuma? Endeleeni kurudi nyuma, tafadhalini. Asanteni. Ninyi watu mlio kwenye marefu ya katikati, mnaweza kuzunguka, pia?"—Mh.]

415 [Maneno ya Ndugu Branham hapa yanasikika tu kwa sehemu, wala hayatoshi kuchapisha wazo kamili lililotamkwa. Mstari wa maombi unaendelea hapa kwa dakika mbili na sekunde ishirini—Mh.]

Pokea kuponywa kwako, ndugu, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, Ndugu Mitchell.

Pokea kuponywa kwako, ndugu, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, dada, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea uponyaji, dada, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, dada, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, ndugu, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, dada, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, dada, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, ndugu, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, ndugu, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, ndugu, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, dada, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, dada, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, ndugu yangu, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, dada, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, dada, kutoka kwa Yesu Kristo.
Pokea kuponywa kwako, ndugu yangu.
Pokea kuponywa kwako kutoka kwa Yesu Kristo.
Pokea kuponywa kwako, ndugu, kutoka kwa Yesu Kristo.
Pokea kuponywa kwako, ndugu, kutoka kwa Yesu Kristo.
Pokea kuponywa kwako, ndugu, kutoka kwa Yesu Kristo.
Pokea uponyaji wako.
Pokea uponyaji, dada, kutoka kwa Yesu Kristo.
Pokea uponyaji, dada.
Pokea uponyaji dada, kutoka kwa Yesu Kristo.
Pokea kuponywa kwako, dada, kutoka kwa Yesu Kristo.
Pokea kuponywa kwako, ndugu, kutoka kwa Yesu Kristo.
Pokea uponyaji wako, dada yangu.
Pokea uponyaji, ndugu.
Pokea uponyaji wako, dada . . .?. . .
Pokea uponyaji wako, dada . . .?. . .
Pokea uponyaji wako, ndugu.
Pokea uponyaji wako.
Pokea uponyaji wako, ndugu . . .?. . .
Pokea uponyaji wako, dada . . .?. . .
Pokea uponyaji wako kutoka kwa Yesu Kristo.
Pokea uponyaji wako.
Pokea uponyaji, dada . . .?. . ., kutoka kwa Yesu Kristo.
Pokea uponyaji.
Pokea uponyaji . . .?. . .
Pokea uponyaji, ndugu yangu, kutoka kwa Yesu Kristo.
Pokea uponyaji.
Pokea uponyaji, dada . . .?. . .
Pokea ule uponyaji, katika Jina la Yesu Kristo.
Pokea ule uponyaji, katika Jina la Yesu. Amina.
Pokea uponyaji.
Pokea uponyaji.
Pokea uponyaji wako.
Pokea uponyaji wako.
Pokea uponyaji wako kutoka kwa Yesu Kristo.

416 [Ndugu Billy Paul Branham anaenda kwenye maikrofoni na kusema, “Kuna mtu mwingine anayetaka kuwa kwenye mstari wa maombi? Waombwa kuingia, tafadhali. Kama kuna mtu

mwingine ye yote anayetaka kuwa kwenye mstari wa maombi, unaombwa kuingia, tafadhali."—Mh.]

Pokea kuponywa kwako, ndugu yangu, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, dada, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, ndugu, kutoka kwa Yesu Kristo.

417 Pokea kuponywa kwako, Dada Woods, kutoka kwenye mkono wa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako . . .?. . .

Pokea kuponywa . . .?. . .

418 Pokea uponyaji, Dada Roberson, kwa mkono wa Yesu Kristo.

Pokea uponyaji, ndugu yangu, kwa mkono wa Yesu Kristo.

Pokea uponyaji, dada . . .?. . ., kutoka kwenye mkono wa Yesu Kristo.

Katika Jina la Yesu Kristo, pokea kuponywa kwako.

Mponye, katika Jina la Yesu Kristo.

Pokea uponyaji, dada . . .?. . .

Pokea kuponywa kwako, mwanangu, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, dada, kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, ndugu, kutoka kwa Yesu Kristo.

Ndugu Weerts, pokea kuponywa kwako, ndugu, kutoka kwa Yesu Kristo.

Dada, pokea kuponywa kwako kutoka kwa Yesu Kristo.

Pokea kuponywa kwako, ndugu . . .?. . .

Ndugu, kwa Jina la Yesu Kristo, pokea . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo Bwana wetu, pokea kuponywa kwako.

Katika Jina la Yesu Kristo, pokea kuponywa kwako, ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo, pokea kuponywa kwako, dada.

Katika Jina la Yesu Kristo . . .?. . .

419 [Ndugu Billy Paul Branham anaenda kwenye mikrofoni na kusema, "Hao ndio tu waliotaka kuombewa kwa sasa huu?"—Mh.]

420 [Ndugu Lee Vayle anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Naomba mkono wa Bwana Yesu ukujalie, Ndugu Vayle, ombi hili kwa ajili ya mpendwa wako, katika Jina la Yesu.

421 [Ndugu Billy Paul Branham anaongea na Ndugu Branham—Mh.] Billy Paul, kwa kadiri ya kadi nyingi za ulizosambaza kadi, sasa pokea kuponywa kwako, katika Jina la Yesu Kristo.

> Ni Tabibu wa Karibu,
> Tabibu wa ajabu,
> Na rehema za daima,
> Loo! ni dawa Yake Yesu.

Sote pamoja:

> Imbeni Malaika
> Sifa za Yesu Bwana,
> Pweke limetukuka,

422 Mungu, kwa maskini hawa mume na mke waliomleta, ulimwenguni, mmoja wa…?…Naomba wapate haja yao, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo.

423 …?…la Yesu Kristo, naomba mtu aliye kwenye nia ya dada yetu sasa hivi, naomba nguvu za Mungu ziambatane na haja hiyo. Naomba akombolewe. Tujalie, Bwana. Amina.

424 Bwana Mungu, katika Jina la Yesu, ridhia ombi la mtu huyu. Namwombea, Bwana, kwa maombi yangu. Amina.

425 Loo! hili si ni la ajabu! [Kusanyiko linashangilia na kusema, "Amina."—Mh.] Ninaamini ya kwamba kama kila mtu aliyepitia hapa, asubuhi ya leo, chini ya upako huu mkuu, na—naamini kama utaninii tu…Sasa usitazamie makubwa kwa kitu fulani kikuu. Kumbuka tu jambo rahisi la kuamini yale Yeye aliyoahidi.

426 Sasa hebu sote na tuseme pamoja. Sisi [Kusanyiko linasema, "Sisi"] hatutazamii ["hatutazamii"] jambo fulani kubwa. ["jambo fulani kubwa."] Lakini, katika Jina la Yesu, ["Lakini, katika Jina la Yesu,"] tunapokea ahadi Yake. ["tunapokea ahadi Yake."]

427 Hilo latosha. Hilo linalimalizia. [Kusanyiko linasema, "Amina," na kushangilia kwa sauti kuu—Mh.] Amina! Mungu awabariki!

Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Pili
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume Two)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2001 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org